

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Tisa – Tarehe 12 Aprili, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Swali letu la kwanza asubuhi ya leo linaelekezwa kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na linaulizwa na Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto.

Na. 68

Kukarabati Shule za Msingi na Sekondari - Lushoto

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI aliuliza:-

Serikali imekuwa na utaratibu wa kukarabati shule zake za msingi na sekondari nchini:-

Je, ni lini Serikali itazifanyia ukarabati Shule za Msingi Kwemashai, Bandi, Milungui, Kilole na Shule za Sekondari za Ntambwe, Ngulwi - Mazashai na Mdando?

MWENYEKITI: Ahsante. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Serikali kupitia Program ya Lipa Kulingana na Matokeo (*EPforR*) imepeleka jumla ya shilingi milioni 467 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili, matundu sita ya vyoo na madarasa mawili katika Shule ya Msingi Shukilai (Shule ya Elimu Maalum) na ujenzi wa mabweni mawili Shule ya Sekondari Magamba, ujenzi wa bweni moja na madarasa mawili Shule ya Sekondari Umba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali imetoa shilingi bilioni 29.9 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 2,392 ya madarasa nchi nzima ambapo kati ya fedha hizo Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imepewa kiasi cha Sh.512,500,000 kwa ajili ya kukamilisha maboma 46 ya madarasa shule za sekondari. Serikali itaendelea kukarabati na kujenga miundombinu ya elimu kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali, nimpongeze Rais wangu Mungu azidi kumjaza hekima na maisha marefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja kwamba tumepata fedha zote hizo kama nilivyosema nashukuru lakini bado sekondari nyingi katika Jimbo la Lushoto hazina hosteli

na hii imepelekea watoto wengi kufeli na watoto wengi wa kike kupata ujauzito. Je, Serikali ina mkakati gani sasa tena wa haraka kuhakikisha kwamba wanajenga hosteli katika sekondari ambazo hazina hosteli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wa Jimbo la Lushoto kwa nguvu zao wamejenga majengo ya maabara tena yote matatu lakini mpaka sasa majengo yale hayajamalizika. Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu sasa wa kumalizia maboma yale ili watoto wetu waweze kusoma elimu kwa vitendo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Shekilindi maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Mbunge nimefika kwenye Jimbo lake la Lushoto, wananchi wa eneo lile na yeye mwenyewe wamefanya kazi kubwa kuongeza miundombinu ya elimu lakini pia afya na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anaomba kujua mpango wa Serikali kuongeza hosteli. Katika bajeti ambayo inaendelea kujadiliwa sasa kila mtu akipitia kwenye kitabu cha bajeti cha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, utaona kuna maeneo mbalimbali fedha zimetengwa kwa kazi hiyo lakini iko miradi mingine ya elimu itakayoimarisha hosteli mbalimbali. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avumilie mwaka huu wa fedha tumetenga fedha na kadri zitakavyopatikana tutaweza kumaliza hiyo shida kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusu maboma ya maabara, tumeanza kupeleka vifaa na

kukamilisha maboma katika shule nyingi kadri itakavyowezezana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane huenda shule au maeneo yake anayotaja tutapeleka vifaa vya maabara lakini pia tutamalizia maboma ya maabara hizo. Lengo ni ili tupate wataalamu wa sayansi ili tutakapoanza *issue* ya viwanda tuwe na wataalam wa kutosha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa misingi ya elimu bora, sawa, shirikishi kwa wote, elimu ya msingi inaanzia darasa la ngapi mpaka la ngapi na elimu ya sekondari inaanzia darasa la ngapi mpaka la ngapi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu tunaotumia tuna darasa la awali, darasa la kwanza mpaka la saba, *form one* mpaka *form four* na kidato cha tano na cha sita baadaye elimu ya juu. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hivi karibuni Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa shule za sekondari kongwe ikiwemo Shule ya sekondari ya Mpwapwa lakini mimi nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri mnafanya ukarabati wa shule tu lakini nyumba za walimu

zimechakaa kweli kweli. Je, mna mpango gani wa kukarabati shule na nyumba za walimu?

MWENYEKITI: Ahsante, mna mpango wa ukarabati wa nyumba za walimu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa George Malima Lubeleje (*Senator*), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba tunakarabati shule tu ukweli ni kwamba tumekarabati shule nyingi zaidi kuliko nyumba za walimu. Hata kwenye kitabu cha bajeti tunachojadili sasa ambapo Mungu akipenda tutahitimisha Jumatatu tarehe 15 akipitia kwenye majimbo mbalimbali ataona fedha zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za walimu. Uwezo wa Serikali siyo mkubwa sana, tunaomba Mheshimiwa Mbunge na wadau mbalimbali tushirikiane katika jambo hili kupunguza shida ya walimu katika nchi hii. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Catherine.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa tumeona shule nyingi kongwe zilizotoa viongozi mbalimbali zimekuwa zikikarabatiwa. Kwa Mkoa wangu wa Arusha, kuna Shule ya Arusha Sekondari ambapo miundombinu yake ni mibovu na chakavu. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga pesa kwa ajili ya kukarabati shule hii kongwe ya Arusha Sekondari?

MWENYEKITI: Ahsante, shule kongwe ya Arusha Sekondari.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, msemaji mzuri sana wa Mkoa wa Arusha na Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali kukarabati shule zote kwa wakati mmoja kama ingewezekana lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti jambo hilo halijawezekana, tutakarabati kulingana na uwezo lakini pia kuna vigezo mbalimbali. Kwa hiyo, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge, tufanye tathmini, tumeshamaliza awamu ya kwanza tupo kwenye mpango wa awamu ya pili, huenda kwenye awamu ya tatu Shule ya Arusha Sekondari ikaingizwa kwenye mpango huu wa Serikali wa kukarabati shule hizi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri sambamba na matatizo ya Lushoto, Wilaya ya Busega haikupata mgao wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma. Je Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza ukatoa maelekezo katika mgao huu na Wilaya ya Busega tupate mgao huo?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi, pesa, pesa, pesa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge wa Busega swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natambua kazi nzuri ambayo anaifanya katika Jimbo lake la Busega kuwasemea wananchi wake lakini sina hakika kwa sababu fedha zile zilisambazwa kwenye wilaya zote kwa maana ya Halmashauri inawezekana kwenye Jimbo hilo kuna bahati mbaya. Naomba tuwasiliane baada ya kipindi cha maswali na majibu tuone njia bora ya kumaliza shida hiyo. Ni nia ya Serikali kila Jimbo lipate mgao wa kupunguza shida ya maboma na kuchangia nguvu za wananchi ili wasilalamike.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay,

Mbunge wa Mbulu Mjini na linaelekezwa ofisi hiyo hiyo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na.69

Maboresho ya Mji wa Mbulu

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY atauliza:-

Serikali ina nia njema ya kuuweka Mji Mkongwe wa Mbulu kwenye mpango kabambe wa maboresho ya Mji na Majiji, Mikoa na Wilaya na kwenye Awamu ya Pili ya mpango huo kwa ajili ya miundombinu ya masoko, barabara, vituo vya mabasi na taa za barabarani:-

(a) Kwa kuwa Mji wa Mbulu ni mkongwe toka kuanzishwa kwake, je, ni lini sasa nia hiyo njema itatekelezwa?

(b) Je, mpango huo wa maboresho ya Mji utasaidiaje miundombinu ya barabara za mitaa ya Mji wa Mbulu ambazo ni zaidi ya kilomita 40 za changarawe kwa kuwa ni kilomita 1.8 za lami kwa sasa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatekeleza miradi ya uboreshaji Miji Tanzania ambayo ni *Urban Local Government Strengthening Programme (ULGSP)* na *Tanzania Strategic Cities Project (TSCP)* na Dar es Salaam *Metropolitan Development Project*

(DMDDP) kwa fedha za mkopo nafuu toka Benki ya Dunia. Mpaka sasa miradi hii inatekelezwa katika Majiji 6, Manispaa 19 na Halmashauri za Miji 6. Utekelezaji wa Programu ya Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Miji (*Urban Local Government Strengthening Programme-ULGSP*) ulianza katika mwaka wa fedha 2013/2014 na unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2019/2020. Wakati wa maandalizi ya programu hii, Mji wa Mbulu ulikuwa haujapata hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji na hivyo kukosa vigezo vya kujumuishwa kwenye programu. Serikali itatoa kipaumbele kwa Mji wa Mbulu kwenye awamu nyingine za mradi huu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Miji inajumuisha ujenzi wa miundombinu ya msingi katika miji, kujenga uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuwezesha uandaaji wa mipango kabambe ya uendelezaji wa miji na kuboresha uwajibikaji na utawala bora. Hivyo Mji wa Mbulu ukijumuishwa utanufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu umuhimu wa kuboresha miundombinu ya barabara katika Mji wa Mbulu. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 kupitia fedha za Mfuko wa Barabara, Serikali inajenga barabara yenye urefu wa kilomita 0.4 kwa kiwango cha lami nyepesi (*double surface dressing*) kwa gharama ya shilingi milioni 300 na kazi ya ujenzi inaendelea.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Issaay.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, mpango unaotekelezwa sasa wa kilomita 0.4 ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na kwa kuwa ahadi hii ya Mheshimiwa Rais ni kilomita 5 katika Mji wa Mbulu, nini majibu ya Serikali kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa kuwa Rais atakuwa anataka

ahadi hiyo iwe imetekelezwa na mimi nimeshatimiza wajibu wangu wa kuikumbusha Serikali mara kadhaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ni kweli Mji wa Mbulu ni mji mpya ulioanzishwa lakini ni Halmashauri au Wilaya kongwe katika ya Wilaya kongwe Tanzania. Kwa hivi sasa Mji wa Mbulu una kilomita 1.8 katika mitaa yake kwa kiwango cha lami. Kwa kuwa hali ya barabara na madaraja katika kata kumi ukiacha kata zingine nane za vijijini ni mbaya; na kwa kuwa *TARURA* wanapewa fedha kidogo sana hivyo kushindwa kutekeleza mahitaji yaliyoibuka, nini kauli ya Serikali kuwezesha miundombinu ya barabara katika Mji wa Mbulu pamoja na ahadi hiyo ya Rais?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge Zakharia, Mbunge wa Mbulu Mji maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anauliza kuhusiana na ahadi ya Mheshimiwa Rais, naomba nimhakikishie kwamba hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, kipenzi cha Watanzania, namhakikishia kabla ya 2020 ahadi hii itakuwa imekamilishwa ili Mheshimiwa Rais atakapoenda kuomba kura kwa awamu nyingine kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi, asipate vikwazo kwa wananchi wa Mji wa Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, anapenda kujua tuna mpango gani, nitoe maelekezo kwa *TARURA* Mkoa na Wilaya yake ya Mbulu kama hali ya mji huu ni mbaya kiasi hicho wafanye mchakato walete maandishi hapa tujue namna ya kufanya ili tuweze kuboresha wakati tukisubiri kutafuta fedha nyingi zaidi za kuboresha Mji wa Mbulu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba mipango ya kuendeleza barabara za miji ni pamoja na Mpango wa *DMDP*. Katika Manispaa ya Ubungo mpango wa *DMDP*, unatekelezwa kwa upande wa Jimbo la Ubungo peke yake lakini upande wa Jimbo la Kibamba kwenye Kata sita za Kwembe, Msigani, Mbezi, Saranga, Goba mpango huu hautekelezwi kabisa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua utekelezaji wa mpango wa *DMDP* ili kuzigusa kata sita za Jimbo la Kibamba kwenye masuala ya miundombinu ya barabara?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyika, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mkoa wa Dar es Salaam ikiwepo maeneo ambayo ametaja ya Ukonga na maeneo mengine, tunatekeleza awamu ya kwanza ya mpango ya *DMDP*. Naomba niwahakikishie kwamba itakapokuja awamu ya pili Wabunge watashirikishwa waweze kuainisha maeneo yao ili tupanue wigo zaidi wa kuendeleza Mji wetu wa Dar es Salaam.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mji wa Mafinga ulikuwa Mamlaka ya Mji Mdogo kwa miaka tisa na Julai 2015 ikawa Halmashauri kamili ya mji. Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wana-Mafinga kwamba kwa kuwa Halmashauri ya Mji kamili na wao wameingia katika Mpango Kabambe wa Maboresho ya Miji? Kwa sababu sasa hivi

Mafinga ni Halmashauri ya Mji kamili. Tunataka tu kuhakikishiwa na sisi tunaingia katika awamu ya pili? Kwa sababu ndiyo ukombozi wa barabara zetu?

MWENYEKITI: Ahsante, umeeleweka. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge alikuwa na Mheshimiwa Rais amekubaliwa mambo yake yote manne leo amelala usingizi mnono kabisa. Katika suala hili, kama nilivyojibu swali la Mheshimiwa Zakharia, Mbunge wa Mbulu Mji, tutakapoanza kufanya mchakato miji mipya yote na huo mji wako utaingizwa katika awamu hiyo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, namba 70 linaulizwa na Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Rungwe, linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Mwambalasma, kwa niaba.

Na. 70

Barabara ya Kuunganisha Kata ya Kisondele – Rungwe

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. SAUL H. AMON) aliuliza:-

Hakuna barabara ya kuunganisha Daraja la Nyubati na Kata ya Kisondele hadi Nzunyuke umbali wa zaidi ya kilomita 30 kufika kijiji cha Nyubati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya kuunganisha Kijiji cha Nyubati na Kata ya Kisondele?

MWENYEKITI: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa wananchi wamekuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilometa 30 kwa kuzunguka kutoka Nyubati hadi Nzunyuke kutokana na kukosekana kwa daraja. Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (*TARURA*) umefanya usanifu na tathmini ya ujenzi wa barabara hiyo ambapo kiasi cha shilingi milioni 847.36 kinahitajika ili kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, *TARURA* imetenga kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Nyubati – Lutete yenye urefu wa kilometa 6 inayounganisha Kijiji cha Nyubati na Kata ya Kisondelea.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwambalaswa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa matatizo ya wananchi wa Rungwe kuhusu barabara yanafanana kabisa na matatizo ya wananchi wa Chunya hasa hasa kwa barabara inayotoka Chunya – Kiwanja - Ifumbo - Mjete, ambayo sasa hivi inaunganisha Mikoa miwili ya Songwe na Mbeya; na kwa kuwa Mamlaka ya Wakala wa Barabara (*TARURA*) toka imeanzishwa Chunya hakuna barabara hata moja ambayo wameikarabati. Je, Mheshimiwa Waziri anatoa maagizo kwa *TARURA* ili waikarabati barabara hiyo iweze kupitika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri kijana mchakapa kazi yupo tayari kuongozana name kwenda Chunya ili akaangalie kazi ambazo wanafanya TARURA katika Halmshauri ya Chunya?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kwa barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja na mipango iliyopo na kwa sababu michakato hii inaanzia kwenye ngazi ya Halmashauri, inakuja kwenye Mkoa mpaka ngazi ya TAMISEMI, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane baadaye tupate taarifa sahihi ya eneo hili na tuweke mipango mahususi ambayo inaweza kutatua shida hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anauliza kama nipo tayari. Mimi nipo tayari sana wakati wowote. Tupande ratiba twende tuone eneo hili, turudi kufanya mipango ya kukamilisha na kuondoa kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naipongeza Serikali kwa mradi wake wa kuleta mpango wa *DNDP* kwenye Mkoa wa Dar es Salaam. Jimbo la Ilala tumepata Kilometa mbili tofauti na maeneo mengine wamepata zaidi ya Kilometa 40.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuboresha barabara za kata zote 10 za Jimbo la Ilala ili ziweze kuonekana za kupitika kwa sababu ni katikati ya mji na zinasaidia

kupunguza msongamano katikati ya mji kuelekea pembezoni mwa mji? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna miradi inaendeshwa katika Mji wa Dar es Salaam, UNDP na sasa kilichobaki, baada ya kutengeneza barabara nzuri zaidi, ni vingumu zaidi barabara za pembezoni zikawa nzuri. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Mbunge tupo wote llala na tunampongeza Meneja wa TARURA kwamba ni msikivu sana, tutawasiliana naye tuone mipango iliyopo na sisi tuishi kama Wabunge wa Dar es Salaam ili kuwezesha mipango ya kukamilisha barabara zetu na hasa wakati wa mafuriko watu wa Dar es Salaam wasiweze kupata shida zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mndolwa.

MHE. ZAINABU AMIR MNDOLWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara itaokayo Korogwe kupitia Kwa Mndolwa - Mkaalie - Tamota hadi kuunganishwa na Kiwanda cha Chai Mponde ni takribani kilometa 40 lakini haijajengwa kwa kiwango cha lami. Hii ni barabara muhimu sana katika nchi kwa sababu mazao mengi kutoka Jimbo la Bumbuli ambayo yanasafirishwa kwenda Dar es Salaam hupita pale, lakini wakati wa mvua barabara hii haipitiki kabisa na kuna maporomoko ya mawe:-

Je, ni lini sasa Serikari itajenga hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu la swali hilo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza kuendelea kuwasema

wananchi wa Korogwe, lakini namwomba sana kwa sababu tupo kwenye wakati wa bajeti hii aunge mkono bajeti ya TAMISEMI Jumatatu tutakapofika kwa majaliwa ya Mwenyenzi Mungu tupate fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilijibu swali hapa nikasema, tuliunda timu ya wataalam, inapitia sasa namna ya ku-*identify* hizi barabara ili tuangalie ule Mfuko wa TANROADS na TARURA. Nimesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge kwamba TARURA inafanya kazi nzuri sana. Shida hapa ni fedha. Tukipata chanzo *realible* cha fedha na *formula* ambayo ipo sawaswa na wadau mbalimbali na bajeti ikaungwa mkono. Nia ya Serikali ni kukamilisha barabara zote ikiwezekana kwa kiwango cha lami ikiwepo hiyo ya Korogwe. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Suleiman Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene.

Na. 71

Barabara ya Tabora – Mambali – Itobo-Kagongwa

MHE. SELEMAN J. ZEDI atauliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Tabora – Mambali – Itobo - Kagongwa yenye urefu wa Kilometa 149 utaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Kwani ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na pia imo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 - 2020.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi Uchukuzu na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kutekeleza mpango wa ujenzi wa barabara ya Tabora – Mambali – Itobo – Kagongwa yenye urefu Kilometa 149 kwa kuanzia na hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) wameingia mkataba na Mhandisi Mshauri *NIMETA Consult Ltd.* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Tabora – Mambali – Itobo – Kagongwa kwa gharama ya shilingi milioni 789. Hadi sasa Mhandisi Mshauri amekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na kazi ya usanifu wa kina itakuwa imekamilika kufikia Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, gharama za ujenzi pamoja na maandalizi ya nyaraka za zabuni kukamilika, Serikali itatafuta fedha za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii. Aidha, wakati kazi ya usanifu ikiendelea, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) itaendelea kutenga fedha za matengenezo mbalimbali kwa barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Jumla ya shilingi 345 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kazi hiyo. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongezea Serikali kwa kazi ambayo imefanywa kwenye barabara hii. Kimsingi wakati naandika swali hili, kuliwa hakuna kazi yoyote ambayo imefanyika, lakini sasa hivi nakubaliana kabisa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Mshauri Mhandishi *NIMETA Consult* ameshaanza kazi, nami mwenyewe ni shuhuda nimemwona akifanya kazi hii ya usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba kwa kuwa Serikali imesema kazi ya usanifu wa kina inaisha mwezi Juni, 2019 na hii barabara ni ahadi ya Rais na pia ni jambo ambalo lipo kwenye ilani:-

Je, Serikali inaweza ikatoa kauli hapa kwamba barabara hii kwa kuwa usanifu utakuwa umekamilika mwezi Juni, sasa kwenye bajeti ijayo itatengewa fedha ili Mkandarasi wa kuanza kujenga aanze kazi kabla ya Awamu hii ya Tano haijamaliza muda wake?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditije.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunapokea pongezi kwa moyo wa dhati kabisa lakini napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Selemani Zedi kwa jinsi ambavyo anafuatilia sana kipande cha barabara hii iliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mpango wa Serikali na nia ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara zote nchini kwanza zimepitika na pili zinaunganishwa kwa kiwango cha lami. Nimhakikishie Mheshimiwa Zedi kwamba barabara yake kama tulivyoahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kama ahadi ya Mheshimiwa Rais, tutaijenga kwa kiwango cha lami kabla ya mwaka 2020 kwisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Matiko halafu Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama ilivyo ahadi kwa Jimbo la Bukene, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni zake na hata Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga barabara ya Tarime Mugumu ambayo ni kilometa 89 kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa hii barabara ikijengwa itakuza uchumi siyo tu wa Tarime au Mara, bali wa Taifa, maana yake watalii watakao toka Kenya wataweza kupita kwenye njia ile:-

Ni lini sasa hii ahadi ya Mheshimiwa Rais itatimilika kwa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Tarime Mugumu almaarufu kama *Nyabwaga Road*?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali iliahidi kujenga kipande cha kilometa 44 kutoka Tarime mpaka Mugumu kwa kiwango cha lami. Naamini hata Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba upembuzi yakinifu ulishafanyika, usanifu wa awali ulishafanyika na usanifu wa kina ulishafanyika. Sasa hivi tunatafuta pesa kwa ajili ya kumpa Mkandarasi wa kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekitik, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo, tutajenda hiyo barabara kwa sababu ya umuhimu wa utalii wa nchi yetu kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Magufuli kwa uzinduzi wa barabara ya kutoka Makambako mpaka Mufindijana. Naomba niulize swali moja. Katika ujenzi wa barabara ya kutoka Dodoma - Mtera mpaka Iringa, pale katika kona za Nyang'holo huwa kunakuwa na maporomoko makubwa sana ambayo huwa yanajitokeza hasa wakati wa mvua:-

Je, Serikali inatusaidiaje? Maana kutakuja kutokea ajali kubwa sana, hata jana nimepita pale. Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tayari ameshafika ofisini zaidi ya mara tatu akifuatilia kipande cha barabara hii ya kutoka Mtera - Iringa hasa kwenye kona zile za Nyang'holo ambazo ni korofi kabisa. Tunakiri na bahati nzuri nimeshamwelekeza Meneja wa *TANROAD* Mkoa kufuatilia eneo hilo ili tuanze taribu za kulirekebisha kwa ajili ya usalama wa Watanzania. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mabula Stanslaus.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mji wa Mwanza unaendelea kukua kila siku na miundombinu ya barabara hasa barabara ya Kinyata inayotoka Mwanza Mjini kwenda Usagara hali yake kimsongamano siyo nzuri; na leo nauliza karibia mara ya nne:-

Ni lini sasa Wizara itakuwa tayari kuhakikisha barabara inayotoka Mwanza Mjini kupitia Igogo - Mkuyuni na Butimba - Nyegezi mpaka Buhongwa, inapanuliwa kwa njia nne sasa na kuweza kuwa barabara inayofanana na mazingira halisi ya mji wenyewe? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Jiji la Mwanza linapanuka kwa kasi sana na ni mipango ya Serikali kuhakikisha kwamba Jiji hilo linaundiwa program maalum ya kupanua barabara zake kupunguza msongamano. Namshauri Mheshimiwa Mbunge, baada ya kikao hiki, baada ya kipindi cha Maswali na Majibu, tuambatane naye mpaka Wizarani akaone mipango ya Serikali kuhusu Jiji la Mwanza kurekebisha barabara zake. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gashaza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhandisi Mshauri yupo *site* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Nyakahura - Lulenge – Mulugarama; na kwa kuwa barabara hii ni ya muda mrefu.

Ni lini sasa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utaanza?

MWENYEKITI: Haya, kama utaweza kulijibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Gashaza, ni kwa muda mrefu sana amekuwa akifuatilia hii barabara ambayo naomba niitamke kwa ladha yake; inaitwa Nyakahuura – Kumubuga, inapatia Murusangamba - Lulenge mpaka Murugarama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri anakiri kwamba Mshauri Mwelekezi yupo pale kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na baada ya kumaliza zoezi hilo atafanya usanifu wa awali kisha usanifu wa kina kupata michoro kwa ajili kutambua gharama za ujenzi. Hatua zinakwenda vizuri mpaka sasa hivi. Namshauri Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo. Tukishapata nyaraka zote hizo husika, hiyo barabara itaanza kurekebisha tena kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Na. 72

Utekelezaji Mradi wa Maji Katoro- Buseresere

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa Katoro- Buseresere unaokusudia kutoa maji Ziwa Victoria?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremia Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kutekeleza miradi ya maji ambayo lengo lake ni kufikisha huduma ya maji kwa asilimia 95 ya wakazi wa mijini na asilimia 85 ya wakazi wa vijijini hadi ifikapo mwaka 2020. Malengo hayo yanahusu pia maeneo ya Katoro na Buseresere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa Majisafi kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Katoro na Buseresere ambapo hadi hivi sasa mazungumzo ya awali kati ya Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) na wafadhili kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*EIB*) yamefanyika. *EIB* wameonesha nia ya kufanya mradi wa maji kwa ajili ya miji hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, andiko ya mradi wa maji kwa ajili ya miji ya Katoro na Buseresere limeshawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango ili maombi yaweze kuwasilishwa rasmi *EIB*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bukwimba.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa hatua ambayo imechukua kuweza kuhakikisha kwamba kuna mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria, Katoro, Buseresere. Wananchi wanahitaji kujua ni lini utekelezaji utaanza rasmi?

Swali la pili; kwa kuwa azma ya Serikali mpaka mwaka 2020 ni kuhakikisha kwamba mijini asilimia 95 ya maji, asilimia 85 vijijini, jambo ambalo nikiangalia hali halisi, kwa mfano katika Mkoa wa Geita Jimbo la Busanda, naona hali iko chini sana. Napenda kujua sasa kwamba nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunapata maji kwa asilimia 85 katika Jimbo Busanda na asilimia 95 Mji wa Geita ambapo sisi wananchi wote ni Makao Makuu ya Mkoa wetu wa Geita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Lolesia kwa kazi nzuri sana ya kuwapigia wananchi wake. Kubwa, tunatambua kabisa maji hayana mbadala. Ndiyo maana sisi kama Wizara ya Maji tumefanya jitihada ya kuwasilisha hili andiko kwa Wizara ya Fedha ili waweze kuwasilisha *E/B*. Wizara ya Maji itafanya ufatiliaji wa karibu katika kuhakikisha jambo hili linakamilika kwa wananchi wake ili mradi uweze kuanza kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mwanamama ndoo kichwani na kutimiza Ilani ya Chama cha Mapinduzi asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini na asilimia 95 ya upatikanaji mijini, tumeshakamilisha miradi zaidi ya mitatu katika Jimbo lake. Moja, Nyakagongo, Luhuhu pamoja na Mharamba katika kuhakikisha wananchi wale wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati uliokuwepo sasa hivi ni katika kuhakikisha tunakamilisha mradi wa zaidi ya shilingi bilioni nne wa Nachankorongo ili mradi ule ukamilike kwa wakati na umeshafikia zaidi ya asilimia 90 upo katika muda tu wa matazamio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa na la msingi kabisa, sasa hivi tunakamilisha mradi wa Lamugasa na tunajenga mradi wa maji Nkome, Nzela ambao ni wa zaidi ya shilingi bilioni 25 katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji katika miji 25 katika mpango wa kutatua tatizo la maji, Mkoa wa Geita tumeuangalia kwa ukaribu zaidi na tunafanya jitihada kubwa ya kutatua tatizo la maji. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Kwa kuwa Bwawa la Yongoma, katika Mto wa Yongoma lilikuwa-*designed* na Serikali ya Japan kupitia *JICA* tangu 2012; na kwa kuwa mwaka huu 2018/2019 liliwekwa kwenye bajeti kwamba lijengwe, Serikali inatoa tamko gani kuhusu ujenzi wa bwawa hili?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo, kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Kaboyoka. Kubwa ambalo nataka niseme ni utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Nia ya Serikali bado ipo pale pale, na sisi kama Wizara tunaendelea kuhakikisha fedha hizi zinapatikana ili bwawa lile liweze kujengwa na wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mji wa Liwale ni Mji unaokua kwa haraka sana na una chanzo kimoja tu cha maji; na kutokana na mabadiliko ya tabianchi, chanzo kile hakitoshelezi tena. Je, ule mradi wa kutafuta chanzo mbadala cha maji kwa Mji wa Liwale, umefikia wapi?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, mpango huo umefikia wapi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, lakini na pili nimepata nafasi ya kufika katika Jimbo lake la Liwale. Pamoja na jitihada kubwa za Serikali zinazofanyika lakini kiukweli, Liwale kuna changamoto. Sasa sisi kama Wizara tulishawaagiza watu wetu wa rasilimali za maji katika kuhakikisha wanafanya utafiti wa kina ili tuweze kupata chanzo cha uhakika, tuweze kubuni mradi mkubwa ambao kwa ajili ya kutatua kabisa tatizo la maji Liwale. Nataka nimhakikishie sisi tutalifanya jambo hili kwa haraka ili wananchi wake wa Liwale waweze kupata maji ya uhakika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Willy Qambalo.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Miradi ya maji katika Vijiji vya Matala, Kansay, Buger, Endonyawet na Getamock Wilayani Karatu chini ya mpango wa *WSDP* imejengwa chini ya kiwango na hivyo haifanyi kazi, karibu shilingi bilioni nne zimetumika na haziwanufaishi wananchi. Tulimwomba Mheshimiwa Waziri mara nyingi aje Karatu ili aje atatue tatizo hilo...

MWENYEKITI: Uliza swali sasa.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba awaambie wananchi wa vijiji hivyo ni lini atakwenda ili kutatua changamoto za miradi hiyo? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, binafsi nilishapata taarifa za Karatu na nimefika, lakini kubwa kuna miradi ambayo imefanyiwa ubadhirifu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Viongozi wa Wizara tumesha-*note* na tumekubaliana tutakwenda katika maeneo yale yote na wale walioshiriki katika ubadhirifu ule, lazima fedha watazitapika na hatua kubwa kali tutazichukua.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Mradi wa bomba la Ziwa Victoria umeshafika katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, lakini usambazaji katika Kata nyingi bado haujafanyika, Kata ya Mwenda kulima, Kagongwa, Iyenze, Isagee maji hayajafika. Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza maji ya Ziwa Victoria ili wananchi waweze kunufaika? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza tutambue jitahada kubwa zilizofanywa na Serikali, tunatambua kabisa tulikuwa na changamoto kubwa sana, katika Mji wa Kahama na Shinyanga na Serikali ikaona haja sasa ya kuyatoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya kutatua matatizo haya ya maji, kikubwa maji yale yamekwishafika lakini imebaki changamoto tu ya usambazaji. Hivyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge, wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani, sisi tumekwishawaita Wakurugenzi wote na tumekwishawaagiza katika mapato yao wanayoyakusanya watenge asilimia katika kuhakikisha wanasambaza maji kwa wananchi ili waweze kupata maji safi salama na yenye kuwatosheleza.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba anijibu swali langu la nyongeza. Mheshimiwa Waziri alifika katika Kata ya Ruaha Mbuyuni na akaona jinsi matatizo ya maji yanavyosumbua. Wananchi wamekuwa wakipata kipindupindu kila mwaka na yeye aliahidi mambo makubwa. Sasa je, ni lini wananchi wa Ruaha Mbuyuni ambao wanategemea kupata kituo cha afya watapata maji pale?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Mbunge wa Kilolo, Mzee wangu, kwa kazi kubwa sana anayoifanya, lakini tulipata nafasi ya kufika Ruaha Mbuyuni. Changamoto kubwa tuliyoiona kwa Wahandisi wetu walitengeneza tenki la maji lakini hawakuwa na chanzo cha maji. Kwa hiyo tuliwaagiza watu wa rasilimali za maji wa bonde lile waende na wameshafanya tafiti kikubwa tunawaagiza watu wa *DDCA* waende kuchimba kisima haraka katika kuhakikisha mradi ule unafanya kazi kwa wakati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ongezeko la watu na hasa Jiji la Dodoma limekuwa kubwa baada ya Makao Makuu kuhamia Dodoma, je, Serikali ina mpango kabambe au mkakati gani wa kuhakikisha kwamba maji ya Ziwa Victoria yaliyofika Tabora yanafika Dodoma kuwasaidia wananchi wa Dodoma kutokana na upungufu wa maji?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Bura kwa swali lake zuri sana, sisi kama Wizara ya Maji tunatambua kabisa sasa hivi kumekuwa na ongezeko kubwa sana katika Mkoa huu wa Dodoma, lakini jitihada kubwa ambazo tulizozifanya sasa hivi, uzalishaji wetu zaidi ya lita milioni 55, lakini mahitaji lita kama milioni 44. Kwa hiyo, tuna maji kwa kiasi kikubwa, kubwa ambalo tunaloliona hapa ni suala zima la usambazaji, lakini itakapobidi tutafanya kila jitihada katika kuhakikisha tunatatia tatizo la maji na wananchi wa Dodoma wasipate tatizo hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kutokana na shida kubwa ya maji hapa nchini, Bunge hili lilitengeneza, liliunda Wakala wa Maji, sasa ningependa kujua, je, tayari, Serikali imeshatengeneza kanuni za huo Wakala na kama zitagawiwa kwa Wabunge?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Kanuni ziko tayari na lini zitagawiwa.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilipongeze sana Bunge lako Tukufu kutokana na jitihada kubwa walizofanya kupitisha Muswada wetu, pia kwa namna ya kipekee tumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Baada ya Bunge kupitisha Muswada ule, Mheshimiwa Rais ameshasaini na imeshakuwa Sheria, sisi kama Wizara ya Maji, tutazileta kwa haraka kanuni zile ili tuanze utekelezaji kwa haraka sana. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda nimuulize Waziri, kwa kuwa kuna mradi mkubwa wa maji kutoka Nyamtukuza katika Wilaya ya Nyang'hwale, kupita Kakora, Kitongo, Kiangala, Kharumwa, Izunya hadi Bukwimba ambao umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu, lakini Serikali ikiwa ikitoa pesa. Je, ni lini sasa

mradi huu utakamilika na namwomba Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili aende akauone mradi huo kwa nini unaendelea kusuasua?

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Kubwa pamoja na mradi huo, lakini tumeshalipa zaidi ya bilioni moja na milioni mia saba *certificate* yake kwa Mkandarasi anayedai, ili mradi usikwame.

Kuhusu kusuasua kwa mradi, sisi kama Wizara ya Maji, Wahandisi ama Wakandarasi wababaishaji tutawaweka pembeni, nataka nimhakikishie kabla ya Bunge tutakwenda Nyang'hwale katika kuhakikisha tunaenda kuukagua mradi ule na ikibidi kama Mkandarasi hana uwezo wa kutekeleza mradi huo tutamwondoa mara moja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge nimetumia muda mrefu kwa swali hili kwa sababu nafahamu changamoto ya maji tuliyonayo nchini.

Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 73

Kupandisha Hadhi Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

MHE. KIZA H. MAYEYE (K.n.y. MHE. HAMIDU H. BOBALI)
aliuliza:-

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni cha muda mrefu na pia kimetumika kuandaa viongozi wa nchi yetu na nchi jirani:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kukipandisha hadhi Chuo hicho kuwa Chuo Kikuu?

(b) Je, kwa nini Serikali haipeleki fedha za maendelo katika Chuo hicho kama zilivyopangwa?

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa niaba, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA - K.n.y. WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali Mbunge wa Mchinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni Taasisi ya Elimu ya juu iliyoanzishwa na Sheria Na.6 ya mwaka 2005. Chuo kinatekeleza majukumu yake makuu kuendesha mafunzo ya Kitaaluma katika fani ya Sayansi ya Jamii katika ngazi za Cheti, Stashahada, Shahada ya Kwanza na umahiri. Aidha, Chuo kinaendesha mafunzo ya Uongozi, Maadili na Utawala Bora, Mafunzo ya Elimu ya kujiendeleza, kinafanya tafiti na kinatoa ushauri kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Serikali kwa sasa si kupandisha hadhi Vyuho vilivyopo, bali ni kuboresha mazingira ya Vyuho Vikuu vilivyopo kwa kukarabati na kujenga miundombinu, kwa kuwa na vifaa vya kisasa na kuwa na Wahadhiri wengi zaidi wenye Shahada ya Uzamivu. Hatua hizo zitawezesha kuongeza nafasi za Udahili na kuimarisha ubora wa elimu itolewayo. Jitihada zinazofanyika katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kupata wataalam zaidi katika fani zenye uhaba ambapo Chuo kimepeleka wataalam 33 kwenda kusoma Shahada za Uzamivu; na

(ii) kuongeza miundombinu ya Chuo kama vile ujenzi wa vyumba vya madarasa na kumbi za mihadhara ambapo, ujenzi wa ukumbi wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 330 kwa wakati mmoja umekamilika na kuzinduliwa tarehe Mosi Aprili, 2019.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikipeleka fedha za maendeleo katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kadri fedha hizo zinavyopatikana, mfano mwaka 2017/2018, Serikali ilitoa fedha zote zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya maendeleo kiasi cha shilingi Biloni 1 nukta 89 ambazo zilitumika kukamilisha ujenzi wa hosteli ya wanafunzi, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiza Mayeye.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini ningeomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Chuo hiki cha Mwalimu Nyerere kilijengwa na Wazalendo wa nchi hii, tena kabla ya Uhuru na Mwalimu Nyerere alikipa jina ya Kivukoni lenye maana ya eneo lililopo Chuo kilipo. Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kukipandisha hadhi Chuo hiki kuwa Chuo Kikuu, ili tumuenzi Baba wa Taifa, ukizingatia kwamba Barani Afrika kuna nchi nyingi ambazo wamezipa majina ya Waasisi kama Mandela *South Africa*, Kenyata Kenya lakini Nkurumah Ghana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Chuo hiki, Mheshimiwa Waziri kuna bweni ambalo limejengwa toka mwaka 2013 kwa ajili ya wanafunzi hawa wa Shahada ya Uzamivu, lakini mpaka sasa halijakamilika. Je, ni kwa nini halijakamilika na ni lini litakamilika na nini kauli ya Serikali katika kukamilisha bweni hilo. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa niaba.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA - K.n.y. WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kiza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza linaenda kwenye majibu ya swali langu la msingi, tumesema mpango wa Serikali kwa sasa si kupandisha hadhi Vyuo. Vilevile tukubaliane kwamba ili kupandisha Chuo kuwa na level ya Chuo Kikuu, kuna vitu vingi inabidi kuzingatia, kwanza inabidi uunde Kikosi kazi cha Wataalam waende wapitie Mitaala, aina ya Walimu kama wanatosha, eneo lenyewe Hatimiliki ya eneo lao. Kwa hiyo kuna vitu vingi vya kuangalia, lakini kwa sababu tunazungumza kuna vitu vingi vya kufanya, tumesema tuboresha hivi vilivyopo, itakapofika wakati, Serikali ikaona haja ya kufanya hivyo, tutafanya hivyo kwa kuzingatia taratibu na sheria za nchi ambazo zimewekwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, anasema kuna bweni ambalo halijakamilika, naomba hili tulichukue tulifanyie kazi, lakini kwa kweli kama kuna bweni lipo pale na kuna upungufu wa mabweni, tutafanyia kazi ili liweze kukamilika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Halima Bulembo.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, wote tunatambua jambo kubwa linalotuweka Watanzania pamoja ni kutokuwa na ubaguzi, lakini mikopo ya wanafunzi wa Chuo Kikuu imekuwa ikitolewa kwa ubaguzi. Mfano, mimi nimepata *division one* nasoma Feza, mwenzangu kapata *division one* anasoma Msalato, atakayepewa mkopo ni yule anayetoka Msalato kwa maana ya kwamba wa Feza ni wa kishua, wa Msalato ni maskini, huu ni ubaguzi wa hali juu, tunajua *hustles* zinazotumiwa na wazazi kuwapeleka watoto wao shule nzuri tu na si kwamba wana pesa nyingi sana. Je, Wizara itakubaliana na mimi umefika wakati sasa wa kubadilisha

kigezo cha kupata mikopo na kigezo kikuu kiwe ni ufaulu wa mwanafunzi badala ya kwamba huyu ana mahitaji zaidi ya mwenzie? Nashukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, nimekuona Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Halima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi vigezo vilivyowekwa ni hasa vinazingatia hali halisi ya uhitaji wa mwanafunzi kwamba mwanafunzi mwingine hana uwezo. Kwa hiyo kama hana uwezo ndiyo atakayesaidiwa kwanza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nnauye.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya msingi, kwenye swali la Kivukoni, mimi ni moja ya *product* ya Kivukoni. Kwa kuwa historia ya Chuo hiki kilikuwa ni Chuo cha ku-*train* Viongozi na kutokana na changamoto tunazoziona katika utekelezaji wa majukumu yao hasa Viongozi kwenye *Local Government*, wilayani, Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kukirudishia chuo hiki kazi yake ya msingi ya kufundisha viongozi *skills* za namna ya kutekeleza majukumu yao kwenye maeneo yao na nakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kutokukipandisha hadhi badala yake tukibadilishie sasa majukumu kitoke kwenye ku-*train social sciences* kiende

kwenye ku-*train* viongozi wetu kwa sababu kwa kweli changamoto ya utekelezaji wa majukumu yao kwenye maeneo yao imekuwa ni kubwa sana?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NASERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA - K.n.y. NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba nimjibu Mheshimiwa Nape Nnauye swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba Chuo hiki kimeanzishwa kwa majukumu aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge na yataendelea kufanyika hivyo, sasa kama kuna upungufu umeonekana, hilo ni jambo la kulichukua na kwenda kulifanyia kazi, lakini tunaamini kwamba kazi ya msingi iliyoanzishwa kwayo inaendelea kufanyika. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Susan Peter Massele, Mbunge wa Viti Maalum na bado linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo, kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 74

Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Umma katika Mkoa wa Mwanza

MHE. SUSAN P. MASSELE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo Kikuu cha Umma au Vyuo Vikuu vya Umma vyenye hadhi ya juu katika Mkoa wa Mwanza?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa niaba.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NASERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA - K.n.y NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Peter Massele, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu katika kuandaa rasilimali watu itakayochangia katika kufikia azma ya Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Kwa sasa Serikali inatekeleza Mpango wa kuboresha Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu zilizopo kwa kukarabati na kujenga miundombinu mipya pamoja na kuongeza vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia ili kuongeza nafasi za udahili na kuimarisha ubora wa elimu itolewayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa tuna idadi ya Vyuo Vikuu 11, Vyuo Vikuu vishiriki viwili na Taasisi za Elimu ya juu 32 zinazotoa Elimu ya juu nchini. Mkoa wa Mwanza una matawi ya Taasisi ya Elimu ya juu za Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*), Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*). Aidha, Mkoa una Tawi la Chuo kikuu Huria cha Tanzania (*OUT*) mbali na Vyuo Vikuu vya Mtakatifu Augustino na Chuo Kikuu cha Afya na Tiba Bugando ambavyo vinamilikiwa na taasisi binafsi. Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu ni za Kitaifa ambapo hupokea wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaboresha mazingira vya Vyuo vilivyopo lakini kama itaona kuna umuhimu wa kuongeza Vyuo vingine itafanya hivyo katika maeneo yatakayoonekana yanafaa. Wito wangu kwa wananchi wa Mkoa wa Mwanza na maeneo mengine ni kuendelea kutumia Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu zilizopo katika Mkoa wa Mwanza. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Massele.

MHE. SUSAN P. MASSELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Serikali, ya Waziri, ambayo yanavunja moyo kabisa, kwa sababu hawajatoa *commitment* ni ni lini watamaliza huo ukarabati na ukizingatia Vyuo hivyo alivyovitaja viko kwenye hali mbaya sana na ukizingatia pia Jiji la Mwanza, ni Jiji ambalo linakua kila siku. Vyuo vingine viko uchochoroni kabisa ambapo ni mazingira mabaya kwa wanafunzi na Wakufunzi katika kufanya kazi. Sasa katika majibu haya nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, mwaka jana tuliona Serikali kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Nchini (*TCU*) ikivichukulia hatua Vyuo Vikuu binafsi ambavyo havikuwa na vigezo vya Vyuo Vikuu na kuviacha Vyuo Vikuu vya Umma ambavyo vilevile vilikuwa havina vigezo vya kuwa Vyuo Vikuu kama alivyojibu kwenye swali la msingi. Je, Waziri haoni kwamba zoezi hili lilikuwa linagandamiza Vyuo Vikuu vya binafsi ambavyo vinatoa nafasi kubwa kwa wanafunzi ambao wamekosa nafasi kwenye Vyuo vya Umma na kupata nafasi?

MWENYEKITI: Sema tu *straight*.

MHE. SUSAN P. MASSELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina ndoto ya Tanzania ya Viwanda ni lini sasa itajenga, *Polytechnic College* katika Mkoa wa Mwanza, ambapo itatoa ujuzi kwa ajili ya mahitaji ya viwanda ukiachilia mbali Chuo cha ... (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, inatosha. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa niaba.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Susanne Maselle, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba zoezi hili lililofanyika lilikuwa la ugandamizi na ndiyo maana vyuo ambavyo vilionekana vina matatizo havijalalamika, vimetii masharti, vimeboresha vyuo vyao na wale ambao wamekamilisha wamekabidhiwa kuendelea kufanya kazi. Kwa hiyo, hii siyo kweli lakini na vyuo vya umma pia vinazingatia utaratibu na ubora wa elimu kwa kadri ya miongozo iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, tumesema nia ya Serikali si kuanzisha vyuo kila mkoa bali ni kuhakikisha vyuo vilivyopo vinaendelea kuboreshwa kwa kuongeza miundombinu na wataalam waliobebea katika nyanja hizo. Vikiimarishwa vinatosha kutoa wataalam kwenye viwanda na kubaki na kutumia utaalam wao nje ya nchi yetu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Na. 75

Kuvipatia Umeme vijiji vya Jimbo la Mpwapwa

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Katika Jimbo la Mpwapwa Vijiji vya Mkanana, Nalamilo, Kiboriani, Igoji Kaskazini, Mbori, Tambi, Nana, Majani (Mwenzele), Mafuto, Kiegea, Kazania, Chimaligo, Mbugani, Chilembe, Mazaza, Mwanjili, (Makutupora) na Chibwegele havina huduma ya umeme:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia huduma ya umeme vijiji hivyo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Mgalu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya vijiji 31 katika Wilaya ya Mpwapwa vitapatiwa umeme kupitia Miradi ya Umeme Vijijini inayoendelea. Kupitia Mradi wa *REA III* Mzunguko wa Kwanza unaoendelea jumla ya vijiji 14 vitapatiwa umeme. Hadi sasa Vijiji vya Mbori, Tambi, Mnase, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mpwapwa, Kimangai na Chunya Sekondari vimepatiwa umeme kupitia Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini (*REA III*) Mzunguko wa Kwanza unaoendelea kutekelezwa hivi sasa na mkandarasi Kampuni ya *A2Z Ifra Engineering Limited* kutoka nchini India. Kazi za mradi katika Wilaya ya Mpwapwa zinahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 9.45, njia za umeme wa msongo kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 68, ufungaji wa transfoma 34 za kVA 50 na 100, pamoja na kuunganisha umeme kwa wateja wa awali 1,148 na gharama za mradi ni shilingi bilioni 2 na milioni 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vilivyosalia ikiwa ni pamoja na Mkanana, Ngalamilo, Kiboriani, Nana, Majami, Mafuto, Kiegea, Kazania, Chimaligo, Mbugani, chihembe, Mazaza, Mwanjiri na Chibwegerea vitapatiwa umeme katika Mzunguko wa Pili wa Mradi wa *REA III* unaotarajiwa kuanza Julai, 2019 na kukamilika Juni, 2021. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa *line* inayopeleka umeme Wilaya ya Mpwapwa inahudumia pia Wilaya za Chamwino, Kongwa, Gairo na Mpwapwa yenyewe na hivi karibuni *line* hiyo imeongezwa Tarafa ya Mwitikila, Mpayungu na Nagulo. Kwa hiyo, *line* hii imekuwa *overloaded* na kusababisha kukatikakatika kwa umeme

katika Mji wa Mpwapwa. Je, mko tayari kujenga *line* mpya ya umeme kuanzia Zuzu *Main Station* itakayopita Kikombo *Station*, Kiegea mpaka Mbande ambako mtajenga *substation* na pale ijengwe *line* moja kwa moja kuelekea Mpwapwa itakayojulikana kama Mpwapwa *fider*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa vijiji vya Mima, Sazima, Igoji Mbili, Isalaza, Chamanda na Iwondo tayari vinapata huduma ya umeme lakini mkandarasi aliruka Kijiji cha Igoji Moja na tatizo la sasa ni transfoma. Je, uko tayari kupeleka transfoma katika Kijiji cha Igoji Moja ili wananchi wa pale waweze kupata huduma ya umeme? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Waziri Wizara ya Nishati, kwa kifupi tu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Lubeleje kwa kufuatilia masuala ya nishati kwa wananchi wa Mpwapwa, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lubeleje la kwanza, ni kweli umeme unaokwenda Mpwapwa unatoka Zuzu ambapo ni umbali wa kilomita 120 ni mbali sana. Mpango uliopo ni kwamba sasa hivi Serikali kupitia *TANESCO* tumeanza utekelezaji wa kujenga *line* mpya ya kutoka Zuzu kupita Kikombo ambapo ni kilomita takribani 42 na kutoka Kikomo mpaka Msalato kilomita 45 lakini kwenda Mpwapwa tutatoa sasa Kikombo kupita Kiegea kutoka Kiegea tunajenga *substation* Mbande na pale Mbande kwenda mpaka Mpwapwa itakuwa takribani kilomita 70. Kwa hiyo, wananchi wa Mpwapwa sasa wataanza kupata umeme kutoka Mbande ambao utakuwa ni mkubwa kuweza kuwahudumia wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili, ni kweli tumepeleka umeme kwenye vijiji takribani 32 Mpwapwa lakini viko vijiji vya Mkanana, Mbande pamoja na maeneo aliyoyataja kama Igoji Moja au Igoji Kaskazini, nimpe taarifa

Mheshimiwa Mbunge Igoji Kaskazini au Igoji Moja wakandarasi wameanza kazi tangu juzi na kufikia Jumapili ijayo watawasha umeme na watafunga transfoma nne za kilovoti 50 na kilomita zingine mbili wataweka na kufunga transfoma mbili za kilovoti 120 na wataunganisha wateja wa awali 78 wa *phase one* na wateja 9 wa *phase three*. Kwa hiyo, Igoji itakwenda kuwashwa umeme Jumapili ijayo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Na. 76

Kuwajengea Uwezo Wakulima na Wafugaji

MHE. DAIMU I. MPAKATE (K.n.y. MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO) aliuliza:-

Idadi ya watu nchini inazidi kuongezeka sambamba na ongezeko la mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo wakulima na wafugaji ili kuendeleza shughuli zao kwa tija na kuwaondolea adha wanazozipata?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu

ufugaji bora na uzalishaji wa malisho kupitia mashamba darasa ili kuwajengea uwezo wa kufuga kwa tija pamoja na kuendeleza malisho katika maeneo yaliyotengwa. Lengo la kutoa elimu hii ni kuhakikisha wafugaji wanaachana na ufugaji wa kuhamahama na kutulia kwenye eneo moja lenye malisho yaliyoboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya mashamba darasa 265 yameanzishwa katika Halmashauri mbalimbali nchini ambapo wafugaji wanaweza kujifunza jinsi ya kuzalisha mbegu na malisho bora ya mifugo ili kuongeza upatikanaji wa uhakika wa mbegu na malisho ya mifugo. Aidha, katika mwaka wa 2018/2019, Serikali imeongeza hekta 2,500 katika mashamba yake kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu za malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepanga kutoa mafunzo rejea kwa wafugaji na Maafisa Ugani nchi nzima juu ya ufugaji bora unaozingatia ukubwa wa ardhi iliyopo. Mafunzo hayo tayari yameanza kutolewa katika Halmashauri ya Simanjiro, Mkoani Manyara na Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Mkoani Tabora na kuendelea kutolewa kwa awamu katika Halmashauri zote nchini. Aidha, Serikali imeendelea na juhudi za kuwasaidia wafugaji kukabiliana na tatizo la maji kwa ajili ya mifugo kwa kuchimba malambo 1,381 na visima virefu 103 katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mawaziri nane iliyoundwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kutafuta suluhu ya migogoro ya matumizi ya ardhi iliyoko nchini tunaamini itakuja na mapendekezo chanya ambayo yatapelekea kuondoa migogoro na adha zinazowakabili wafugaji na wakulima nchini.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mpakate.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba itatoa mafunzo kwa wafugaji na Maafisa Ugani katika Halmashauri zetu, je, ni lini itatoa mafunzo hayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ambayo wafugaji wanaongezeka kwa kasi kubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imetenga maeneo kwa maana ya vitalu vya wafugaji mbalimbali vinavyofikia 100; na kwa kuwa wakulima wengi wameshapewa maeneo hayo lakini mpaka sasa hawajaenda. Nini kauli ya Serikali kuhusu hawa wafugaji ambao wameshindwa kwenda kwenye maeneo yale ya wafugaji na kuendeleza migogoro na wakulima mbalimbali kwa mifugo yao kula mazao ya wakulima? Ahsante? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Naibu Waziri Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni lini tutakwenda kupeleka mafunzo haya Wilayani Tunduru? Naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba timu yetu iliyoko Kaliua ikitoka huko itakwenda Tunduru na Halmashauri zingine katika nchi yetu kwa ajili ya kutoa elimu hii kwa wafugaji na Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili analotaka kujua ni namna gani na tunatoa kauli gani kwa wale waliopata vitalu. Kwanza nataka niwapongeze sana viongozi wote wa kule Wilayani Tunduru kwa kazi kubwa waliyoifanya ya mfano ya kuandaa vitalu wao wenyewe Halmashauri na kuvigawa kwa wafugaji kwa ajili ya kufanya kazi ya ufugaji iliyo na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kauli ya Serikali ni kama ifuatavyo: Wafugaji wote waliopewa vitalu hivi na wakaacha kuvitumia kwa wakati, tunawapa tahadhari kwamba

watanyang'anywa na watapewa wafugaji wengine walio tayari kufanya kazi hii kwa ufanisi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awamu ya Kwanza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Baba wa Taifa alisambaza mitamba bora katika maeneo yote ambayo yanafanya *zero grazing*. Kwa kuwa ni muda mrefu sasa na *cross breeding* imeshafifisha mazao yale ni lini sasa Serikali itaweza kuboresha na kutawanya mitamba bora, vifaranga bora vya kienyeji na vifaranga bora vya samaki katika maeneo ya wafugaji kama Kilimanjaro ambapo kuna wanawake wengi sana ambao ni wafugaji?(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza swali ni zuri sana juu ya Serikali kuhakikisha kwamba tunasambaza mitamba bora kwa wafugaji hasa akina mama wa Mkoa wa Kilimanjaro na Taifa zima. Progamu hii Serikali tunayo kupitia mashamba yetu ya mifugo yaliyosamba nchi nzima tunafanya kazi hii. Kwa mfano tu ni kwamba hivi karibuni kupitia dirisha letu la sekta binafsi tumewawezesha Ushirika wa Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa Mkoani Tanga yaani TBCU, wamekopeshwa pesa na Benki yetu ya Kilimo ili waweze kununua mitamba bora 300 ambapo kufikia tarehe 30 ya mwezi huu mitamba ile itaenda kusambazwa kwa wafugaji wote wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tuko tayari kuhakikisha kwamba na wafugaji wengine kote nchini wanapata fursa hii. Shime wafugaji wote wa ng'ombe wa maziwa, kuku hata wale wa samaki wajiunge katika vikundi

ili waweze kutumia fursa hii inayopatikana kupitia dirisha letu la ukopeshaji la Benki ya Kilimo.

MWENYEKITI: Ahnsate. Swali letu la mwisho kwa leo linaulizwa na Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Na. 77

Serikali Kuunga Mkono Tamko la Kilimo Ndio Uti wa Mgongo

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono tamko la Kilimo ndiyo Uti wa Mgongo wa Taifa kwa vitendo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Jimbo la Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Serikali inatambua na inaunga mkono tamko la Kilimo ni Uti wa Mgongo kwa Taifa. Umuhimu wa sekta ya kilimo unajidhihirisha katika viashiria mbalimbali vya kiuchumi na kijamii kama vile mchango wa kilimo katika ajira, pato la Taifa, usalama wa chakula na malighafi za viwandani. Takribani asilimia 65.5 ya wananchi wameajiriwa katika sekta ya kilimo, asilimia 28.7 ya pato la Taifa hutokana na sekta ya kilimo, mazao ya chakula huchangia kiasi cha asilimia 65 ya pato la Taifa litokanalo na kilimo. Zao la mahindi huchangia zaidi ya asilimia 20 ya pato la Taifa litokanalo na kilimo, mazao ya

chakula na biashara yanachangia asilimia 70 ya kipato katika maeneo ya vijijini. Aidha, sekta ya kilimo ni muhimu katika mikakati ya kuendeleza sekta ya viwanda nchini kwa kuchangia takribani asilimia 65 ya malighafi za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo mikakati na mipango inayolenga kuimarisha sekta ya kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo pamoja na kuwapatia wakulima masoko ya uhakika. Sera, mikakati na mipango inayotekelezwa ni pamoja na Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya II (*ASDP II*) pamoja na sera, mikakati na mipango mingineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jitihada madhubuti ya kutambua Kilimo ndiyo Uti wa Mgongo ni kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*TADB*) ambayo inatoa mikopo ya riba nafuu ya asilimia 8 tu. Aidha, Serikali imeendelea kupunguza ada, tozo na kodi katika kilimo, kuimarisha huduma za utafiti ikiwa ni pamoja na kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (*TARI*) na kuimarisha ushirika ili uweze kuwezesha na kusimamia masoko ya mazao ya kimkakati.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la MKUKUTA na Ilani ya Chama cha Mapinduzi sekta ya kilimo ilikuwa ikue kwa asilimia 8 ndani ya miaka 10 lakini uhalisia kuanzia mwaka 2011 na 2015 sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 3.4. Ndani ya miaka ya Awamu ya Tano katika miaka yake mitatu ya bajeti sekta ya kilimo imekua kwa wastani wa asilimia 1.9. Uhalisia unajionesha kwenye bajeti zake, bajeti ya mwaka 2016/2017...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 tulitenga shilingi bilioni 101 katika sekta ya kilimo lakini fedha iliyotoka ilikuwa ni shilingi bilioni 3 peke yake. Pia mwaka 2017/2018 tulitenga shilingi bilioni 150 ikatoka shilingi bilioni 24. Swali, hii ndiyo tafsiri ya Kilimo ni Uti wa Mgongo katika Taifa letu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wote tunajua kwamba Watanzania wengi wanaohitimu vyo vikiu katika Taifa hili ni 800,000 lakini watu ambao wanaajiriwa kwenye sekta rasmi karibu watu 20,000 tu ambapo 780,000 wanakwenda kuajiriwa kwenye sekta ya kilimo. Hata hivyo, sekta ya kilimo kumekuwa na tatizo la uwekezaji, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wahitimu hawa wanapewa mikopo ili wajajiri na wainue maisha yao pamoja na kuchangia pato la Taifa? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, kwa kifupi Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashungwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwakajoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza Mheshimiwa Mwakajoka anasema kwamba sekta ya kilimo imekua ikikua kwa asilimia ndogo kinyume na matarajio. Pamoja na mipango mizuri ya Serikali katika kukuza sekta ya kilimo nchini lakini kuna mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri *productivity* ya kilimo nchini. Hata hivyo, Serikali inayo mipango madhubuti kupitia Mpango wa Kilimo wa *ASDP II* kama nilivyotaja kwenye majibu yangu ya msingi, kuhakikisha tunatumia ardhi vizuri kwa kilimo, tunazingatia matumizi mazuri ya utumiaji wa maji ili kwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji yaani *drip irrigation* pamoja na mikakati mingine ambayo tumeiweka ndani ya Serikali kupitia Mpango huu wa Maendeleo ya Kilimo wa *ASDP II*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa Mwakajoka ni kwamba tuna vijana wengi ambao

wanahitimu kwenye vyuo vikuu lakini kuna changamoto ya ajira; na wanaoenda kwenye kuajiriwa kwenye sekta ya kilimo ni wachache, asilimia ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali katika hili ni kuhakikisha tunaleta mageuzi ya kilimo na kufungamanisha kilimo na viwanda. Kama unavyojua Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge, Serikali inaendelea kufanya jitihada hizi kuangalia kilimo kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, asilimia 65 ya malighafi za viwandani zinategemea mazao yetu ya kilimo. Sasa mkakati wa Serikali ni kuongeza hizi asilimia ili tuweze kufungamanisha uchumi wa viwanda na kilimo.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ndiyo huo mnauona wote.

Wageni wetu waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika, wageni 30 wa Mheshimiwa Spika waliokuja kwa ajili ya Semina kuhusu Masuala ya Albino wakiongozwa na Ndugu Delivinus Mosha. Hebu msimame wageni wetu hao; karibuni sana ndugu zetu. Nitakuja kusema baadaye Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo mahsus kwa hilo. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ni viongozi kutoka Benki ya *CRDB* ambao ni Dkt. Bennett Bankobeza, Mkuu wa Huduma za Serikali *CRDB* Makao Makuu; mwingine ni Ndugu Suzan Shuma, Meneja Mwandamizi Serikali za Mitaa *CRDB* Makao Makuu na watatu ni Ndugu Chabu Miswaro, Mkurugenzi wa Tawi la *CRDB* Dodoma. Huyu ni maarufu, mnamfahamu sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tuna wageni 32 wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge, ambao ni wafanyakazi wa *EFM Radio* na *ETV* na wafanyakazi wa Benki ya *NBC* wakiongozwa na Mheshimiwa Mohammed Lukwili, Meneja Mkuu wa *EFM* na *ETV* pamoja na Ndugu Jesca Mwanyika, Meneja Mawasiliano na Matukio ya *EFM* na *ETV* na Ndugu Hellen Mzava, Meneja Rasilimaliwatu katika vituo hivyo.

Wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Naibu Spika ni kutoka *National Bank of Commerce (NBC)* ambao ni Meneja Mawasiliano Sekta ya Umma *NBC Bank* Ndugu Pascas Mhindi na Kaimu Mkurugenzi Wateja Binafsi *NBC Bank* Ndugu Gaudence Shawa. Karibuni sana wageni wetu.

Halafu tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mbunge, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni mmoja wa watunzi wa Wimbo wa Afrika Mashariki Ndugu Joseph Mugango ambaye ameambatana na binti yake Ndugu Johanitha John Mugango. Karibuni sana. Hongera sana kwa kazi nzuri uliyofanya. (*Makofi*)

Wageni wengine 10 ni kutoka Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Ndugu Valarie Msoka. Mheshimiwa Msoka na timu yako karibuni sana. Waheshimiwa wengi mnamfahamu Ndugu Valarie Msoka kwa mambo yake, mnayajua sana. Mliokuwa kwenye Bunge Maalum la Katiba mnamkumbuka sana. (*Makofi*)

Wengine ni Waheshimiwa saba wageni wa Mheshimiwa Cosato Chumi, ambao ni vijana wahitimu wa Vyuho Vikuu ambao wameamua kujiajiri na kujiinua kiuchumi kwa kufuga kuku na nyuki kutoka Mafinga Mkoani Iringa, wakiongozwa na ndugu Loveness Hiluka. Mko wapi vijana? Hongereni sana, ninyi ni vijana wa mfano, tunapambana na hali zetu. (*Makofi*)

Wageni 12 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka, ambao ni wanafamilia, Viongozi wa CCM Zanzibar na wanafunzi kutoka Zanzibar wakiongozwa na mume wake Ndugu Makame Ame Ussi. Karibuni sana ndugu zetu. Tunaye Angelina pale anafanya kazi nzuri tu. (*Makofi*)

Tunao wageni 70 wa Mheshimiwa Daniel Mtuka, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) wakiongozwa na Ndugu Meshack William Madole. Karibuni sana.

Wageni 15 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, ambao ni kutoka Taasisi ya Jamii Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo ndugu Richard Nnko. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 17 wa Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, ambao ni Katibu wa Jimbo Kata ya Kisesa pamoja na wanafunzi wa *UDOM* wakiongozwa na Katibu wa Mbunge Ndugu Yambijonas Masuka, wako wapi karibuni wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo tunaye Ndugu Kondwani Nyirenda kutoka Mkoani Shinyanga, ambaye amekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi zake. Karibu sana.

Tunao wageni watatu kutoka Taasisi ya *Skyfree International ya Arusha* ambao ni Ndugu Samuel Malugu, Ndugu Mariam Ally na Ndugu Adilla Chigomelo. Pia tunao wanachuo 10 kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM* wakiongozwa na Ndugu Heri Daimon, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 80 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Miyuji iliyopo Jijini Dodoma ambao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi kwa leo. Karibuni sana kwa mafunzo. *(Makofi)*

Vile vile tunaye mgeni wa Mheshimiwa Omary Mgumba, Naibu Waziri Wizara ya Kilimo, mgeni wake Ndugu Charles Mboma ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Mkambarani Morogoro, karibu sana.

Nilianza na hawa wageni wetu kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika. Sasa ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Napenda niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Jumapili tarehe 14 Aprili, saa 5.00 asubuni kutakuwa na Semina kwa Wabunge wote kuhusu Uelewa wa Masuala ya Ualbino. Ndiyo maana hawa wenzetu wako hapa. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa na Wabunge wote tunaombwa tuhudhuri. *(Makofi)*

Nilikuwa nimeruka wageni wengine sita wa Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa ambao ni Viongozi wa CCM pamoja na wajasiriamali kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Diwani wa Mpwapwa, Mheshimiwa George Fuime. Karibuni sana ndugu zetu. (Makofi)

Nina tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mwenyekiti wa Jumuiya ya *St. Thomas Moore* hapa Bungeni anapenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba leo Ijumaa tarehe 12 Aprili kutakuwa na Ibada ya Njia ya Msalaba na Upatanisho kwa Wakristo Wakatoliki mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge saa 7.00 mchana. Hii itakuwa katika Ukumbi wa Msekwa ghorofa ya pili.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge na wengine wote mnaopenda kushiriki Ibada hiyo mnakaribishwa sana. Wakristu wote, sio *Wa-Roman Catholic* tu na Wakristo wote mnakaribishwa.

Nadhani mimi hayo ndiyo matangazo niliyonayo hapa.

Mheshimiwa *Chief Whip* wa Serikali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa tangazo lifuatalo kwa niaba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote, kufuatia uamuzi wa Serikali kuhamishia Makao Makuu ya Serikali hapa Jijini Dodoma katika eneo la Mtumba, ninapenda kuwafahamisha kuwa Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaalikwa sasa rasmi kwenye sherehe za uzinduzi wa Mji Mkuu wa Serikali hapa Dodoma Mtumba siku ya tarehe 13 Aprili, 2019 yaani kesho saa 2.30 asubuhi. Uzinduzi huo utafanywa na Mheshimiwa Dkt.

John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na ni tukio kubwa sana la kihistoria katika nchi yetu ya Tanzania. Hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wote kushiriki kwa ukamilifu katika tukio hilo siku ya kesho katika eneo la Mtumba hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Usafiri utatupa?

MBUNGE FULANI: Moja ya haki za Bunge.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Utatupa usafiri?

MBUNGE FULANI: Utakuwepo?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu mimi huwa sipendi mambo ya watu kuanza kuongea kwenye *micro-phone*. Kanuni hazituruhusu. Ni lazima tuheshimu kanuni zetu.

Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Hebu ngoja. Mheshimiwa Msigwa, hebu anza Mheshimiwa Msigwa, unataka Mwongozo?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za hivi karibuni kumezuka tabia ambayo inakiuka kabisa na haitambui kabisa kwamba nchi yetu ni ya mfumo wa vyama vingi, lakini mahali

popote ambapo Mheshimiwa Rais anapita bendera za Chama cha Demokrasia na Maendeleo zinang'olewa mpaka kwenye Ofisi za Vyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Mafinga, bendera zimeng'olewa barabarani na zimewekwa za Chama cha Mapinduzi na ukija Iringa Mjini bendera za CCM zimewekwa mpaka kwenye nguzo (mistimu) kitu ambacho kinakiuka kabisa na hakiakisi kwamba nchi hii ni ya Mfumo wa Vyama Vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lichochea vurugu na chuki katikati ya Watanzania. Vile vile jambo hili linamdanganya Mheshimiwa Rais kwamba vyama vingine havipo kwa kuweka bendera ya Chama cha Mapinduzi tu, kitu ambacho wasaidizi wake wanamdanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba utupe mwongozo wako, nchi hii ni ya Mfumo wa Vyama nami ni mwakilishi wa wananchi: Je, jambo hili linaruhusiwa kwamba tukikuta bendera ya chama kingine tuing'oe? Ambapo ni jambo linalochochea ghasia kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ili Taifa lipate kujua ni namna gani tupate kuendeleza amani na utulivu ambao kila siku inahubiriwa katika jengo hili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 51 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 37 ili kuweza kutoa hoja ya kuhusu haki za Bunge kwa sababu tarehe 8 Aprili, 2019 hapa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 37, kuliwekwa Mezani Hati za Serikali na kati ya hati hizo zilikuwa ni pamoja na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Siku hiyo Wabunge tuliomba kupewe nakala za ripoti hizo kama ambavyo kimsingi Kanuni ya 37 inataka hati zote zinazowekwa mezani Wabunge tupewe nakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiti cha Spika kikajibu tu kwamba, Kiti cha Spika kimepokea na Serikali itafanya utaratibu wa kutoa nakala kwa Wabunge, lakini mpaka naketi kwenye kiti hiki, nimeangalia kwenye *pigeon holes* na hapa Bungeni vilevile mpaka sasa ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nakala hizo 17 hazijatolewa kwa Wabunge. Jambo hili linaminya haki yetu kama Wabunge kuweza kupata taarifa za kuishauri na kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nipewe fursa ya kuitoa hii hoja ili Bunge lijadili juu ya kunyimwa haki ya kupewa nyaraka muhimu za kuweza kuishauri na kuisimamia Serikali na kuiwajibisha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba jambo hili lijadiliwe na tukabidhiwe ripoti hizi siku ya leo muda huu tuweze kuzifanyia kazi kwenye mjadala unaoendelea na kwenye kazi nyingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama)

MWENYEKITI: Hebu kaeni Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Msigwa kwa mujibu wa kanuni ya 68(7), nisingependa kurudia aliyoyasema, mimi naamini alitaka tu kusikika, lakini tukio hilo kwa mujibu wa kanuni hiyo aliyoisema, halikutokea mapema hapa Bungeni. Kwa hiyo, naishia hapo, hakuna kitu cha kuniomba mwongozo kwa suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mnyika amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 51 ambayo inahusu haki za Bunge hili, ikisomwa pamoja na Kanuni ya 38 ambayo ni uwasilishaji Mezani wa Hati na amelenga kwenye *Report* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba tangu ziwasilishwe hapa Mezani Waheshimiwa Wabunge hatujapata nafasi ya kuzipata.

Nianze na moja, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 38 ukisoma vizuri unaanza na yale Magazeti ya Serikali kwa sababu ni sheria za nchi; magazeti ya Serikali yanayowasilishwa hapa, sheria ndogo zile kupitia gazeti la Serikali, lazima zipatiwe kwa Wabunge. Ninyi kama wawakilishi wa Wananchi myafahamu yale ambayo yametungwa kama sheria ndogo kwa maeneo yote ya Tanzania na yanayowahusu ninyi. Ndiyo dhana hiyo.

Kwa hati nyingine ambazo kisheria zinapaswa ziwasilishwa hapa *including* Taarifa ya CAG, ukisoma tena kanuni, zina utaratibu wake. Hatua ya kwanza ya msingi ni kuwasilishwa Mezani na mhusika, Waziri au Mwanasheria Mkuu. Ziliwasilishwa.

Waheshimiwa Wabunge angalieni, hizi hapa. Hii ndiyo *fulfillment* ya kwanza. Haiwezekani Serikali ikaja ikasema tumewasilisha kitu hewa, hapana, ziko hapa. Ukishafanya hivyo, tumetekeleza jukumu hilo. Inafuata hatua ya pili, hizi zitakapopatikana na Waheshimiwa Wabunge mjue hizi ni gharama jamani, mimi nimeulizia na niseme Waheshimiwa Wabunge, hatua yetu ya sasa kama ilivyowasilishwa hapa mnajua inaenda kwenye Kamati husika. (*Makofi/Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Taarifa hii haisomwi humu. Hatuwezi kubishana! Mwongozo wangu kwa suala hilo kwa mujibu wa Kanuni ya 51 namuuliza Mheshimiwa Mnyika, anioneshe ni kifungu kipi cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge kinachosema kwamba hizi zikiwasilishwa hapa ni lazima zigawiwe kwa Wabunge kwa mujibu wa sheria yenyewe. Hatuwezi kwenda...

Mheshimiwa Zitto nakuomba ukae, ukiona nimesimama nakuomba ukae. Aliyetoa hoja hii ni Mheshimiwa Mnyika ndiyo maana nimemuuliza yeye, anza na sheria sio kanuni, unapoenda na kifungu cha 51 ni haki za Bunge kwa mujibu wa Sheria ya Nchi. Hapana! Mimi

nakuongoza kama Mwanasheria, mimi kazi yangu ni kuwafundisha pia. (*Makofi*)

Haki zinazoongelewa ni zile ambazo zimetajwa kwenye Sheria ya Haki na Kinga. Wewe umeomba hiyo kwamba tusimamisha shughuli zetu kwa sababu mpaka ripoti ya CAG ipatikane kwa Wabunge.

WABUNGE FULANI: Ndiyooooo.

MWENYEKITI: Hatuwezi kufanya shughuli za namna hiyo kwa mwongozo wangu ni kwamba...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Umeniuliza...

MWENYEKITI: Hapana Mheshimiwa, kaa chini. Uamuzi wangu ni kwamba Serikali itawasilisha kwa Wabunge kupitia taratibu zetu hapa kwenye *pegion holes* kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

(*Majadiliano Yanaendelea*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunao wachangiaji wetu wa leo, nianze na Mheshimiwa Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Kiwelu na Mheshimiwa Munde ajiandae.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Leo asubuhi tulipoingia hapa, tulianza na dua, kwa hiyo tulianza na Mungu kwanza, sio kilimo kwanza au elimu kwanza, tulianza na Mungu kwanza na tulisali; *“Ewe*

Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba mbingu na Dunia, umeweka katika Dunia Serikali za wanadamu na Mabunge ya Mataifa ili haki yako itendeke. Twakuomba ibariki nchi yetu idumishe uhuru, umoja, haki na amani. Umjaalie Rais wetu hekima, afya njema na maisha marefu ili pamoja na wanaomshauri wadumishe utawala bora."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba mchango wangu wa leo kwa kweli uongozwe na hii sala ambayo tumeisali leo. Kwa sababu tunachangia Ofisi ya Rais nitaomba bila kuvunja kanuni ya kujadili mwenendo wa Rais, nitaomba niguse maswali mbalimbali kuhusiana na Ofisi ya Rais, lakini ambalo naliomba sana Ofisi ya Rais, Utawala Bora na TAMISEMI, walitolee kauli, hivi ilikuwa ni halali kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora kusema kwamba anakwenda kufanya nini Mheshimiwa Selasini?

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Kumwomba Mungu amshukuru Rais.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani anamwomba Mungu amshukuru Rais, hii ni kufuru!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, ongea na kiti.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee na kiti kwamba Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ituambie hivi ni halali kwa Wakuu wa Mikoa na viongozi wa Kiserikali kukufuru na kufanya dhihaka dhidi ya Mwenyezi Mungu? Wengine utasikia wanajiita Mungu wa Dar es Salaam na mambo mbalimbali. Serikali itoe kauli juu ya jambo hii ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezwa hapa kwamba Mheshimiwa Rais atakuja kesho kuzindua Makao Makuu, ujenzi wa Mji wa Serikali. Ningeomba sana sana Ofisi ya Rais imshauri Rais kama ambavyo anapata wasaa wa kuzunguka kuzindua majengo pengine kupatikane wasaa wa siku moja wa Taifa letu na siku ya sala *A National day of prayer* tuiombe nchi yetu. Pengine tutaponya majeraha ya Kibiti,

majeraha ya watu kupigwa risasi kama Mheshimiwa Tundu Lissu, majeraha ya miili kuokotwa Coco *beach* na mambo mengine ambayo kwa kweli, Mheshimiwa Selasini anasema kipindi cha Kwaresma yatatusaidia kutuweka pamoja kama Taifa, kwani Taifa linalokwenda pamoja ni Taifa linaloweza kwenda kwa kasi zaidi kuliko kasi tuliyonayo ya maendeleo ya nchi yetu kwa sababu kasi yetu tunapewa takwimu za uongo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba uchumi wa nchi utakua kwa asilimia saba huku Shirika la Fedha Duniani linatoa taarifa kwamba hiyo asilimia inayosemwa na Serikali haiwezekani sanasana tukijitahidi ni asilimia nne. Taifa la namna hii linahitaji uponyaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumza, tumeapa kulinda Katiba, naelewa wenzetu tukisema kuhusu Katiba wanasema kipaumbele cha msingi cha wananchi ni maji, umeme na miradi mingine ya maendeleo, lakini tulipoapa na Mheshimiwa Rais aliapa cha kwanza tuliapa juu ya katiba kwa sababu Katiba ndiyo nyenzo ya kusimamia mambo yote na ndiyo nyenzo ya kuleta maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, nasema Katiba ni jambo la pili muhimu sana kwa nchi yetu na kwa sababu Katiba ni jambo la pili ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais alipokuja kuhutubia Bunge wakati anazindua Bunge aliahidi hapa Bungeni kwenye hotuba yake kwamba ataendeleza na kukamilisha mchakato wa Katiba mpya. (*Makofi*)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Hebu subiri tu Mheshimiwa Mnyika, Taarifa.

T A A R I F A

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimkumbushe mzungumzaji anayeongea kwamba

siku Rais amekuja hapa kutoa maelekezo yake ya nchi yeye hakuwepo Bungeni, alijuaje hayo maneno? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mbunge wa wapi ambaye hajui kwamba kila kinachojadiliwa Bungeni kinawekwa kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge? Kwa hiyo analiaibisha Bunge tu. Naomba niendele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Rais akiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye kongamano, kinyume na kauli yake ya Bungeni, Rais amesema eti hataki mchakato wa Katiba mpya kuendelea kwa sababu kuna watu wanataka wapewe posho ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Ofisi ya Rais ikamkumbusha Rais. Wao walikaa kwenye Bunge Maalum wakapitisha Katiba inayopendekezwa kinyume na Katiba na wananchi kwa Sheria ya Kura ya Maoni na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, hatua inayofuata ni kura ya maoni dhidi ya hizi rasimu mbili uamuzi wa wananchi kufanyika, jambo hilo halihusu Wabunge kukaa kikao, jambo hilo halijusu Wabunge kupewa posho.

Kwa hiyo kauli ya Rais ilikuwa inataka kupotosha tu mjadala wa Katiba mpya ni muhimu katika majumuisho. Ofisi ya Rais ikasema ni kwanini katika Bunge hili hakijatengwa pesa kwa ajili ya kura ya maoni na kukamilisha mchakato wa Katiba mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikubaliane kwa namna yoyote na kauli ya kwamba eti hakikuwa kipaumbele chenu wala kipaumbele cha Rais. Nimeisoma Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Ilani ya Uchaguzi ya CCM imesema bayana, CCM itaendeleza na kukamilisha mchakato wa Katiba Mpya, tekelezeni Ilani yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitarudi kwenye haya mambo...

T A A R I F A

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu mzungumzaji anayezungumza kwamba Katiba inayopendekezwa tulishiriki wote Wabunge tuliokuwepo Bunge lililopita na mchakato ule ulipofikia hatua, wenzetu wa upinzani hatukuwa nao mpaka hatua ya mwisho waliikataa. Leo hii wanakuja hapa kusema wanataka mchakato uendelee wa kupigia kura, Katiba ipi mpya inayopendekezwa wakati wao waliikataa na hawakushiriki zoezi mpaka mwisho? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mnyika taarifa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kura ya Maoni inasema Katiba inapendekezwa ikishapitishwa kwenye Bunge Maalum hatua inayofuata ni kura ya maoni bila kujali nani alikuwepo na nani hakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea. Nitaomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Ofisi ya Rais, ripoti iliyopita ya CAG sio ya sasa, ripoti ya mwaka uliopita ililubua madudu mengi kwenye sekta mbalimbali na Wizara mbalimbali na kati ya mambo yaliyoibuliwa ni pamoja na suala la 1.5 trillion ambayo baadaye ilipanda mpaka kuwa 2.4 trillion. Katika ufafanuzi wa Serikali juu ya 1.5 trillion kuna taarifa zilitolewa toka 1.5 mpaka 2.4 kwamba bilioni 976.96 zilihamishwa kwenye Mafungu mbalimbali zikapelekwa kwa maana ya kibajeti reallocation zikapelekwa kwenye Fungu la 20 la bajeti ambalo ni sehemu ya hotuba yetu ya leo Ofisi ya Rais, Ikulu. Sasa mimi kama Mbunge naamini moja, Bunge halikupitisha uamuzi wa kufanya reallocation ya bilioni 976.96 kupeleka Fungu namba 20 Ikulu. Pili... **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, hebu nisaidie Sheria ya Bajeti kuhusiana na *reallocation* inasemaje? Nisaidie?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya *interests...*

MWENYEKITI: Ni Bunge linafanya au mamlaka husika inafanya?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa *interest ya time* nijikite zaidi kwenye hoja yangu.

MWENYEKITI: Hapana.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kujadili hilo tuta...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utalinda muda wangu?

MWENYEKITI: Naulinda! Mheshimiwa Mnyika na Waheshimiwa Wabunge, tusifanye *generalization* ambazo huwezi kuzi-*defend* hapa. Sisi wote hapa tumeshiriki, baadhi yetu tumeshiriki katika utungaji wa sheria hiyo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: *Shut up!*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, kiwango ambacho kimetajwa na Sheria ya Bajeti kama kuna Mbunge anataka ku-*challenge* hiyo, *warranty ya reallocation* inapowekwa na Serikali hapa wewe unapaswa sasa useme kwamba *reallocation* hiyo imezidi kiwango ambacho kimewekwa na Bunge, ukomo, lakini hatuwezi hapa kuja tunafanya *generalization* tu ili -*m-get away* na hiyo, hapana si kweli! Waziri wa Fedha, jamani Wizara hiyo ni makini sana. Endelea. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: *Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuondoe utata kuhusu jambo hili la bilioni 976.96 kwa kuwa CAG anabanwa banwa kidogo kukagua Ikulu, Ofisi ya Rais ikija kwenye majumuisho hapa itueleze hizi bilioni 976.96 Ikulu zilitumika kwa matumizi gani? Tupewe mchanganuo wa kina...[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusubiri kuja kujibu kuwaachia Watanzania wanapotoshwa. Lazima watu wanaosema uongo ndani ya Bunge lako Tukufu wathibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiomba kiti chako kimwelekeze Mheshimiwa Mnyika aweze kuthibitisha kwamba CAG anabanwa banwa kukagua Fungu 20 la Ofisi ya Rais, kwa sababu kinachofahamika kila Fungu lina *Resident Auditor* kutoka Ofisi ya CAG including Fungu 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiki kinachoelezwa kisiwapotoshe Watanzania kule nje. Naomba iwekwe wazi kwamba hakuna Fungu hata moja ambalo CAG anazuiwa kulikagua na Fungu hili lilikaguliwa na CAG hakuja na hoja hizi zinazoletwa kuwadanganya Watanzania humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kiti chako kitende haki kwenye jambo hili ili Watanzania wasiendelee kudanganywa na Mheshimiwa Rais wetu asiendelee kuchafuliwa bila sababu za msingi. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini ulilinda muda wangu, lakini mimi bado naomba katika majumuisho Ofisi ya Rais ilete mchanganuo hizi pesa zimetumika kwenye kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Hotuba hii ya...

MWENYEKITI: Una dakika mbili.

MHE. JOHN J. MNYIKA... Utumishi wa Umma inahusu maslahi ya wafanyakazi wa umma...

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Kanuni namba ngapi?

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(a).

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni iliyovunjwa ni ya 64(a). Kanuni inasema hivi; Mbunge hatatoa ndani ya Bunge Taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la 1.5 *trillion* limeendelea kuongelewa humu ndani ya Bunge tena limeongelewa kwa uongo. Kwa sababu nitahitajika kuthibitisha kuwa huo ni uongo, Ripoti ya PAC Mwenyekiti wake ambaye ni Mpinzani, Mheshimiwa mama Kaboyoka, Mbunge wa CHADEMA inasema hivi ukurasa wa 35; *"Mheshimiwa Spika katika kuhitimisha suala la tofauti la 1.5 trillion kati ya mapato ya Serikali na makusanyo kwa mwaka 2016/2017, naomba kuweka kumbukumbu sahihi katika Bunge lako Tukufu kuwa tofauti hiyo haikuwepo baada ya marekebisho ya mahesabu kufanyika."* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Bunge lako limeendelea kutumika kama jukwaa la kuichafua Serikali kuwa imefanya matumizi ya 1.5 *trillion* na Bunge lako limekaa kimya bila kuwakemea hawa. Watanzania wameendelea kupotoshwa na Bunge lako limekubali. Naomba likemewe suala hili na utoe maelekezo. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlinga, umesimama kuhusu utaratibu, umetaja hiyo Kanuni ya 64(1)(a)...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, *please*. How can you get to (a) without reading 64? (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, naendelea, hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Sasa Kanuni hii lazima uisome pamoja na Kanuni ya 63, Mbunge aliyekuwa anaongea hapa alikuwa ni Mheshimiwa Mnyika, kwa hiyo, ni Kanuni ya 63(2), inasema, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni, hutachukuliwa unasema uongo kama unafanya *reference*. Fasisli ya (3) inasema, Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka “kuhusu utaratibu”, tumemskiliza Mheshimiwa Mbunge kafanya hivyo na Mheshimiwa Mnyika kwa mujibu wa fasili ya (4), aliketi, lakini sasa huyu aliyesema wewe husemi ukweli anapaswa aseme kitu, atoe maelezo kwa kiwango ambacho kinaliridhisha Bunge kwamba kuna uongo umesemwa. Ameenda mbali zaidi amesema Taarifa ya Kamati ya PAC kuhusiana na *amount* hiyo, kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ilisema suala hilo si hoja tena, kwa hiyo, hiyo ni rekodi ya Bunge. (Makofi)

Kwa maana hiyo Mheshimiwa, kwa mujibu wa Kanuni zetu, kwa sababu ya maamuzi ya Kamati ya Bunge ya PAC, kwa hayo iliyoyasema, wewe sasa ndiyo unatakiwa uthibitishie kweli au si kweli. Kwa maana hiyo, nakupa *options* mbili tu, ya kwanza, ufute tu kauli yako kuhusiana na hayo maelezo yako, yale uliyosema ya bilioni ambazo zilikuwa *summarized* zote, wewe umesema bilioni 900 lakini ukasema ni trilion 2.4 kwa maana kwamba *1.5 trillion* kujumlisha na hizo bilioni ndiyo unapata hiyo. Sasa maelezo ya *1.5 trillion* yapo kwenye ripoti ya PAC. Maana wewe umefanya majumuisho, sasa nakupeleka ufute kauli yako au nikupe muda wa kuja kuthibitisha Bungeni hapa, chagua mojawapo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niweke rekodi sawa, nimesema...

MWENYEKITI: Tunabishana tena?

MHE. JOHN J. MNYIKA: *Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, naomba niweke rekodi sawa. Nimesema, nataka maelezo ya Serikali Bungeni juu ya shilingi bilioni 976.96 zimetumika kwa matumizi gani? Nimesema jambo hili liko outstanding na hili ndilo linasababisha mjadala wa 1.5 trillion na 2.4 trillion kuendelea. Kwa hiyo, kama ni uthibitisho, nitakiwe kutoa uthibitisho kuhusu suala la shilingi bilioni 976.96 za Vote 20 ya Ikulu. Nipewe nafasi ya kuzungumza kuhusu hilo. (Makofi) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, huna hoja yoyote, unatupotezea muda wetu wa Bunge. Kwa sababu kama *issue* yako ilikuwa ni 1.5 trillion kama ulivyoanza, usingekimbilia kutafuta 900 billion shillings. Ulifanya majumuisho ya 2.4 trillion na ndiyo maana Mheshimiwa Naibu Waziri akasimama. (Makofi)

Kwa hiyo, kama unataka tupitie *Hansard* ili tuone mtiririko wa *argument* yako. Mimi naagiza watu wa *Hansard* kabla ya sasa saba tupate *Hansard* hiyo halafu nitatoa uamuzi wangu kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Mnyika. Ahsante. (Makofi)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba...

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, si nilikwambia dakika mbili.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umekwisha wakati nimekuwa *interrupted!*

MWENYEKITI: Umekwisha!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie muda wangu, nilikuwa nazungumza nikawa *interrupted.*

MWENYEKITI: Sasa kama hutumii vizuri muda wako, umekwisha. Nimekulindia muda nikakwambia zilikuwa zimebaki dakika mbili, umeongezewa nyingine mbili.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Heche, Heche, Heche, narudia Heche, *please, please!*

Haya tunaendelea na Mheshimiwa Kiwelu.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza hotuba zetu zote mbili za Kambi ya Upinzani. Zimeeleza mambo mengi mazuri na tunaishauri Serikali kuzingatia yale yote yaliyoelezwa na kambi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pole kwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe pamoja na Mheshimiwa Esther Matiko ambao walikaa gereza kwa siku 104 kwa kunyimwa haki yao ya dhamana. Nimpongeze Jaji Rumanyika kwa kuweza kuona hilo na kutoa haki na hata leo wako nje kwa dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mwenyekiti wetu wa Chama, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, tunakupongeza kwa uimara wako, pamoja na yote ambayo unafanyiwa umeendelea kuwa imara na wewe ndiwe Mwenyekiti wetu...

MBUNGE FULANI: Atabaki kuwa juu.

MHE. GRACE S. KIWELU: Najua wako ambao wanaumia kwa ajili ya wewe kuwa Mwenyekiti lakini utaendelea kuwa juu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu Tume huru ya Uchaguzi. Najua wengi watatushangaa ni kwa nini tunazungumzia Tume hii lakini kitanda usichokilalia huwezi kujua kunguni wake. Sisi tunayo maumivu tuliyoyapata kwa sababu ya Tume hii ya Uchaguzi kutokuwa huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi ambazo mfumo wake ni wa kupata viongozi kwa mujibu wa sheria kwa kupigiwa kura, viongozi wengi wameanza kudharau wapigakura wao na tumeona wakifanya maamuzi bila kujali wanawaathiri vipi wapigakura wao. Tumefanya maamuzi mengi bila kujali waliotupa dhamana ya kutuleta humu ndani wanataka nini. Wanafanya haya kwa sababu wanajua Tume wameimiliki, si huru, wanafanya maamuzi bila kujali mawazo ya wananchi wao ambao ndiyo wamewapa dhamana ya kuwaleta humu. *(Makofi)*

T A A R I F A

MHE. MAULID S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MBUNGE FULANI: Kaa, jamani.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hii itakuwa ni taarifa ya mwisho.

MHE. MAULID S.A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

MWENYEKITI: Tutumie muda wetu vizuri.

MBUNGE FULANI: Wewe poyoyo vipi?

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. MAULID S. A. MTULIA: *Mheshimiwa Mwenyekiti, sishangai kwanza baadhi ya Wabunge wako nidhamu yao kuwa chini ni kwa sababu namna wengine wanavyopatikana*

ni aibu kuizungumza humu ndani. (Makofi) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: Poyoyo.

MHE. MAULID S.A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yangu ni kwamba, Mheshimiwa Mbunge anazungumzia kwamba Tume ya Uchaguzi haiko huru, siyo kweli. Nataka kumpa taarifa Tume ya Uchaguzi iko huru na wao hawana haki ya kupima uhuru wa Tume ya Uchaguzi kwa sababu hata uchaguzi wenyewe siku hizi hawagombei.

MBUNGE FULANI: Wewe poyoyo.

MHE. MAULID S.A. MTULIA: Usipogombea huwezi kujua, Tume sasa hivi iko vizuri, inatenda haki, kila anayeshinda anatangazwa. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza msiende hivyo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Kaeni kwanza, Waheshimiwa ninyi wawili wote kaeni.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. JOHN W. HECHE: Atuambie wamepatikanaje?

MWENYEKITI: Ngoja kwanza nitafika huko, *please*. Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Esther Matiko kaeni chini.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechoka.

MWENYEKITI: Aliyekuwa anapewa taarifa ni Mheshimiwa Kiwelu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwa sababu...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Afute.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu, kaa tena Mheshimiwa Kiwelu.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

MWENYEKITI: Niambie Kanuni gani?

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(g), Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhallisha watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mbunge wa Kinondoni akitoa mwongozo wake, alisema kwamba...

MWENYEKITI: Akitoa taarifa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, akitoa taarifa alisema kwamba kuna baadhi ya Wabunge

kupatikana kwao kunatia aibu. Sasa mimi napenda alithibitishie Bunge hao waliopatikana kwa njia ya aibu ambayo haiwezi kusemekana ni watu gani na hiyo aibu ni nini, vinginevyo afute kauli yake. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Alikuwa anampa taarifa nani?

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anampa taarifa Mheshimiwa Kiwelu na kutoa taarifa ndani ya...

MWENYEKITI: Mheshimiwa ngoja tu, nawapeleka polepole tu, *logically*. Mheshimiwa Kiwelu, nilikuomba upokee taarifa au unaikataa?

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naikataa lakini naomba utoe maelekezo kwake athibitise hiyo kauli yake aliyoisema. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kufundishana Kanuni, yeye kasema...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, yeye katoa madai aliyoyasema kwa njia ya taarifa. Kama kuna Mbunge sasa anasema kwamba amesema uongo, eleza kwa kiwango ambacho utaliridhisha Bunge kwamba amesema uongo ili sasa *burden* ihamie kwake. Eleza maana yeye hajamtaja yeyote. Mtusaidie tu, maana umetumia Kanuni ya kuhusu utaratibu siwezi kuiacha hivyo hivyo. Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu utaratibu kama alivyokuwa amesema Mnadhimu. Hii iko *straight*, mzungumzaji alisimama akitaka kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Grace Kiwelu kuhusiana na Tume huru lakini katika kutaka kutoa taarifa yake akatumia lugha ya kuudhi na kudhalilisha, wakati akitaka kutoa taarifa kuna baadhi huku waliongea akasema, kuna wengine upande huo wanapatikana kwa kuuza

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, uliniambia nifafanue.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko, nilipenda wewe uwe *very specific*.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda aliyetoa taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni, kwanza kabisa kwa Kanuni ya 64(1)(f) na (g), aidha athibitishie kwa Bunge lako hili, ni Wabunge gani ambao wako upande huu waliopata Ubunge kwa aibu. Maana yake tunajua Wabunge wanapatikana kwa kupigiwa kura, wawe Wabunge wa Viti Maalum au Wabunge wa Kuchaguliwa kwa Majimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa atuthibitishie kwamba ni Wabunge gani waliopatikana kwa aibu huku na ni aibu gani hiyo waliyoifanya mpaka wakawa Wabunge? Kinyume cha hapo afute maneno yake. Hili Bunge lako siku hizi linatumika kudhalilisha akina mama, *of which we wan't agree at all. (Makofi)*

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante, umeeleweka.

MHE. MARGARET S. SITTA: Ataweza kuthibitisha hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni...

MBUNGE FULANI: Umezoea.

MHE. MARGARET S. SITTA: Ni kweli.

MWENYEKITI: Unaweza ukafuta hayo maneno?
(Makofi)

MHE. MARGARET S. SITTA: Afute hayo maneno bwana.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, afute bwana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ngoja nataka twende vizuri tu.

MHE. MARGARET S. SITTA: Afute hiyo bwana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sitta, umesimama kwa Kanuni gani?

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Msigwa alisema hapa mpaka wabebe vidumu vya petroli.

MBUNGE FULANI: Kaa chini.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye yule si alipatikana kwa aibu masanduku ya kura yalichukuliwa yakahesabiwa kwake huyo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, msiongee, tulieni tu, hebu kaa tu Mheshimiwa Sitta. Mheshimiwa Mtulia.

MBUNGE FULANI: Huyu amezoea kudhalilisha wanawake.

MHE. MAULID SAID MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta kauli japokuwa...

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. MAULID S.A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutaja wanawake, nafuta kauli yangu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana niliwapeleka kwa utaratibu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Tusikilizane basi, Mheshimiwa nakusikia vizuri sana mpaka hapa, hebu tusikilizane. Ndiyo maana nilitaka kusema kwa vile yeye amefuta kauli hiyo...

WABUNGE FULANI: Hajafuta.

MWENYEKITI: La pili niliwapeleka polepole kwa utaratibu. Mimi sitaki kuendeleza mjadala huo kwa sababu hakuwa ametaja jina la mtu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiwelu, endelea kuchangia tumelinda muda wako.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie akina mama wa Kinondoni kwamba Mbunge wao hana heshima kwa akina mama ambapo mama yake amemzaa yeye na kuweza kuwa kiongozi leo. Wabunge wanawake wa CHADEMA tumechaguliwa kama walivyochaguliwa Wabunge wengine wa Viti Maalum kwa kufuata taratibu na kanuni za chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo, tumeshuhudia mabadiliko makubwa sana sasa hivi ya uteuzi wa Wakurugenzi wa Wilaya umeacha kufuata taaluma, taratibu na sheria zilizokuwa zinafanyika hapo awali lakini sasa hivi kigezo namba moja ni kuwa kada wa Chama cha Mapinduzi. Kibaya zaidi tunakwenda kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa ambazo tunajua Tume haina muundo mpaka chini, wanakwenda kuchukua watu kutoka TAMISEMI, sasa kwa muundo huu ambao Awamu ya Tano umeanza nao wa kuchagua Wakurugenzi sifa zao wawe makada wa Chama cha Mapinduzi, tunawaambia mapema kwamba, kama walivyosema wenzangu jana kwamba hatutakubali kudhulumwa, wakatende haki kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua haki hii haitatendeka kwa sababu walishaonywa na Mkuu wa Nchi kuwa wasipomtangaza mgombea anayetokana na chama tawala akatafute kazi nyingine na kauli hii haijawahi kufutwa mpaka leo. Kwa maana hiyo, Wakurugenzi, Maafisa Kata ambao wako kwenye kata zetu zinazokwenda kufanya uchaguzi watakwenda kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka TAMISEMI ituambie hawa Maafisa Kata walioletwa pamoja na Wakurugenzi, wana haki kweli ya kuendelea kuwa wasimamizi wa uchaguzi wakati wanakwenda kufuata maelekezo ambayo walishapewa na Mkuu wa Nchi? Ndiyo maana tunaendelea kulalamika na kusema kwamba Tume hii si huru tunataka Tume huru itakayozingatia haki za wapigakura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona uhuni uliofanyika kwenye chaguzi za marudio, watu wamepora maboksi na kwenda kujaza kura na kurudisha kwenye vituo wakisaidiwa na Polisi. Pia tumeona kwenye vituo vya kupigia kura, mawakala tuko ndani tunaheshabu kura lakini Mapolisi wanabandika matokeo nje, wanaingia kuchukua maboksi ya kura. Halafu mnatuambia hii ni Tume huru, kwa kweli Kambi ya Upinzani na wapinzani wote bado tunaendelea kudai Tume huru ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la ma-DC na Wakuu wa Mikoa. Mimi ninatoka Mkoa wa Kilimanjaro, sina tatizo na Mkuu wangu wa Mkoa, anafanya kazi zake vizuri, anatumiza wajibu wake kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Nina tatizo na Mkuu wa Wilaya ya Hai, DC Sabaya. Huyu kabla ya uteuzi wake alikuwa Diwani Kata ya Sambasha, Halmashauri ya Arusha DC, kwa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, DC huyu ameletwa Wilaya ya Hai, anasema anakuja kupambana na Mheshimiwa Mbowe. Namwambia hana ubavu wa kupambana na Mheshimiwa Mbowe. Amekuwa akiingilia shughuli za vyama vya siasa, pia mmeona akiwa anawabughudhi wawekezaji. Tunajua Ma-DC na Wakuu wa Mikoa ni wanasiasa, lakini tunajua ziko sheria na taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kuwawesha kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sabaya amekuwa akikamata viongozi wetu wa chama kuzuia wasifanye vikao, tuna chaguzi zinaendelea chini za chama, Mheshimiwa Sabaya hataki vikao vifanyike, lakini amekuwa akimsumbua Mwenyekiti wa Halmashauri kwa kumbambikizia tuhuma za uongo. Nampongeza Mwenyekiti wa Halmashauri, ni mwanamke na yuko imara kweli kweli. Amekuwa akiwalazimisha Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji kusaini barua za kujuzulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo haki na siyo kazi aliyotumwa kufanya Hai. Ametumwa akashirikiane na wananchi wa Hai kuleta maendeleo na siyo vinginevyo.

Kama ni mwanasiasa, kwanza atekeleze kazi zake, akimaliza ndiyo akafanye siasa ya chama chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kushuka kwa mapato kwa Halmashauri zetu. Halmashauri nyingi nchini zimeshindwa kukusanya mapato kutokana na vyanzo vingi vikubwa vya mapato kuchukuliwa na Serikali Kuu. Hii imesababisha Halmashauri zetu kushindwa kuleta maendeleo na ile mipango waliyokuwa wamepanga kushindwa kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naitaka Serikali, yale mapato ambayo waliyokuwa wanakusanya, ni wakati muafaka sasa kurudisha kwenye Hamashauri zetu ili ziweze kujiendesha, kwa sababu kutakuwa hakuna maana kuanzisha Halmashauri ambazo zinashindwa kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo madogo madogo ambayo yalikuwa yanafanywa kutokana na hayo mapato ya ndani ikiwemo ujenzi wa vyoo, kulipa *bill* za maji na umeme, lakini yameshindwa kufanyika mpaka sasa. *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kiwelu kwa mchango wako. Mheshimiwa Munde. *(Makofi)*

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia. Nilikuwa na mambo mengi ya kuchangia kuhusu Tabora, lakini nimeona muda wangu kidogo nichukue kumjibu kaka yangu Mheshimiwa Mnyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika amesema Mheshimiwa Rais kwa sababu ana nafasi ya kufanya uzinduzi wa miradi, angechukua nafasi ile akafanya Sala ya Kitaifa kuiombea nchi hii. Mimi nadhani Mheshimiwa

Rais anafanya kazi kubwa na ndiyo maana kuna miradi mingi ya kuzindua. Hiyo ni kazi, tena kubwa ya kuwaonesha Watanzania ni nini Serikali yao inafanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina dini; ina Wakristo, Waislam na dini tofauti tofauti. Kila siku tunasali kumwomba Mwenyezi Mungu. Hapa leo ni Ijumaa, nikitoka hapa naende Msikitini kusali, kumwomba Mwenyezi Mungu kwa ajili yangu na familia na nchi yangu. Nadhani watu wote wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Rais ameweza kuita viongozi wa dini mara kadhaa, anaongea nao kutaka maoni yao na kuwaomba waendeleo kuiombea nchi yao. Mimi nadhani Mheshimiwa Mnyika labda ana *stress*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika ameongea kuhusu Katiba mpya. Ni hao walijiunga UKAWA mara ya kwanza kwa ajili ya kwenda kuipinga Katiba iliyopendekezwa. Namshangaa leo anaidai Katiba hiyo ambayo wao kwa mara ya kwanza waliungana kwenda kupinga nchi nzima watu wasiunge mkono Katiba iliyopendekezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo namshangaa ndiyo niseme ndimi mbili, ndiyo niseme mna *stress* kwamba hamtapata Ubunge tena, yaani nachanganyikiwa kwa kweli. Mliikataa Katiba, leo mnaitaka Katiba. Yote hiyo ni kui-*frustrate* Serikali ishindwe kufanya kazi yake, tukae na Katiba tushindwe kuendeleza miradi iliyopo ili pesa yetu tuimalizie kwenye Katiba mje msem kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi maendeleo, ameshindwa kufanya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema tena Mheshimiwa Rais fanya kazi yako kama inavyostahili, achana na mambo ya Katiba, hukuwaahidi Watanzania Katiba, uliwaahidi maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee tena kidogo kwamba wamekuwa wanasema sana kwamba

Wakurugenzi, Ma-DC, ni wana CCMni nani anaweza kufanya kazi na mtu ambaye hamwamini. Hata leo nikifungua duka, nitamweka ndugu yangu, nitamweka mtu ninayemwamini aliye karibu name. Ni nani anaweza kuwa Rais kati yao wao akachukua Mbunge wa CCM Munde akampa Ukuu wa Mkoa? Hatuwezi kufanya hivyo. Mheshimiwa Rais angalia watu unaowaamini, uliowachuja, wakakuridhisha kufanya kazi na wewe kama vile wao ambavyo wanabebana, wanasaidiana wao kwa wao kwenye nafasi zao chungu nzima ikiwepo Ubunge. (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Wape dozi. (*Kicheko*)

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo na Bajeti Wizara. Naipongeza Wizara ya TAMISEMI kwa kazi nzuri wanayoifanya. TAMISEMI wamefanya kitu kizuri sana, wameboresha ukusanyaji wa mapato. Leo hii ukiwa popote, viongozi wa TAMISEMI wanaweza kuangalia Halmashauri gani imekusanya shilingi ngapi, imetumia shilingi ngapi na imefanya nini? Hii ni hatua kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Jafo na Manaibu Waziri pamoja na Menejimenti nzima ya TAMISEMI. Vile vile naipongeza Wizara ya Utawala Bora, mzee wetu Mheshimiwa Mkuchika, mpenzi wetu Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa tunakupongeza sana, mnafanya kazi kubwa mno tunawaona. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu mwendelee kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *system* waliyoiweka ni nzuri sana. Kwa kweli mimi nimefanya kazi Halmashauri, naomba ni-*declare*. Hakuna tena mtu atakayeweza kuiba *revenue* ya Halmashauri. Watu wataiba kwenye matumizi hewa, kwenye *ten percent*, kuagiza vitu ambavyo siyo vya kweli. Kwenye *revenue* kwa kweli mmedhibiti na mtaacha *legacy*, hii kazi mmeifanya ni kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kuhusu vitambulisho. Wenzetu hawa wamekuwa wanaongea sana

kuhusu vitambulisho vya 20,000 wakiviponda na kuvibeza. Kama nilivyosema, nimefanya kazi Halmashauri. Zamani akina Mama Lishe, Wamachinga walikuwa wanatozwa shilingi 500 kwa siku. Anapewa risiti ya shilingi 500/=, kesho anapewa risiti ya shilingi 500, analipia shilingi 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wiki mbili anaenda kufurumuliwa, masufuria ya wali yanamwagwa, maharagwe yanamwagwa, mboga zao zinatupwa. Leo Mheshimiwa Rais amewatambua kwenye Sekta Rasmi ya Wamachinga kwa kuwapa vitambulisho wa shilingi 20,000. Nilidhani tutafurahi, tutaridhika wamama hawa, Wamachinga, vijana wetu hawatanyang'anywa tena vitu vyao, watafanya kazi wakiwa na *confidence* zao na wameambiwa wasiguswe wafanye kazi popote. Mnaka nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani shilingi 500/= ukiidisha mara siku 365 za mwaka walikuwa wanalipa shilingi 182,000/=. Leo shilingi 20,000/= ukiigawa kwa siku 365, wanalipa shilingi 55/= kwa siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetoka Tabora. Sisi ni maarufu sana wa kupika vitumbua. Mama anayepika vitumbua; kitumbua kimoja shilingi 500/=, akiuza vitumbua 40 ana shilingi 20,000/=. Mwaka mmoja una wiki 52. Kila wiki mama huyu aweke hela ya kitumbua kimoja tu 500, ndani ya wiki 40 amefikisha 20,000/=. Hivi mnataka nini jamani? Au mmezoea kupinga tu? Mlipinga reli, mmepinga *Stiegler's*, mnapinga ndege. Tumewazoea! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaambie Serikali, nimwambie Mheshimiwa Jafo, vitambulisho hivi viendeleo, ni kitu kizuri sana, kinawatambua Wamachinga wetu, Mama Lishe wetu, hawafukuzwi tena, hawamwagiwi vitu vyao, lakini 20,000 ni *reasonable price*. Wale watu ilikuwa vikishachukuliwa vile vitu vikamwagwa na Mgambo wao wanawachukua wanawatumia kwenye maandamano. Safari hii mmewakosa. Safari hii mtoto wake ambaye yuko

India, yuko Marekani, amlete aandamane. Wamachinga tena hamwapati. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie haraka haraka. Niseme tu, ni lazima kila Mtanzania achangie pato la Taifa. Tuache kujidanganya. Hamna nchi yoyote duniani watu hawalipi kodi; hamna nchi yoyote duniani watu wanafanya kazi bila kulipa ushuru; tusidanganyane. Hawa watu wenye sekta ambazo siyo rasmi, ndogo ndogo ndio walio wengi. Kwani wanapita barabara zipi? Hospitali wanatibiwa ipi? Kwa nini wasichangie pato la Taifa? Kwa hiyo, tusitake kuivuga Serikali na kutoa kwenye msimamo wake thabiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu Jimbo la Ulyankulu. Jimbo hili lina wakimbizi wengi sana. Wakimbizi hao wamekubaliwa kupiga kura ya Mbunge na kura ya Mheshimiwa Rais. Wakimbizi hawa wamekataliwa kuchagua Diwani kwenye maeneo yao, hawachagui viongozi wa Serikali za Mitaa, jambo linalotushangaza kabisa. Kwa sababu huu ni uadui mkubwa. Huwezi kukaa na mtoto wa ndugu yako ukambagua, hiki fanya, hiki usifanye. Kama walikuwa hawatakiwi, wasingepewa uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wameshakuwa raia sasa, Watanzania, kwa nini mnawazuia wasichague Madiwani? Kwa nini mnawazuia wasifanye uchaguzi wa Serikali za Mitaa? Ukiangalia ni *double standard*. Kwa sababu kwa yangu Mheshimiwa Kakoso kule kuna wakimbizi, lakini wanachagua Madiwani, wanachagua Serikali za Mitaa, wanachagua Wabunge, wanachagua Rais. Sasa huku ninyi mmetuwekea wachague Wabunge na Rais tu. Sasa kama anamchagua Rais, anamchagua Mbunge, kwa nini unamkatilia asichague Diwani na umeshampa urai? Huyu ni raia. Kwa hiyo, naomba mwatendee haki, wapate nafasi, wapate fursa nao wachague na wajichague. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeenda mbali zaidi, hawapati chochote cha Kiserikali wakati tumeshawapa urai. Juzi nilikuwa kule Kaliua, wamana hawo wanakataliwa

kupata mikopo ya Halmashauri na wakati vikundi vyao na wakati tumeshawapa uraia: Je hii ni sahihi jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatengeza bomu ndani ya nchi yetu. Hawa tumekuwa kama tumewapa uraia, lakini tunawabagua. Basi kama ni hivyo, tuwanyime uraia, tuwanyang'anye. Kwa sababu tumeshawapa, naomba pia wakubaliwe kufanya kila kama wanavyofanya wengine. Kule kwa Mheshimiwa Kakoso, kwa kaka yangu Mbogo kuna wakimbizi, lakini wanafanya kila tu. Kwa nini isiwepo na Ulyankulu hivyo hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Kambi za wakimbizi zitafungwa? *(Makofi)*

(Hapa kengele ya pili illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Munde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwigulu.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. La kwanza, nitumie fursa hii kuwapa pole sana wananchi wangu wa Kata Tulya ambao wamepatwa na matatizo ya shule ya msingi kuharibiwa na mvua pamoja na zahanati yao. Niwaambie wawe watulivu, nami nitapata fursa *weekend* kwenda kuungana nao katika shida hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya yeye pamoja na wasaidizi wake kwenye Wizara hizi ambazo leo hii tuna mjadala mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kwa sababu leo ni *weekend* na nchi yetu itakuwa na jambo kubwa upande wa michezo, nawatakia kila la heri vijana wetu wa umri wa chini ya miaka 17 na wapeperushe vizuri bendera yetu ya Taifa.

Nawatakia kila heri pia *club* ya Simba ambao na wenyewe watakuwa wanapeperusha bendera ya nchi yetu kwa upande wa vilabu bingwa barani Afrika watakapopambana na wenzetu wa kule Kongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimeyasema hayo, niende moja kwa moja kwenye maombi. Jambo la kwanza ambalo ningependa kulileta mezani kwa Mheshimiwa Waziri ni hili ambalo moja kwa moja lina muunganiko na dhahama iliyowapata ndugu zetu wa Kata ya Tulya, kwamba kwa kuwa zahanati ile imeharibiwa na kwa kuwa ndugu yetu Mheshimiwa Jafo amekuwa mstari wa mbele sana katika kusaidia upande wa Sekta ya Afya, naomba apatapo nafasi tena ya kutupatia vituo vya afya, basi Kata ya Tulya ambayo zahanati yake imeharibika katika Kijiji cha Doromoni, iweze kupewa kipaumbele. Sambamba na hiyo, aikumbuke pia Kata ya Mtoa ambayo ni Kata ya Mbugani ambako upatikanaji wa huduma za afya umekuwa wa shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimeyasema hayo, naomba niende kuweka ushauri kwenye mambo mawili makubwa. Jambo la kwanza, nimefuatilia mijadala tangu Waziri alipotoa hoja hii. Ni vizuri sana niwashauri Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania, kuna mambo ambayo tunatakiwa tuwe tunayabeba kwa umakini mkubwa sana, hasa katika kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Rais wetu ametangaza vita ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wakati wa kubigania uhuru walikuwa na stahili zao za kupambana na walikuwa na namna ambazo wanakumbana nazo. Sasa hivi ambapo pana vita ya kiuchumi, hao watu tunaopambana nao kwenye vita za kiuchumi ni watu wenye akili, ni watu wenye fedha, na ni watu watu wenye uwezo wa kijasusi. Kwa maana hiyo, kila jambo linapotokea kwenye nchi yetu ni vyema sana tukawa tunalitafakari kwa uzito mkubwa badala ya kwenda kwenye uzito mwepesi kama sisi tunavyofanya mambo yanapotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumeshuhudia katika nchi yetu yakitokea matukio ya kiuhalifu mengi mengi hivi, ambayo kwa bahati nzuri sana Serikali iliyadhibiti yote; moja ya matukio mabaya ni kama yale ya Kibiti; matukio mengine kama yale ya utekwaji wa watoto kule Arusha; matukio mengine ni kama yale ya utekwaji watoto kule Njombe; na mengine ya kiuhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya aina hii yote yamedhibitiwa na Serikali kupitia vyombo vya dola hivi hivi. Ni jambo la ajabu sana linapotokea tukio mojawapo la kiuharifu, badala ya watu kuona kwamba nchi yetu imekuwa na matukio ya kiuhalifu ambayo yanashughulikiwa na Serikali, kwa sababu za kisiasa na kutengeneza taswira chafu kwa Serikali, watu wanakimbilia kwenda kuhisi kwamba huenda matukio yanafanywa na vyombo vya dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilimsikiliza mchangiaji mmoja, Mheshimiwa Mbunge wa kutoka Dar es Salaam akisema matukio ya aina hii kwa nini yasichukuliwe kwamba yamefanywa na Serikali au kupitia vyombo vyake? Akatolea mfano tukio la kutekwa kwa Mo. Hata mwizi tu ambaye ajaenda shule; mwizi wa mifugo aliyeko kijijini, hawezi kuiba mfugo, akaenda kuchinjia ng'ombe wake wa wizi mlangoni kwa nyumba yake. Sijui nimeongea Kiswahili cha Kikenya! Yaani mwizi hawezi kwenda kuiba ng'ombe, akamchukua ngo'ombe wa wizi akaenda kuchinjia nyumbani kwake ama mlangoni kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukianza kuwaza kwamba vyombo vya dola vinaweza vikawa vimeshiriki kwenye utekaji, halafu yule mtu akaokotwe, halafu vyombo hivi vikampeleke pale; ni kitu ambacho ni kuwaza kwa haraka haraka na kwa kutafuta kuaminisha watu jambo ambalo silo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watu wanaofikiria, unaweza ukaona na ni muunganiko mkubwa kwamba hawa ni watu wanaotengeneza chuki dhidi ya Serikali na mambo

mengine yanaweza yakawa yanafanyika ya muundo huu.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo niliona pia ni vyema nikalishauri, hiki ni chombo cha uongozi. Bunge ni chombo cha uongozi, ni chombo cha uamuzi, ni chombo cha sera. Kwa kuwa ni chombo cha viongozi, tunapokuwa tunajadili hapa, ingefaa miaka kadhaa itakayokuja watu wakipitia *Hansard* zeweze kuwapa dira kwamba katika kipindi hiki Taifa lilikuwa linatekeleza mambo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sote tunajua kwamba tunatekeleza miradi mikubwa itakayoivezesha nchi kwenda uchumi wa kati. Kwa maana hiyo, kwa kila tunachokusanya kama Taifa na kwa kila Mtanzania siyo viongozi tu; kila mtanzania anatoa mchango wake katika kutekeleza masuala haya; ni vyema sisi tulio viongozi tukaweka kipaumbele kuwaelezea Watanzania kwamba kila jambo linalotokea halitokei kwa bahati mbaya, bali linatokea kwa mpangilio kwamba tuna ajenda tunayoitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, siyo halali kwa viongozi ambao wanajua kinachofanyika kuwa wa kwanza kulalamika kwamba hatuzioni fedha za matumizi mengineyo. Tunatekeleza miradi ambayo itafanya siku zijazo tupate fedha za matumizi mengineyo nyingi kuliko za sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tunajenga vituo vya afya ambavyo havikujengwa kwa muda mrefu; siyo kwamba havijawahi kujengwa, vilishajengwa, lakini sasa hivi pia kuna vituo vituo vinajengwa maeneo ambayo hajawahi kuwa na kituo. Mfano kama Kinampanda pale hatukuwahi kuwa na kituo lakini kimejengwa. Sasa tunapokuwa tunatekeleza miradi ya aina hiyo tunatumia fedha hizo hizo ambazo tunajibana Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inapotokea kwamba tunajibana ili tutekeleze miradi ya maendeleo, wengine wasitumie kama fursa ya kutengeneza chuki dhidi

ya kundi mojawapo kwamba halijatendewa haki. Mifano inayotolewa ya watumishi wa Umma; na wenyewe ni sehemu ya mpango mkakati huu tunaotekeleza wa kuweza kuhakikisha kwamba tutakapokuwa tumeshatengeneza miradi itakayotengeneza fedha nyingi, tutaweza kujipandishia mishahara tunavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuwapandishia watumishi wa umma...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwigulu.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe ajiandae.

MHE. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Nitangulize kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri hawa kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais pamoja na kulitumikia Taifa hili kwa juhudi kubwa na kwa nidhamu kubwa. Naomba pia niwapongeze Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kuwasaidia Mawaziri na kumsaidia Rais katika kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na sekta ya afya; naomba kuchukua fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano na kuwashukuru sana Mawaziri kwa kutuwezesha sisi Jimbo la Bagamoyo kuweza kupata vituo viwili vya afya. Vituo hivi viwili vya afya kimoja kimejengwa Kata ya Kerege, kingine kimejengwa katika Kata ya Yombo. Vituo hivi vitachangia sana kutoa huduma nzuri ya afya kwa wananchi wetu akinababa na akinamama na watoto katika kata hizi na kwa

maana hiyo pia kupunguza mzigo mkubwa ambao ulikuwepo katika hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo ambayo ilikuwa inazidiwa kiasi cha kwamba inashindwa kutoa huduma nzuri. Tuliitengewa pesa nyingi jumla ya shilingi milioni 910 kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya, lakini pia tumetengewa pesa jumla ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya vifaa tiba kwa vituo hivi viwili. Nashukuru sana kwa kazi hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, hili jambo ni kubwa sana. Tunapozungumzia kuunganisha au kujumuisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi hapa ndipo ambapo kwa kweli mwananchi anaweza akaona ukuaji wa uchumi wa nchi yake na hili ndiyo jambo kubwa la kumfanyia mwananchi wa Tanzania. Mwananchi mfanyie mambo mawili; mpe elimu na mpe afya bora. Hivi vitu viwili ndivyo vinatengeneza rasilimali kuu ya nchi yetu ambayo ni mwananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakuna rasilimali zaidi ya rasilimali watu katika hii nchi yetu. Kwa hiyo niishukuru sana Serikali kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kile cha afya katika Kata ya Kerege kimeshaanza kazi na kituo cha afya katika Kata ya Yombo kinatarajiwa kuanza kazi baada ya muda mfupi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, katika Kata yetu ya Kerege ambapo kituo kimeanza kazi, lakini bado kina upungufu. Upungufu ni katika *theatre* haijakamilika na vifaa tiba bado havijakamilika, kwa maana hiyo hata upasuaji bado inabidi tuendelee kuufanya kule katika hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo. Hivyo, tunaomba tusaidiwe ili upungufu huu uweze kuondoka, tuwe na jengo la *OPD*, *theatre* ikamilike ili wananchi wetu waweze kupata huduma ile ambayo inatarajiwa katika Kituo cha Afya cha Kerege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Yombo chenye bado hakijakamilika kwa maana kinahitaji sasa samani na vifaa tiba ili kituo hiki kiweze kufanya kazi, lakini pia hakijapangiwa watumishi bado. Kwa hivyo, tumefanya kazi nzuri ya kujenga vituo hivi na nina imani kwamba, kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya na mwaka jana tulitangazwa

kuwa ni Jimbo namna moja kwa ubora wa kituo cha afya tulichokijenga katika awamu ile. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atuunge mkono ili tukamilishe na hiki Kituo cha Afya cha Yombo ili nacho kiweze kuanza kufanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho haya yanapelekea wivu pia kwa sababu afya ni jambo muhimu sana. Katika Jimbo langu la Bagamoyo, barabara hii inayotoka Bagamoyo kwenda Msata njia nzima hii kuna zaidi ya vijiji 20, Kijiji cha Makurunge, Kidomole, Fukayosi, Mwavi, Mkenge, Kiwangwa na vijiji kadhaa ndani ya Jimbo la Chalinze vyote hivi havina huduma yoyote inayofanana na kituo cha afya. Kwa hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa heshima na taadhima niombe katika bajeti hii inayokuja angalau tupate kituo kimoja cha afya katika barabara hii ya Bagamoyo kwenda Msata ambacho kiweze kuhudumia wananchi wengi katika vijiji vingi katika eneo hili, pamoja na wasafiri kama ambavyo nakumbushwa. Barabara hii imeshaanza kuwa maarufu sana na inatumika na wananchi wengi wa Kanda ya Kaskazini. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuwe na huduma nzuri ya afya katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu *TARURA*; Waheshimiwa Wabunge wamezungumza sana na hili jambo ni nyeti, ni muhimu sana Serikali ikaliangalia kwa mapana yake. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, barabara za *TARURA* zina jumla ya kilomita 332 lakini ziko katika hali ngumu sana. Mwaka huu wa fedha hakuna pesa kabisa ambayo imetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya barabara za vijijini kwa maana hiyo hatuwezi kufungua barabara, hatuwezi kuzitengeneza barabara katika hali nzuri zaidi. Kipindi kama hili cha mvua barabara zimefungwa kabisa, vijiji vimefungwa, huduma za jamii kama shule, afya na kadhalika zinakuwa mtihani kupatikana. Tumetoka safari ndefu sana ya miaka mingi iliyopita wakati Wilaya zilikuwa hazijaunganishwa kwa barabara za lami, mikoa hajaunganishwa na barabara za lami, lakini hivi sasa kwa kazi kubwa ambayo zimefanywa na Serikali zilizopita na Serikali ya Awamu ya Tano mikoa yote inafikika kwa barabara za lami na karibu Wilaya zote zinafikika pia. Sasa mkazo

tuupeleke kwenye barabara za vijijini huku ambako wananchi wanaishi na huku ambapo wananchi wanafanya kazi nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri Serikali yetu iangalie uwezekano hata wa kubadilisha mgao ule katika Mfuko wa Barabara ambao *traditionally* tulikuwa tunapeleka asilimia 70 ya *TANROADS*, asilimia 30 katika Halmashauri na kwa sasa *TARURA* ili angalau tuifanye 50 kwa 50 ili tuweze kufanyakazi nzuri zaidi ya barabara katika vijiji vyetu. Huko tutakuwa tumemkomboa mwananchi aweze kuzalisha mazao na kufanya kazi zingine zitakazotuletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie eneo la mpango wa kunusuru kaya maskini chini ya *TASAF*. Mpango huu ni mkombozi sana kwa kaya maskini, ni mpango ambao unaleta tabasamu kwa kaya maskini, yaani hakuna jambo ambalo limenifurahisha katika Jimbo langu kama pale kukutana na mwananchi wa kaya maskini naye anatabasamu...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Maghembe atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Mbene na Mheshimiwa Mussa Mbarouk ajiandae.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara hizi mbili ambazo zote kiongozi wake ni Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Napenda nipongeze sana kwa kazi nzuri ambazo zinafanywa katika

Wizara zote hizi mbili. Pia ningependa niwashukuru sana Waheshimiwa Suleiman Jafo, Mheshimiwa George Mkuchika na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kuendeleza Wizara hizi. Unaweza kuseka chochote lakini Wizara hizi zinafanya kazi nzuri sana na ni vizuri tuzipongeze, tuzipe moyo ili waendeleo kuwaletewa Watanzania maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda wenyewe wa kuongea ni mchache nitapenda sana nizingatie maendeleo kule kwenye Jimbo langu. Nikianza na sekta ya afya; napenda sana niipongeze tena Wizara hii ya TAMISEMI kwa kuvipangia ujenzi vituo hivi 95 katika bajeti hii ambayo tunaijadili sasa. Hata hivyo, Mheshimiwa Suleiman Jafo atakumbuka kwamba nilimletea rasmi kabisa matatizo niliyonayo katika Wilaya ya Mwanga katika hospitali yetu ya Wilaya ambayo awali ilikuwa ni kituo cha afya na kupandishwa kuwa hospitali ya Wilaya, Mwanga ilipokuwa Wilaya, kwamba tangu mwaka 1979 hadi leo hakuna kitu kingine kilichofanywa juu ya kituo cha afya kubadilishwa kuwa hospitali ya Wilaya. Hivi sasa majengo yamechakaa, *theatre* zimechakaa, vitendeakazi vimechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Jafo kwa kutuma timu ambayo ilikwenda ikafanya tathmini ya hospitali ile na kuona matatizo yaliyopo, lakini katika orodha hi ya hospitali 95 siioni hospitali ya Wilaya ya Mwanga. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri tafadhali ikiwezekana twende sisi wawili tukaangalie pamoja ili uone shida kubwa ambayo ipo. Hivi sasa *theatre* karibu inafungwa kwa sababu hakuna vitendeakazi, hakuna vifaa tiba, *mortuary* jengo limeanguka na majengo kwa ajili ya kuwapa uhifadhi wafanyakazi, nyumba za wafanyakazi hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie kama anavyosaidia kwenye Wilaya zingine ili hospitali hii iweze kutumika vizuri. Aidha, naendelea kushukuru na kupongeza sana katika hatua kubwa zilizofanywa za kujenga na kuboresha vituo vya afya na sisi katika Wilaya ya Mwanga awali tumepata shilingi bilioni

1.4 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kisangara na Kituo cha Afya cha Kigonigoni. Tunaendelea kushukuru na fedha ambazo zimepangwa katika bajeti hapa kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya cha Kifaru. Hata hivyo, bado wananchi wa Mwanga wamejenga vituo vingine viwili ambavyo ni karibu kumaliza kama hicho cha Kifaru, Kituo cha Afya cha Mwaniko na cha Kileo ambapo tunawaomba sana fedha zikipatikana basi tuwasaidie wananchi kukamilisha. Wameshajenga, wamebakiza vitu vidogo sana ambavyo wangetupatia shilingi milioni 400 hivi, basi maneno yote yangukuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika sekta hi ya afya, wananchi wa vijiji sita katika Wilaya ya Mwanga wanaendelea kujenga zahanati na karibu zinakamilika. Zahanati hizi za Kituri, Mrigeni, Lembeni, Nyabinda, Lang'atabora na Vanywa ziko karibu kabisa kukamilika, wananchi wamejenga mpaka wamepaua lakini wamechoka. Tunawaomba sana katika huu utaratibu wa kumaliza maboma, ya kwao siyo maboma wameshapaua, basi watusaidie kukamilisha zahanati hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kubwa ambalo nataka niliongelee ni suala la elimu. Katika Wilaya ya Mwanga na hasa katika elimu ya msingi nimesema hapa mara nyingi shule zetu hazina Walimu kabisa. Kati ya shule 117, shule 50 zina Walimu wawili, wawili peke yake na shule zingine 40 zina Walimu watatu, watatu, sasa utapiga hesabu mwenyewe uone ni ngapi ambazo zina Walimu wanne. Hakuna shule ambayo ina zaidi ya hapo labda zile ambazo ni za watoto wa mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Mwanga hatuhitaji Walimu wapya. Tunachoomba Serikali itupe ni Walimu ambao watachukua nafasi za Walimu waliostaafu, wale ambao wamefariki au wale ambao wamehamishwa na Serikali kwenda maeneo mengine kufanya kazi. Kwa hivyo, sioni sababu ya kuchukua mwaka na nusu kulishughulikia jambo hili. Watoto wanateketea, wanapotea, hawana Mwalimu wa kuwafundisha, Walimu wawili wakiingia kwenye

madarasa saba, watoto wa madarasa matano wanabadilisha shule inakuwa soko. Kwa hivyo, tunawaomba sana, hatuombi Walimu wapya, mishahara yao ipo kwa sababu wale waliokuwepo walikuwa na mishahara na hakuna sababu yoyote ya kutotupa Ealimu kwa sababu Ealimu wako barabarani hawana kazi. Kwahiyo nawaomba tena...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa kwa mchango wako mzuri.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbene atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarouk na ajiandae Mheshimiwa Mbatia

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hizi mbili muhimu sana. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku njema, lakini vilevile nataka kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizi mbili, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hizi muhimu sana kwa mustakabali na maendeleo ya nchi yetu. Hizi ni Wizara ambazo unaweza ukasema ni pacha; moja inasimamia Utumishi na Utawala Bora, nyingine inasimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya halmashauri na miji yetu. Kwa hali hiyo, kuna haja kubwa sana ya kuhakikisha kuwa kwanza zinawezeshwa kifedha, lakini vilevile kimfumo na pia kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza hivyo kwa sababu tunapozungumzia utumishi na tunaposikia michango yote ya Wabunge ikilalamikia watumishi na upungufu wake nafikiri

kuna haja sasa ya kuchukua hatua ya makusudi ya kimkakati ya kujaza hizi nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa la watumishi katika Wilaya zetu hasa kwenye sekta ya afya, kwenye sekta ya elimu, kwenye sekta ya maji yaani karibu kila sehemu ina matatizo ya upungufu wa watumishi. Mimi binafsi katika wyangu nia upungufu mkubwa sana wa Walimu katika shule za msingi na shule za sekondari, lakini hasa hasa katika shule za sekondari ni Walimu wa sayansi. Tuna tatizo kama alilolisema Mheshimiwa Maghembe kuwa sehemu nyingine ni kujaza nafasi tu za watu ambao wameondoka aidha kwa kustaafu, au kwa kufa, au kwa kuhama. Sasa hili ni jambo ambalo naamini halipaswi kuchukua mlolongo mrefu kama vile ambavyo tunavyongojea vibali vya ajira mpya labda nisahihishwe kuwa hivyo sivyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitakuwa mtovu wa shukurani kama sikutoa shukurani zangu kwa jinsi ambavyo wilaya yetu imepatiwa fedha ya kumaliza hospitali ya wilaya ambayo Awamu ya Nne tulipata fedha kwa ajili ya kuianza na sasa hivi tumepata bilioni moja na milioni mia tano kwa ajili ya kuimalizia. Naamini fedha hii itatosha kumaliza hospitali, itajenga nyumba za Wauguzi na vilevile kumaliza miundombinu yote iliyokuwa inahitajika, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashukuru kwa kupata fedha ya vituo vya afya viwili vikubwa na tumeahidiwa kingine cha tatu, lakini niombe tupate na cha nne kwa sababu wilaya yangu mimi ina tatizo la miundombinu migumu; milima, mabonde na umbali kati ya kata moja kwenda nyingine. Hii kwa vyovyote vile inasababisha umbali kuwa mkubwa na bila kuwa na zahanati za kutosha hata vituo hivi vya afya vinaweza visisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye zahanati; tulikuwa tumeweka kwenye bajeti yetu milioni 200 kwa ajili ya kukarabati maboma ya zahanati saba ambayo ilishapitishwa kuwa zitakuwepo, lakini ghafla tukaja kuambiwa tuziondoe katika bajeti yetu kwa sababu zinapelekwa Mbozi

na Songwe. Hii imetuathiri sana kwa sababu haya maboma ya zahanati yameshafikia mahali pazuri kumaliziwa na hizi fedha tulikuwa tumeshazitarajia kwa sababu zilikuwa zimeshakubaliwa sasa kuja kuziondoa tu juu juu hivi zinatathiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Wilaya yangu miundombinu ni migumu, usipokuwa na zahanati hata ya kuanzia tu kumtibu mwananchi kufikia vituo vya afya ni tatizo hasa wakati wa mvua. Naomba sana Wizara ya TAMISEMI mliangalie hilo na mturudishie ile shilingi milioni 200 ambayo mlikuwa mmeitoa wakati tayari tulikuwa tumeshakubaliana kuwa itakuwepo katika *ceiling* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kushukuru kwa fedha iliyotolewa kwa Daraja la Mwalisi ambalo linaunganisha Wilaya yangu na Mgodi wa Kiwira. Hili daraja litatusaidia kwa sababu ilibidi kutoa makaa ya mawe na kuyapitishia Kyela na huko ilikuwa ni Wilaya nyingine *of course* na ilikuwa inaleta gharama kubwa na usumbufu kutokana na umbali wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala la *TASAF*. *TASAF* imekuwa msaada mkubwa sana kwa nchi nzima na hata kwa Wilaya yangu. Nataka niombe vile vijiji 21 kati ya 71 ambavyo havijaingizwa katika mpango huu basi na vyenyewe viweze kuingizwa kwa sababu faida zake zimeonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nataka niongelee suala zima la TAKUKURU au masuala mazima ya ufisadi au rushwa. Tunashukuru kuwa imeanzisha Mahakama ya Ufisadi lakini kiwango cha watu wanaopelekwa pale cha bilioni moja ni kikubwa sana, mafisadi wengi sana wanaachwa hapa chini hawawezi kufikia Mahakama hiyo kwa sababu hawajatuhumiwa kwa kiwango hicho kikubwa. Kiwango hiki kingepunguzwa kidogo mafisadi au watuhumiwa wengi zaidi wangeweza kufikiwa na rushwa ikapungua lakini bado rushwa ipo na inalalamikiwa sana, tusijidanganye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo juhudi zinafanywa lakini bado rushwa nyingi ni tena inafanywa waziwazi katika taasisi zilezile ambazo zimekuwa zikilalamikiwa siku zote Polisi barabarani, Mahakama na sehemu zinazotoa huduma za afya na hata elimu. Naomba sana tusielegeze kamba rushwa bado ipo, wanagundua misemo mipya, ohoo, sijui kula samaki gizani, kuna maneno yanayotumika ambayo hayatufurahishi kwa sababu rushwa inaondoa haki za kimsingi za watu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuzungumzia suala la watumishi. Watendaji wakubwa katika taasisi mbalimbali wanahitaji kupata mafunzo ya kutosha ya uongozi. Tulikuwa na vyo vyetu vilikuwa vinatoa elimu hiyo lakini najua sasa hivi tuna *Uongozi Institute*, napenda sana kuona mpango mkakati wa jinsi gani ya kuwapeleka watendaji hawa kwenda kujifunza kwa sababu pamoja na kuwa ni viongozi wa taasisi mwenendo hauoneshi ile *leadership* ambayo inategemewa kwa viongozi wa ngazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo linaanza kuzoeleka la Watendaji Wakuu wanaopata nafasi kuhamishwa kwenye taasisi aliyokuwa mwanzo kuanza kutengeneza himaya zao, wanaondoka na watu wao wote waliokuwa nao kwenye taasisi moja wanawahamishia kwenye taasisi nyingine na kuleta sasa tabaka za waliokuwepo na waliokuja, hii inaleta chuki na inavunja moyo wale waliokuwepo. Mimi nafikiri suala hapa ni kujenga taasisi imara siyo kujenga Watendaji Wakuu wa taasisi imara. Kwa hiyo, naomba hili pia liangaliwe la huu mtindo watu kuhama na ma-*secretary* wao na viti na meza za maofisini kama vile wanahama nchi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Kiswaga watafuata.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezeshwa kuwa na afya njema na kuweza kukutana katika kikao chetu hiki cha Bunge na kuzungumzia mambo mbalimbali ya nchi yetu. Pia nishukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Tanga bila kukusahau wewe kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuchangia TAMISEMI, labda nami niwe miongoni mwa wale ambao tunashukuru kwa ule mpango wa kujenga vituo vya afya 300. Kwenye Jimbo langu la Tanga tumepata vituo vya Makorola, Mikanjuni na Ngamiani. Tumepata takribani shilingi bilioni moja na milioni mia nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia nisisahau kwamba tulikuwa mgogoro wa Hospali ya Wilaya ijengwe sehemu gani. Baada ya kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri hapo mambo yamewekwa sawa na sasa ujenzi unaendelea. Nishukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye suala la elimu hususani elimu bure. Elimu bure mimi niseme imepigwa debe sana lakini wananchi na wazazi bado hawajaiielewa vizuri na hata badhi ya Wabunge nafikiri hawajaiielewa vizuri kwa saabu unaposema kitu bure ni ile *free no charge* sasa wazazi kufuatia suala hilo wamekuwa wazito kuchangia masuala ya umeme na maji, fedha ya mlinzi na hata akuchangia vifaa. Unapowahoji wanakwambia kwamba tumeambiwa elimu bure na ndiyo maana watoto wameongezeka sana katika shule zetu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niitake Serikali sasa, kwa sababu watoto tumekuwa kama tunawaadhibu katika baadhi ya shule maji yamekatwa kwa sababu kufuatia kauli ya Mheshimiwa Rais ile anayosema maneno ni mawili 'Kata'

kwamba panapodaiwa maji na umeme kata. *TANESCO* na Mamlaka za Maji sasa hivi hazitoi huduma zinafanya biashara matokeo yake umeme na maji katika shule yamekatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake tunawaadhibu watoto. Wanafunzi hawa masikini ya Mungu, malaika wa Mungu hawana hata maji ya kunywa shuleni wanalazimika ama kubeba chupa za maji katika mabegi yao wanayoweka madaftari au kama wako shule basi pana nyumba ya jirani karibu waende wakaombe maji ya kunywa katika nyumba za jirani. Naiona hii ni hatari kwa sababu katika baadhi ya nyumba kuna watu wengine siyo wema, mathalani watoto wa kike tunaweza kuwahatarisha maisha yao kwa kubakwa na kupata maradhi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isiongeze fedha katika ule mpango wa kupeleka *capitation* na fedha za matumizi katika shule tukaweza kulipia maji na umeme kwenye shule zetu? Au kwa nini Serikali isisamahe kwenye shule za msingi na sekondari lakini nifike mbali zaidi hata kwenye Misikiti na Makanisa kule ambako Mwenyezi Mungu tunamwomba nchi iendelee kuwa amani tuweke huduma ya maji na umeme iwe bure? Kwa hiyo, naishauri Serikali lifanyiwe kazi suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa nini pia tusiwape umeme wanafunzi wakaweza kutuumia katika kujifunza kwa sababu kuna mambo mengi. Sote tumepitia elimu ya msingi panakuwa na umeme mnajifundisha mambo mengi, sote tumeyaona haya. Kwa hiyo, naiomba Serikali hilo walifanyie kazi na tuliambiwa kwenye bajeti ya mwaka jana kwenye Wizara ya Nishati na Madini kwamba kwenye huu umeme wa *REA* watahakikisha kuwa shule zote nchini zinawekwa umeme, naliomba suala hilo liharakishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nalotaka kulizungumzia ni suala la dawa. Tumeona dawa zilitengewa takribani shilingi bilioni 531 lakini fedha iliyopokelewa ilikuwa

ni shilingi milioni 81, pana tofauti ya takribani shilingi bilioni 450. Kama ikiwa tunatenga fedha kubwa halafu fedha tunayopeleka ni kidogo hatuwasaidii wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hakuna haja ya kuweka kasma kubwa halafu tunapelekea asilimia ndogo ya fedha. Kama tumepanga shilingi milioni 5312 basi angalau kungepelekwa shilingi milioni 400 hapo ingekuwa tumewasaidia lakini katika shilingi bilioni 531 kupeleka shilingi milioni 81 tu tunawakwaza ama madaktari na watumishi wetu wa Idara ya Afya. Kwa hiyo, naiomba Serikali pale inapopanga bajeti ihakikishe fedha inapatikana na inapelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Mfuko wa Maji, Tanga tunayo miradi ya maji ya ile vijiji 10 kila Halmashauri lakini kwa masikitiko makubwa niseme upande wa Kusini tulifanikiwa, maji yanatoka kuelekea upande wa Marungu, Kirare, Tongoni na wananchi sasa hivi wanaomba huduma ya maji ipelekwe mpaka kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika mradi wa Kaskazini wa Mabokweni, Kibafuta, Mpirani na Chongoleani mpaka leo kuna kizungumkuti, maji hayatoki na wananchi wana shida ya maji na mimi mwenyewe nimefika nikashuhudia. Nitamwomba tu Mheshimiwa Waziri wa Maji au Naibu wake mara baada ya Bunge hili tutembelee ili tujue kikwazo kwa nini maji hayatoki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mradi huohuo wa maji, Kamati PAC ambayo nipo tumetembelea mradi wa maji ule wa Chalinze na maeneo mengine naona kuna hitilafu kidogo kwa sababu fedha zilizoahidiwa katika mkopo ilikuwa ni takribani shilingi bilioni 158 mpaka sasa hivi zimetumika shilingi bilioni 93 lakini kuna shilingi bilioni 65 bado hazijatumika. Hata hivyo, kuna masharti ambayo katika miradi ile vifaa vyote hadi *bolit* lazima itoke kwa yule mtu ambaye mmeingia naye mkataba kwamba awakopeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ule mradi unafadhiliwa na India sasa basi hata mipira, *bolt*, nati za kwenye mradi lazima zitoke India! Tunasema tunalinda viwanda vya ndani, tunalindaje viwanda vya ndani kwa miaktaba mibovu kiasi hiki? Ina maana watumishi sasa baadhi ya ma-*expert* ambao wapo hata Watanzania wanashindwa kulipwa sawasawa na wale ma-*expert* wa Kihindi, naona hiyo ni dosari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie utawala bora. Ukitazama Katiba, Ibara ya 146(1)(2)(c) kinaeleza hapa kwamba, madhumuni ya kuwepo Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi na vyombo vya Serikali za Mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa ujumla. Ukienda kwenye kipengele (c) inasema...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: *Thank you.* Tunaendelea na Mheshimiwa Mbatia atafuatiwa na Mheshimiwa Kiswaga na Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi nitoe mawazo yangu kwenye hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa leo ni *Sokoine Day*, alikuwa kiongozi mashuhuri kwa Taifa letu, ni siku ya kumkumbuka miaka 35. Mwenyezi Mungu amrehemu na tutekeleze yale mema aliyofanya kwa Taifa la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraharaka nianze na *TARURA*. Nimpongeze Mtendaji Mkuu wa *TARURA* kwa kazi nzuri kubwa anyoifanya kwa Taifa letu na *TARURA* Halmashauri ya Wilaya ya Moshi wanafanya kazi nzuri. Nachowakumbusha tu ni ahadi za Mheshimiwa Rais kwa barabara za Himo Mjini pamoja na barabara ya Kilema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Vunjo lina barabara zenye kilometa 389.3, *TARURA* walifanya kazi hii ya kupima, nawapongeza sana, wakishirikiana na *Vunjo Development Foundation (VDF)* na barabara hizi zitagharimu shilingi bilioni 12.7, wananchi wameanza kuchanga wenyewe, Mbunge nimenunua mashine, Serikali imeahidi kutoa shilingi milioni 200 kwenye mradi huu kwenye barabara walizoweka kwenye kitabu, naipongeza Serikali. Hata hivyo, shilingi milioni 200 kati ya shilingi bilioni 12.7, naomba waongeze fedha hizi. Waliotengewa shilingi milioni 200 ni barabara ya Chekereni - Kahe ambayo tunashukuru lakini ni kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni elimu msingi, nimeuliza swali asubuhi, naomba tu kujua na tulitendee Taifa haki, hapa tuna Sera ya Elimu na inafafanua vizuri maudhui ya Sera ya Elimu na elimu msingi ni ipi na elimu sekondari ni ipi. Je, Taifa hili leo hii linaongozwa na Sera ipi ya Elimu kuandaa Taifa kwa miaka 30, 40 au 50 ijayo? Nitazungumzia zaidi wakati wa bajeti ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongele kuhusu ikama ya watumishi. Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kuna upungufu wa walimu 379, shule zingine zina walimu wawili, watatu na sekta ya afya pia ina matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tuko na wenzetu wenye *albinism*, niwapongeze kwa kazi nzuri wanayoifanya na mwaka huu ni wa kudumisha, kutetea na kulinda utu, heshima na mahitaji msingi ya watu wenye ulemavu. Nikiangalia bajeti iliyoletwa hapa bado walemavu wetu hatujaweza kuwaweka kwenye hali ya utu wao, heshima yao na mahitaji msingi yao ili na wao wajione ni binadamu. Sisi ambao tunajiona tuna akili nzuri na tumekamilika tunawaita

walemavu lakini kwa kiasi kikubwa ukiangalia sisi tunaowaita walemavu ulemavu wetu wa fikra ni mkubwa kuliko ulemavu wao wa viungo vya nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimponge sana Dkt. Reginald Mengi na Taasisi yake ya kutetea na kukuza utu wa walemavu. Dkt. Mengi anafanya kazi nzuri sana na niombe Serikali imuunge mkono. Tulikuwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais tarehe 17 mwezi uliopita na Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Stella Ikupa katika shughuli ya kuwajengea utu walemavu, kwa hiyo wapewe nafasi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye mkutano wa Dkt. Martin Fatael Shao, Askofu Mstaafu naye amefanya utafiti kwenye sekta ya afya na watoto na imeonekana shule zetu haziko vizuri. Kwa kuwa nina ripoti yake hapa, nampongeza Askofu huyu kwa kazi nzuri anayofanya kwa walemavu, shule za msingi, elimu ya afya na kitabu hiki nitakiweka Mezani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka niingie kwenye utawala bora. Ndugu Isaac Newton anasema katika kila kanimkabala kuna kani iliyo mrejeo sawa na kinyume. Viongozi wowote wale hawaokotwi kwenye majalala viongozi huandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1995 wewe ulikuwepo Bungeni, alikuwepo Mheshimiwa Mzee Lubeleje, Mheshimiwa Ndassa na Mheshimiwa James Mbatia kati ya Wabunge wote waliopo sasa, tulikuwa wanne. Wakati huo tulivyokuwa Bungeni ukiwa Mwanasheria Mkuu viongozi waliandaliwa kwa kupewa semina na kuelezwa jukumu la kwanza la Mbunge ni kwa Taifa lake; la pili kwa Jimbo lake la Uchaguzi; la tatu kwa chama chake cha siasa; na la nne kwa dhamira yake binafsi.

Sasa hapa Bungeni leo hii watu wanachukulia mambo *personal* kana kwamba *issues* ni *personal*, sisi tunapita tu, tuijenge nchi yetu, wanasema *great minds discuss ideas*, Taifa hili ni letu sote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilibahatika kuongea na Mheshimiwa Rais kwa mapana sana tu tukakubaliana Taifa hili likiharibika au likienda mrama tunaangamia sisi sote, halichagui huyu ni wa chama gani, kwa hivyo, tuitazame nchi yetu. *Let us think positive and big, let us think big* yaani tufikiri kwa mapana tu, nchi yetu miaka 50 itakuwa kwenye hali gani. Kapteni Mstaafu Mheshimiwa Mkuchika unakumbuka mwaka 1992, 1995 ukiwa DC wa Ilala wakati tunaanzisha mfumo wa vyama vingi tulikuwa tunakuja ofisini kwako, tulikuwa tunaongea tuwe na Taifa gani baada ya miaka 25, miaka 30 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimesema hayo? Nimesema hayo kwa sababu nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Kapteni Mheshimiwa Mkuchika, ukiangalia Taasisi ya Kupambana na Rushwa kazi walizonazo hapa ni zaidi ya 10 au 15 kama sijakosea lakini ukiangalia bajeti yao ni ndogo kweli kuweza kuzama mpaka chini. Kauli mbiu ya taasisi hii nilikuwa nao wiki iliyopita kwenye semina na dada yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri pale TAKUKURU, tulitoa rai, huwezi ukasema unazuia, unapambana halafu ndiyo unaelimisha, hapana. Nilitoa rai siku ile kwamba tuanze na kuelimisha kwanza madhara ya rushwa. Tukishaelimisha ndiyo tutaenda sasa na hayo mengine ya kuzuia na kupambana, tuelimishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusiseme hapa kwamba kesi ziko 476 na nyingine zinaongezeka tujenge mazingira kesi zipungue zaidi kwa sababu ya watu kujua madhara na kujijelimisha zaidi badala ya kufikiri kwamba zitaongezeka.tuwekeze kwenye kuondoa maovu zaidi kwenye jamii badala ya kufikiria maovu yataongezeka kwenye jamii. Hii ni namna ya jamii kujitambua na kwa moyo wa dhati kabisa nimpungeze CP Diwani Athumani na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuweza kupambana na rushwa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii ukiangalia kwenye uongozi baada ya rushwa, unaona wamepewa majukumu nane ambako tungewekeza zaidi kwenye taasisi

ukurasa ule wa 80, tulishakubaliana tangu mwaka 2002 na Komredi Mangula, Katibu Mkuu wa CCM, wakati huo tuko kwenye *TDC*, nimpongeze sana Nsanzugwanko waanzilishi wa *TDC (Tanzania center for Democracy)* tulikubaliana Taifa liandae viongozi. Ukiangalia ma-*RC*, ma-*DAS* na ma-*DED* wetu wanaibukaje, *vetting* yao ikoje katika utumishi wa umma wa Tanzania ili waweze kuwa ni endelevu katika kutekeleza majukumu yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwa ma-*DC* na Ma-*RC* wetu, tumpongeze Kapteni Mheshimiwa Mkuchika uliwahi kuzungumza hapa, wanaandaliwaje, wanapikwaje ili waweze kutekeleza majukumu ipasavyo? Kwa hiyo, wasiibuke tu kila mtu na mambo yake, huyu anasema hili, yule anasema lile, kwa kweli tukiangalia kama wataendelea kufanya wanavyofanya tutakuwa hatulitendei Taifa letu haki. Mheshimiwa Mwenyekiti,

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali kubwa kuliko zote duniani leo hii ni rasilimali watu (umoja) na utawala bora *is a collective approach* inaanzia kwangu, kwako, kwa jamii nzima, kwa familia baadaye kwa Taifa. Mwalimu alikuwa anajua kwamba Taifa analipeleka wapi ndiyo wanafunzi tukawa tunaimbisha kama kasuku ahadi za mwana-TANU, unaambiwa binadamu wote ni ndugu zangu, unajua kuwa huyu ni ndugu yangu; unambiwa rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala sitatoa rushwa, tulikuwa tunapata Taifa ambalo linaendelea, ni shirikishi, la wote kwa kuwa nchi hii ni yetu sote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujitambua ni jambo muhimu sana na inatupasa sisi sote kwa pamoja kujua utawala bora ni wa pande mbili; anayeongoza na anayeongozwa, *is a collective approach*. Huwezi ukauchukulia utawala bora kwa yule tu anayeongoza. Ukikubali mawazo mbadala ukawa na utulivu; nimeona hata hapa Bungeni, unakuta Mbunge anaongea, mwingine amemwingilia, mwingine amefanya hivi. Hata Maandiko Matakatifu yanasema kujibu kabla ya kusikiliza ni upumbavu na aibu kwako ambaye hujataka kusikiliza. (*Makofi*)

Tusikilizane, tuvumiliane, tuwe na lugha ya staha. Taifa hili ni letu sote. Tukiwa na mawazo mapana namna hiyo, ninaamini hapa tulipo leo hii tutatoka na Tanzania ya leo, nani mwenye kujua kesho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Taifa endelevu kwa maslahi mapana ya mama Tanzania. *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbatia, nakushukuru sana kwa mchango wako, ahsante sana. Ndiyo maana ya uongozi. *(Makofi)*

Tunaendelea, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Ajali Akbar Rashid wajiandae. *(Makofi)*

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii. Moyo usio na shukrani hukausha mema mengi. Napenda kuwapongeza Mawaziri; Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Mkuchika na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na Wakuu wa Taasisi wanazoziongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jambo hili kwanza napongeza kwa sababu nimepata vituo viwili vya afya; na cha kwanza kiko hapa cha Kahangara kwenye mfano wa hotuba hii. Bado nina vituo vya afya vitatu; Kituo cha Afya cha Kabila pamoja na Kituo cha Afya cha Kisesa na Nyanguge. Vituo hivi ni muhimu sana, Serikali ione namna ya kuweza kunisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Mbatia anachangia hapa, ndiyo maana nimeanza na moyo usio na

shukrani; Mheshimiwa Mbatia ameishukuru Serikali hii. Kama wapinzani wa nchi hii wangekuwa kama Mheshimiwa Mbatia, upinzani ungeweza kusaidia nchi. Kwa sababu michango aliyoitoa ni kwa maslahi ya Taifa hili. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inaendelea kuboresha huduma. Kwenye hospitali, ninajua mnaendelea kujenga hospitali mpya, lakini hata hospitali yangu ya Magu, Mheshimiwa Jafo ni shahidi amefika mara mbili, inahitaji ukarabati. Kwa sababu tumezungumza naye ninaamini jambo hili atalichukua kwa uzito wa pekee kwa sababu yeye ni shahidi amefika *OPD*, inaweza kuanguka wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye barabara. Magu tuna kilometa za barabara 1,600. Kwenye bajeti hii tumepangiwa shilingi milioni 900, hazitoshi hata kidogo. Naiomba Serikali, kwa sababu *TARURA* inapokea asilimia 30 na *TANROADS* inapokea asilimia 70, wanganalie namna ya kubadilisha sheria ili mradi *TARURA* ipate asilimia 50 na *TANROADS* ipate asilimia 50 ili barabara zetu za wilayani kule ziweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumpongeza sana *Chief* wa *TARURA* ni msikivu. Ukimpigia simu wakati wowote anapokea, naye anazunguka kwenye barabara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna daraja pale Mahaha, Itubukiro kwako kule, tunaunganishwa na daraja, halipo. Ili kuunganisha mawasiliano ya kiuchumi ni vizuri waanganalie *TARURA* namna yoyote ambayo wanaweza kutusaidia madaraja ili tuweze kuunganisha hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna barabara ya Magu – Isolo, kuanzia Kabila – Isolo na Isawida kule kutokea Itilima, pale tunatenganishwa na daraja. Magu tumelima mpaka kwenye mpaka wa Itilima na Itilima imelima mpaka kwenye mpaka wa Magu; *TARURA* ninakuomba utupatie daraja na tulikuja ofisini kwako na Mheshimiwa Njalu kuomba pale utupe

daraja ili tuweze kuunganisha mawasiliano ya wilaya hizo mbili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magu tumejenga maboma vijiji 21 ambayo yako tayari, zinahitajika fedha za kuweza kukamilisha na hili ni la ki-llani. Tulisema llani ya Chama cha Mapinduzi kila kijiji kiwe na zahanati, wananchi wameitikia, wamejenga, wanahitaji kusaidiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii kama ambavyo inafanya kazi, iangalie namna ya kutoa fedha kwa ajili ya maboma ya nchi hii ikiwemo Wilaya ya Magu ili tuweze kuwapa nguvu wananchi kwa kazi ambazo wamezifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkanganyiko wa waraka. Waraka uliokuja unasisitiza nyaraka zilizopita, lakini Wakurugenzi wameshindwa kutafsiri waraka huu. Wamefuta *per diem* wamekwenda kusisitiza kwenye *sitting* pekee. Madiwani hawa ni viongozi, ndio wanaofanya kazi, ndio Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo za Kata, ni vizuri tukawaona. Kwa sababu hawa huwa tunachagua nao siku moja, ni vizuri tukawapa maslahi yao ya kweli. Kuna Diwani anatoka kilometa 40, kuna Diwani anatoka kilometa 20; wao wameangalia tu pale mwisho kwamba kama kuna uwezekano wa kutolala wasilipwe *per diem*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mbunge. Mbunge na Diwani kila kunapokucha asubuhi watu wanajaa ukiwa Jimboni au kwenye Kata yako. Ndiyo maana ikawekwa *per diem* ili Diwani atoke kwenye familia yake aende akalale Makao Makuu ili *concentrate* vikao vya Halmashauri. Kwa hiyo, *per diem* hii wanapaswa walipwe Waheshimiwa Madiwani hawa. Madiwani hawa hakuna sherehe inayompita, hakuna kilio kinachompita na hakuna mgonjwa anayempita. Mimi nilikuwa Diwani na sasa ni Diwani kwa mujibu wa sheria kwa sababu ya Ubunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege uko hapo. Kandege andika hili,

Kandege andika hili, mtafasiri waraka huu, ili Madiwani waweze kulipwa *per diem* yao. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga naona umepandisha? Mwrite tu Mheshimiwa Kandege.

MHE. MUNGE FULANI: Aongezwe dakika huyu.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze kwa mamlaka uliyokuwanayo.

MWENYEKITI: Tumia basi lugha ya Kibunge, mwrite Waziri Mheshimiwa Kandege.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Kandege. Mheshimiwa Kandege. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Tena, rudia!

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Kandege, sikiliza hili na aandika ili mtafasiri waraka huu Madiwani waweze kulipwa *per diem*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sauti yangu ni ya msisitizo, nasisitiza tu, siyo kwamba, labda nafoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye *Service Levy*. Hii *Service Levy* wakati inatungwa Sheria ya Serikali za Mitaa ilikuwa inalenga viwanda. Kwa mfano, kama kiwanda cha *Tanga Cement* kimezalisha simenti na inauzwa hapa Dodoma, Halmashauri ya Dodoma ina-*claim* madai yake ya *Service Levy* Tanga. Leo *Tanga Cement* kama hapa Dodoma ina tawi, inatozwa hapa, akinunua Dodoma hapa kupeleka Mvumi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kiswaga.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa...

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naunga mkono hoja. Kumbe dakika 15 ni muhimu sana.

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Gulamali, halafu Mheshimiwa Akbar na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu wajiandae.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI na Utawala Bora. Kwanza napenda kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambazo inafanya, ama miradi mikubwa ambayo inatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona miradi kama *Stieglers Gorge* ambapo kwa ukamilishaji wa mradi huu tutapata Megawati kama 2,100 za umeme, tunaona ujenzi wa *Standard Gauge (SGR)*, ujenzi wa kisasa wa reli yetu, tunaona usambazaji wa umeme vijijini, vijiji vyote vitapata umeme, tunaona vituo vya afya na hospitali karibu 67 zinajengwa nchi nzima. Miradi hii yote ikikamilika, ninaamini Tanzania itakuwa kati ya nchi 10 bora katika Bara la Afrika *out of 54 countries. (Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo za Serikali katika kutekeleza miradi mikubwa, binafsi naunga mkono na wananchi wa Jimbo la Manonga wanaunga mkono harakati zote za Mheshimiwa Rais kupeleka nchi yetu katika uchumi wa kati. Sasa nianze kwa maombi yangu kama Wilaya na Jimbo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya TAMISEMI, kwanza nawashukuru kwa kunipatia fedha kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Simbo. Kituo kimekamilika, sasa

kilichobaki ni vifaa tiba. Naiomba Wizara ya TAMISEMI itulettee vifaa tiba katika Kituo chetu cha Afya cha Simbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nawaomba Wizara ya TAMISEMI, Jimbo letu ni kubwa sana. Mwaka 2018 Agosti, alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu Jimboni, alituahidi kutupatia fedha shilingi milioni 400 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Choma cha Nkola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Choma baada ya Hospitali ya Wilaya ya Igunga kinachofuatia ni Kituo cha Afya cha Choma ambacho kinafanya *operation* ndogo ndogo. Karibu *operation* 150 wamekwishafanya, lakini changamoto iliyoko pale hatuna jengo la akina mama na watoto, hatuna jengo la kufulia nguo, hatuna *mortuary*, hatuna *ward* ya akina baba. Kwa hiyo, bado *operation* hizi wanapata changamoto sehemu ya kuwahifadhi wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, nimeangalia kitabu chake sijaona bajeti ya fedha ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi katika ziara yake. Tunaomba fedha kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa Kituo cha Afya cha Choma cha Nkola ili kuweza kuhakikisha kwamba tunasogeza huduma bora kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona bajeti hapa ya Wizara ya Afya. Tumetenga fedha za ujenzi wa hospitali katika Wilaya mbalimbali nchini. Wilaya yetu ya Igunga Makao Makuu ya Wilaya ni Igunga. Pale tuna hospitali ya wilaya. Hospitali yetu imechakaa sana, hatujapata fedha za maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri tuangalie katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga, hatuna *ambulance*. Nilinunua *ambulance* nikapeleka kwenye Kituo changu cha Afya cha Simbo. Sasa inachukuliwa ile *ambulance* ya kijijini, kwenye Kituo cha Afya cha Simbo, inaletwa mjini. Kwa hiyo, ile adha ambayo nilikuwa nimeenda kupunguza kwa wananchi inakosekana. Tunaomba *ambulance* ya wilaya iletwe, ili iweze kuhudumia kwa sababu

mahitaji ni makubwa na katika makao makuu ya wilaya watu ni wengi sana wanahitaji kupata huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena tupate fedha kwa ajili ya kuongeza matengenezo kwani hospitali ya wilaya imechakaa, haina uzio, hakuna maabara ya kisasa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu, mpo hapo Wizara ya TAMISEMI, mtupatie fedha kwa ajili ya kuboresha hospitali yetu ya wilaya ili kuboresha na kusaidia kupatikana huduma za afya katika Wilaya yetu ya Igunga, hasa Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kwenye shule za Serikali za wasichana. Tumeona ujenzi wa shule za Serikali za wasichana zikijengwa maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Tabora Mjini tunayo natambua iko *Tabora Girls*, nimeona Nzega pale imejengwa. Naomba sasa, katika Wilaya yetu ya Igunga hatuna shule hata moja. Mimi binafsi katika Jimbo langu niko tayari na tuko tayari kutoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa shule, tukishirikiana na TAMISEMI, tutajenga pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba shule hizo za wasichana zijengwe katika Wilaya yetu ya Igunga pale Choma cha Nkola iweze kusaidia watoto wa kike wanaotembea umbali mrefu kutoka vijijini, kilometa nyingi kuja shuleni. Kwa hiyo, tukijenga shule hii itasogeza huduma, lakini itawarahisishia watoto hawa wa kike kukaa shuleni na kusoma kwa utulivu, itasaidia kuongeza ufaulu wao katika maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachilia mbali hilo, niombe TAMISEMI, tuna upungufu wa ma-*engineer*. *Engineer* (mhandisi) wetu wa Wilaya tuliyenaye kwa masuala ya majengo inawezekana uwezo wake ni mdogo. Naomba TAMISEMI mtuletee *engineer* ambaye ataweza kutusaidia kuweza kusukuma hizi kazi za Kiserikali ambazo mmetuletea fedha ziweze kwenda kwa usahihi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia *engineer* wetu, tunanunua vifaa vingi sana mwisho wa siku vinabaki

store, halafu inakuwa ni hasara katika maeneo yetu. Mfano ni Kituo cha Afya cha Simbo, tumenunua vifaa vingi hali ambayo imesababisha hata fedha tuliyonayo tumeshindwa kuwalipa wakandarasi wanaotudai. Naomba TAMISEMI ituletee *engineer* ambaye ataweza kwenda na hesabu ambazo zitaweza kukidhi mahitaji sambamba na maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika upande wa *TARURA*. Upande wa *TARURA* fedha inayopata katika Mkoa wa Tabora ni ndogo sana. Mkoa wa Tabora ni mkubwa kijiografia, ni mkoa wenye *square metre* karibu 75,000, miundombinu yake ya barabara ni mikubwa sana, lakini fedha inazopata ni ndogo, hazilingani na mahitaji ya mkoa wenyewe. Naomba TAMISEMI iangalie kutuungezea fedha katika upande wa *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ujenzi mkubwa sana wa madaraja. Kwa mfano Mkoa wa Tabora kuunganisha na Shinyanga. Kila sehemu kuna madaraja, kuna Mto mkubwa wa Manonga. Kwa hiyo, ili uweze kuvuka upande wa pili inabidi kuwe na daraja. Kwa hiyo, mahitaji ya madaraja ni mengi sana katika maeneo yetu, lakini fedha tunazoletewa ni ndogo, haziwezi kukidhi mahitaji ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba TAMISEMI ituongeze fedha upande wa *TARURA* tuweze kujenga daraja la Mto Manonga upande wa Mondo ili kurahisisha wananchi wetu kuweza kwenda Shinyanga kwa urahisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia suala la utawala bora, kuna watumishi wengi sana wamekaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga wanakaimu miaka mitatu, miaka minne, wakati tuna uwezo wa kuwapitishia hizo nafasi wakaweza kuzimiliki, wanalipwa fedha za kukaimu muda mrefu. Ni hasara kwa Serikali na Taifa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Gulamali.
Thank you. (Makofi)

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Akbar halafu Mheshimiwa Balozi Rajabu na Mheshimiwa Daniel Mtuka wajiandae.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara hizi ambazo ni nyeti ambayo ni TAMISEMI pamoja na utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa mchango wangu, katika Wizara hizi nyeti, nami niungane na Wabunge wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais jinsi anavyoweza kugawa maendeleo ya nchi hii bila kujali Wapinzani au ni Chama Tawala. Kwa kweli, namsifu sana Mheshimiwa Rais na ni kweli, tunaona juhudi zake jinsi anavyofanya kazi kwelikweli. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza hawa watendaji Mawaziri ambao wapo katika Wizara zote hizi kwa maana ya TAMISEMI, lakini pamoja na Utawala Bora. Kwa kweli, wanafanya kazi pamoja na wasaidizi wao; nawapongeza ndugu yangu Mheshimiwa Jafo na kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika. Kwa hiyo, moto mdundo waendeleo kufanya kazi kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nichukue nafasi hii naomba kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya TAMISEMI. Namwomba Mheshimiwa Jafo, kwa kuwa tulikuwa wote kwenye ziara, nami nitoe mchango kwenye upande wa barabara. Kwa kweli, Halmashauri ya Wilaya ya Newala ina barabara ambazo ni nyingi sana, lakini ndiyo ambayo inalima karibu nusu ya korosho za Newala. Ila

kutokana na mtandao, magari makubwa ambayo yanapita katika barabara zile, nimwambie Mheshimiwa Waziri Jafo, kwa kweli, zile barabara ni mbovu nasi Wilaya ya Newala, *TARURA* haina gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Jafo tupate angalao gari moja kama walivyopata Halmashauri za wilaya nyingine. Maana yule bwana anashindwa kufanya kazi na kwa hiyo, tutashindwa kusomba korosho katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuomba kwamba, nasi tunahitaji gari moja kwa ajili ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, zile fedha ambazo zinagawanywa za *TARURA* sisi tumepata shilingi bilioni 900. Kwa kweli hizi fedha ni ndogo sana, sijui ni kigezo gani ambacho kinatumika, lakini zile barabara zote zilizopo pale wilayani ni mbovu na magari ambayo yanatumika kusomba zile korosho ni mabovu. Kwa hiyo, vinginvyo zile barabara zikiwa mbovu tutashindwa kwenda mbele kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Jafo tuangalie kwamba kama zile barabara zitashindwa au kuongeza zile fedha, basi aangalie uwezekano yale maeneo korofi ambapo kuna milima, kwamba korosho zikishapakiwa magari yanashindwa kupanda, basi afanye utaratibu wa kuangalia kwamba, basi anaweka japo kilometa moja moja au mbili mbili za lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mlima Miyuyu kwenda Ndanda; ule mlima kwa kweli ni mlima mkubwa na tulishamwandikia Mheshimiwa Waziri kuangalia uwezekano wa kuweza kupata angalau kilometa mbili za lami kutoka Miyuyu hadi kufikia Ndanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, barabara ya Mpalu hadi Mnyambe, wale watu wanalima sana korosho, lakini kutoka pale Mpalu kuna mlima ambao ni mkali sana. Magari yakienda pale yanashindwa kusomba korosho, Kwa kweli, hatuwezi kujenga barabara yote, lakini ile kilometa moja

ambayo magari makubwa yanakwama tunaomba Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Kandege Ndugu yangu waangalie uwezekano wa kuweka pale japo kilometa moja ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, pale inapoanzia chanzo cha maji Mitema pale Kitangali ambapo inakwenda barabara hadi kufika Mto Ngwele, ule mlima ni mkali sana, tunaomba vilevile japo kilometa ya lami. Ikumbukwe kwamba uchumi wote wa korosho unaotoka Newala kwa kiasi kikubwa unatoka Kitangali. Kwa hiyo, tungeomba kwamba kilometa nne au tano, itaufanya uchumi huu ukue sana na wa kitaifa maana yake tutakuwa tunapata mapato makubwa sana ya kitaifa. Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waziri Jafo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, nashukuru kwamba tumepata milioni 200 kwa ajili ya Kituo cha Afya Mkvedu. Kuna kituo cha afya kipo Chihangu, kile Kituo cha Afya Chihangu ni cha muda mrefu sana, kipo tangu mwaka 1969 na operesheni ndogo ndogo zinakwenda pale, lakini kwa kweli hatuna jengo la mama na mtoto.

Kwa hiyo, niwaombe sana Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Kandege wapeleke wataalam wakaangalie Kituo cha Afya Chihangu kwa sababu wale akinamama wanajifungulia jikoni na kulala wanalala nje, kwa hiyo inakuwa ni ngumu sana wakati wa mvua wale akinamama kuwa na sehemu ya kujistiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile zile nyumba za watumishi zote karibu zime-*collapse* tangu mwaka 1969 ambapo kituo cha afya kile kilikuwa kimejengwa mpaka leo kile kituo ni kibovu sana. Kama hiyo haitoshi, kile kituo cha afya kipo wazi kabisa, hakina fensi, maana yake hata kama wale watu ambao wanafanya utunzaji wa vile vifaa/rasilimali kwa mfano ile *OPD* ambayo ilikuwa imejengwa na Wajapan leo ulinzi wake unakuwa ni mgumu. Kwa hiyo, niwaombe sanawaende wakakague ili tuweze kufanya matengenezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; niungane na Waheshimiwa Madiwani wenzangu; kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Newala Vijijini ile ni kama Halmashauri mpya, haina mapato mengine. Baada ya kuwa hizi korosho zimeingia kwenye mtandao maana yake haina mapato, wale Madiwani wanakopwa mpaka vikao maana yake sasa hivi mpaka sasa wanadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Jafo tuangalie namna gani, kama ambavyo tumezungumza kwenye ziara ya Rais, namna gani hizi Halmashauri za Wilaya ambazo zinategemea kilimo hasa korosho na ushuru tulikuwa hatujapata, tutafanyaje ili kuwanusuru Madiwani hawa ambao wanadai malipo yao. Kwa hiyo, tuangalie namna nzuri ambayo tunaweza tukawasaidia kwa kuwalipa posho hawa Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala, tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Halmashauri ya Wilaya ya Newala ni pana sana kwa maana kwamba ina Kata karibu 22 ambayo ina mtawanyiko wa wakulima wa korosho. Je, ni namna gani tutawasaidia japo pikipiki kama itakuwa imeshindikana kuwapa mikopo ya magari, basi tuweze kuwanunulia japo pikipiki kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyotoa mchango kwamba tuangalie uwezekano wa hawa Waheshimiwa Madiwani ni namna gani tunaweza tukawawezesha kwa sababu wanatusaidia sana wakati wa kusimamia uchaguzi kwa maana ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hawa Madiwani wanasafiri zaidi ya siku mbili kutoka Vijijini hadi kufika ilipo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waziri waangalie namna nzuri ambazo tunaweza tukawawezesha Waheshimiwa Madiwani hawa na waangalie vilevile ni namna gani wanaweza wakawalipa posho kwa vile vikao ambavyo wameweza kuwakopa kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtuka.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia kwenye Wizara hizi mbili ambazo ni muhimu sana; Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawasifu sana Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Namsifu sana Mheshimiwa Mkuchika na Naibu wake Mheshimiwa Mary kwa kweli tangu amehamishiwa kwenye wizara hiyo, wizara imetulia. Pia ningependa kuvisifu vyombo vya ulinzi na usalama kwa sababu kazi ambazo wanazifanya sasa hivi za usalama sio siri kwamba uko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongezakwa dhati kabisa kazi zinazofanywa na Mheshimiwa Rais na napongeza kabisa kazi ambazo wanafanya Mawaziri wa TAMISEMI hasa Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Mwita Waitara. Kwa kweli kazi ni nzuri na kwa kweli wanastahili sifa kubwa sana. Wamezunguka sana kwenye hii nchi na wamezunguka sana hasa kwenye Wilaya yetu; nakumbuka Mawaziri wote hao ninaowataja wamefika Muheza na wameona kazi za Muheza ambazo wanazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muheza tumefaidika sana kwa sababu tumepewa kwanza bilioni 1.5 kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya na kwenye mpango wa mwaka huu pia tumeongezewa milioni 500 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Pia tulipewa karibu milioni 400 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mkuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunajenga vituo vya afya kwenye kila Tarafa; kwenye Tarafa ya Amani, Misarai tunajenga kituo cha afya, Tarafa ya Bwembera tunajenga

Potwe na Mhamba na kwenye Tarafa ya Ngomeni tunajenga Umba. Nakumbuka nilikuja ofisini na Mheshimiwa Waziri aliniahidi katika vituo vyote hivyo atajitahidi kadiri anavyoweza kuhakikisha kwamba kituo kimoja ananipa milioni 400 kwa ajili ya jiografia ya Jimbo lenyewe kwa sababu ya ukubwa wa Jimbo lile. Hata hivyo, nimeangalia kwenye kitabu bahati mbaya sijaona kituo chochote ambacho kimepangiwa wakati huu, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kufikiria kutokana na ukubwa wa Jimbo la Muheza ambalo ni kubwa sana lenye kata karibu 37 na vijiji karibu 135.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maboma na madarasa, tunashukuru sana Muheza tumepata milioni 225 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya shule za sekondari na tumeweza kuanza kazi hiyo karibu kwenye sekondari tisa. Kazi hiyo inaendelea vizuri, isipokuwa tunalo tatizo kubwa sana ambalo ni la maabara, tuna maabara karibu shule zote za sekondari, karibu sekondari 21. Haya ni maboma ya maabara ambayo tulitegemea kabisa Serikali itusaidie kukamilisha maabara haya, hii imeleteleza tatizo linafanya hasa wanafunzi wa sekondari katika Wilaya ya Muheza kutokusoma sana masomo ya sayansi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana na tunaomba sana kwa msisitizo mkubwa kwamba tuletewe fedha nyingine za maboma ya maabara ili tuweze kumaliza hili tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la upungufu wa watumishi pamoja na Walimu; suala hili ni kubwa sana na nitamwandikia barua Mheshimiwa Waziri kumpa takwimu sahihi ambazo zinaonesha upungufu ulivyo mkubwa hasa kwenye masomo ya sayansi na hisabati. Tuna upungufu mkubwa na upungufu hasa wa Wauguzi pia na Madaktari kwenye zahanati na hiki kituo chetu cha afya ambacho tunategemea kukifungua karibuni. Kwa hiyo, tunategemea kwamba upungufu huu utaweza kukamilika na kuweza kusaidiwa kuweza kupata Walimu hasa wa sayansi na hisabati kwenye sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa pia kwenye shule za msingi. Shule nyingi za msingi zina Walimu kuanzia wawili, watatu, wanne; huwezi kutegemea Walimu wachache na shule ziweze kufanya vizuri. Matokeo yetu ya mitihani ya shule za sekondari na msingi sio mazuri kutokana na kuwa na Walimu wachache. Kwa hiyo, nashukuru kwamba tuweze kuangaliwa na kupewa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo wenzangu wameliongelea la Madiwani, Madiwani tunawategemea sana kwenye hii miradi ambayo inaendelea sasa hivi. Wanafanya kazi kubwa sana Madiwani kwa sababu hasa *Force Account* kwenye vituo vya afya na madarasa wanajituma sana na wanakuwa ni wahamasishaji wakubwa sana kwa wananchi wetu, ni vizuri suala lao la posho likaangaliwa ili waweze kuongezewa posho waweze kupata posho ambazo ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TARURA*, wenzangu wameoliongelea kwa wingi sana lakini fedha ambazo wanapewa *TARURA* kutokana na kazi yao kubwa ni ndogo sana. Ni afadhali sasa hivi badala ya ile 70kwa30 basi ikaongezeka kidogo. Sisi kwenye Kamati ya Baajeti tunajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba kwa kweli pendekezo hili linaweza kuchukuliwa kwa sababu *TARURA* kazi wanazofanya ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miradi ya mikakati; miradi ya mikakati sisi Muheza tunategemea kujenga stendi ya kisasa na tumeleta maombi yetu yote na tunaamini yametelekezwa kwa ukamilifu kabisa, lakini tumeangalia pia hapa sikuona Muheza ikipewa chochote. Nilikuwa nafikiria Waheshimiwa Mawaziri wajaribu kwa kadiri ya uwezo waowaangalie kwamba wanaweza kutusaidia vipi, tunaamini kabisa kwamba tutakapopata fedha hizo za kujenga stendi mpya pale Muheza, basi tutaweza kujikimu na kuweza kujishughulikia na mambo yote ambayo tunayaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga hoja mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Daniel Mtuka.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa zawadi ya uhai tumekutana tena safari hii, hii ni bajeti ya nne; tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya, kiongozi mahiri, wa kiwango na wa wakati huu. Nipongeze wizara hizi mbili hasa zikiongozwa na Mawaziri mahiri; Mheshimiwa Kapt. (MST) George Mkuchika pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Jafo kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na Naibu Mawaziri wao, Makatibu Wakuu, Naibu Katibu Wakuu na timu nzima katika idara zao katika wizara hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane na Mheshimiwa Mbatia leo ni tarehe 12 ni siku ambayo tulimpoteza kiongozi mahiri kabisa, Waziri Mkuu wa zamani Moringe Sokoine. Wote tunaungana na Watanzania wenzetu katika kukumbuka siku hii muhimu ambayo tulimpoteza shujaa wetu, aliweka alama katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu, niseme tu kwamba kwa kuanzia Wizara ya TAMISEMI wanayo kazi kubwa kuwa na trilioni 6.2, asilimia 18 ya bajeti nzima; hili ni fungu kubwa sana. Mnayo kazi kubwa ya kufanya lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais, timu ambayo ameiweka nina uhakika wanafanya kazi vizuri na fungu hili najua litapita. Niwaombe Wabunge wenzangu tuwapitishie bajeti hii iliwaende wakafanye kazi. Naiona timu ni nzuri imehamasika watafanya kazi kama ambavyo inatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe timu hii ya Wizara na sisi tunawaunga, washughulikie jambo la udhibiti wa ubora hasa majengo na barabara, watusaidie sana. Mheshimiwa Katibu Mkuu yeye ni *engineer* Ndugu Nyamhanga namfahamu, adhibiti sana ubora wa majengo pamoja na barabara. Hizi *BOQ* fedha hizi ni nyingi, ndipo tunapopigiwa hapa kwenye utaalim; mimi nipo *very much concerned* hapa kwenye *BOQ*. Wahandisi wa Wilaya kwenye Halmashauri zetu na Wakurugenzi wasimamie jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie na mimi kama wenzangu ambavyo wamesema natoa shukrani zangu nyingi/kubwa, wametutendea haki sisi Jimbo la Manyoni Mashariki kama Wizara, kabisa. Nimepokea Jimbo hili likiwa limechoka sana katika miundombinu ya elimu na afya lakini hivi ninavyozungumza auheni ni kubwa sana. Tumepokea milioni 900 katika vituo viwili vya afya, bilioni moja katika kuboresha huduma ya maji pale Manyoni Mjini, bilioni 2.2 katika mradi wa vijiji 10 wa maji, milioni zaidi ya 600 katika mradi wa ujenzi wa madarasa hizi fedha za *EP4R* pamoja na *EQUIP* na mambo mengi ambayo siwezi kuyataja. Kwa kweli sasa Manyoni naona inakwenda kinyume na zamani ambavyo niliikuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo tatizo dogo lakini ni kubwa la usimamizi wa fedha hizi, zinakuja nyingi lakini usimamizi bado mimi nauona haupo vizuri. Wanisaidie alizungumza Mheshimiwa Nkamia jana, lakini mwingine amezungumza leo suala la kozi ya viongozi ni muhimu sana na ni msingi kabisa, tunavurugana sana kule. Mbunge anasema hivi na Mkurugenzi anasema hivi badala ya kwenda kwa sauti moja kusimamia mambo haya na fedha hizi za Watanzania tunabaki kuvurugana na fedha na muda vinapotea. Kozi hizi ni muhimu sana, Manyoni tuna shida kidogo ndio maana hata tunadaiwa benki; Madiwani wanadai posho kwa sababu ya mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Mheshimiwa Jafo na timu yake hebu waitazame Halmashauri ya Wilaya

ya Manyoni watusaidie, ndiyo maana tupo hapa, hatuwezi kukaa kimya wala kulindana tunataka Watanzania wapate huduma sio kuzozana na kufukuzana na kukimbilia kwamba huyu ana cheo hiki au mimi ni mkubwa, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, Mbunge anaweza akaenda kufanya mikutano kule kwa wananchi akapokea malalamiko, yale malalamiko Mbunge yeye kazi yake ni kuyapekela sasa kwa wenzake; la Mkuu wa Wilaya nalipeleka kwa Mkuu wa Wilaya na la Mkurugenzi nalipeleka kwa Mkurugenzi. Sasa nikimpeleka asiseme mimi namtuma kazi, ni katika utaratibu wa mgawanyo wa majukumu, mimi napokea kila kitu. Lazima hawa watusaidie sisi, ndio wenye vyombo na watekelezaji, sisi ni wasimamizi; kozi hizi ni muhimu jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa ikama pia tuna shida, upungufu wa watumishi idara ya afya na idara ya elimu kwa kweli bado hali ni ngumu sana, watendaji ni wachache sana, watusaidie sana kwenye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* fedha hii haitoshi, vijana wale wana moyo pamoja na kiongozi wao, wana moyo sana. Mimi wamenifungulia vibarabara vitatu pale wananchi wamefurahi sana, tumewaunganisha na vijana wana moyo wa kufanya kazi, lakini hawana fedha. Naungana na mimi na wenzangu waliotangulia angalau ile *share* ya 70/30 iwe 60/40. Najua *TANROAD* wana barabara chache lakini zina gharama kubwa sawa lakini ile *share* ikiwa 40/60 angalau tutapata fedha kule, ndio kwa wananchi kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kidogo kuhusu TAKUKURU, wawaongezee fedha, wawape nguvu, wanalinda heshima ya nchi hii. Hawa ndio ma-*watchdog* tunavyowaita. TAKUKURU bado ni chombo chenye heshima kubwa na nguvu, kama kuna watu wana matatizo wanashughulikiwa, lakini chombo chenyewe kama *institution* kinabaki bado kina nguvu, wawape hela wakafanye kazi. Naona vijana wale wana mori wa kazi, lakini hawana mafuta hata ya kufanyia

kazi, hawana magari na ofisi bado ni chache kwenye Wilaya kule hebu tuwape nguvu walete heshima katika nchi hii. Mheshimiwa Rais tumsaidie analia sana, bado rushwa ipo, ndugu zangu naomba wanisikilizekwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niseme tu kwamba naunga mkono hoja ya bajeti hizi mbilikwaasilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mtuka, hao ndio wachangiaji wetu kwa mchana huu. Tuna matangazo mawili; tangazo la kwanza linatoka Wizara ya Kilimo, mnakumbushwa Waheshimiwa Wabunge mnaotoka kwenye Wilaya zinazolima pamba ikiwemo Wilaya ya Bariadi, kikao cha saa nane mchana wa leo, wizarani pale mkabala na VETA, saa nane mchana huu.

Tangazo la pili ni marudio lile nililofanya asubuhi, siku ya Jumapili tarehe 14 Aprili, saa tano asubuhi kutakuwa na semina kwa Wabunge wote katika Ukumbi wa Msekwa kuhusu masuala ya ualbino. Semina hiyo itatolewa na Shirika la *Under The Same Sun* ambalo linaleta haki na ustawi wa watu wenye ulemavu hapa nchini na maeneo mengine duniani. Aidha, ujumbe wa shirika hilo upo hapa Bungeni walitambulishwa asubuhi wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Bwana BerthasiaLadslaus. Hayo ndiyo matangazo

Mwisho, tutakaoanza nao mchana huu niMheshimiwa Kiza Mayeye, Mheshimiwa Joseph Haule (Profesa Jay) na Mheshimiwa Vedastus Ngombale na wengine watafuata kwa mtiririko wa vyama vyetu humu Bungeni.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja Jioni leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lllisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Kabla hatujaendelea na wachangiaji niliowataja mchana, nina orodha ya wageni wengine ambao wapo Bungeni. Tunao wageni 127 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Mbunge, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambao ni Washereheshaji (MCs) kutoka mikoa yote Tanzania wakiongozwa na Ndugu Obeid Sarungi. Karibuni sana MCs. (Makofi)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge, ambao ni Madaktari na Wauguzi wa Hospitali ya Wagala iliyopo Mvomero, Mkoani Morogoro ambao ni Ndugu Eva Kisimbo, Ndugu Irene Kuhanga, Ndugu Mathias Sui na Mdugu Slam Mganga. Karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na uchangiaji na tunaanza na Mheshimiwa Mayeye, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Haule na Mheshimiwa Vedasto Ngombale ajiandae.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya TAMISEMI na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya nimeweza kusimama jioni hii ya leo. Kwa kipekee kabisa nimpongeze *Fulbright* Prof. Ibrahim Haruna Lipumba kwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba hizi za Wizara hizi mbili, natambua Serikali inapambana kuhakikisha inaleta huduma bora kwa wananchi. Kwanza nianze na suala la *TARURA*. Barabara za vijijini ni muhimu sana katika maeneo yetu. Wote tunafahamu kwamba wakulima wote wako vijijini lakini barabara hizi ndizo ambazo zinaweza kuwasaidia kutoa mazao mashambani na kuleta mijini kutafuta masoko lakini hali ya barabara hizi kiukweli ni changamoto kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa ambayo *TARURA* wanaifanya, moja ya changamoto ambayo inawakabili ni suala zima la bajeti. Niiombe Serikali katika bajeti hii tunayokwenda nayo tuweze kuwasaidia *TARURA* wapate bajeti ya kutosha ili waweze kufanya kazi yao na kumaliza miradi hii ya barabara zetu huko vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la bajeti tumeona *TARURA* wanapata asilimia 30 na *TANROADS* wanapata asilimia 70. Naelewa Serikali mmeunda Kamati Maalum kwa ajili ya suala hili na mimi nichangie na kuiomba Serikali kwamba *at least* sasa *TARURA* wabaki na 40 na *TANROADS* wapewe 60 kwa sababu ya barabara za viwango vya lami na madaraja kama ya Mfugale. Kwa hiyo, tuwasaidie watu wa *TARURA*, naamini wanafanya kazi na kama watapata bajeti ambayo inatosha wataweza kutusaidia barabara zetu hizi kumalizika kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye *TARURA* changamoto nyingine ni vitendeakazi, watu hawa hawana magari ya kuweza kutoka sehemu moja na kwenda *site*. Mfano Mkoa wangu wa Kigoma takribani wilaya zote, kuanzia Kigoma *DC*, Buhigwe, Kasulu, watu wa *TARURA* hawana magari na imekuwa ni usumbufu mkubwa katika utendaji wao wa kazi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri muangalie ni jinsi gani Kigoma wilaya zote tunaweza tukapata magari kwa watu hawa wa *TARURA* ili wafanye kazi kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika suala la afya. Natambua Serikali mnajituma na mnafanya kazi kuhakikisha mnaboresha vituo vya afya na kutuletea wauguzi. Niwashukuru kwamba Kigoma mwaka jana tuliomba, mmetuletea Kigoma nzima watumishi 402 lakini kiukweli bado changamoto ni kubwa. Maeneo mengi ukienda hospitali za Kigoma na hata maeneo mengine ya Tanzania bado hatuna wauguzi wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kufikia Novemba, 2018 Kigoma tulikuwa na wafanyakazi 2,004, kiukweli bado

idadi ya wafanyakazi ni ndogo ukizingatia Kigoma tuko zaidi ya watu milioni mbili lakini ni mkoa ambao tuko mpakani tunahudumia mpaka wakimbizi kutoka Kongo na Burundi. Kwa hiyo, niombe sana Serikali, pamoja na jitihada ambazo mnafanya lakini mtuangalie kwa jicho la pili mtuongezee wauguzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo katika afya, Kigoma tuna Hospitali hii ya Mkoa ambayo inaitwa Maweni. Mpaka sasa hatuna vifaa kama *CT Scan* na *x-ray machines* za kutosha hali inayosababisha usumbufu mkubwa sana kwa wananchi watu wanakwenda kutibiwa pale wanahitaji huduma hii ya *CT Scan* wanapewa rufaa kwenda Mwanza (Bugando) au kwenda Muhimbili. Kulingana na hali ya maisha ilivyo, siyo watu wote wataweza kwenda Muhimbili au Bugando kwa wakati. Sasa kama tunataka kuwasaidia wananchi ili tupunguze vifo, niombe sana Serikali muweze kutusaidia vifaa hivi vya *CT Scan*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niko katika hospitali ya mkoa; hospitali hii kama nilivyosema inahudumia watu wengi sana lakini mpaka sasa hatuna ma-*specialist* wa kutosha, tuna *specialist* mmoja wa akina mama na mmoja wa watoto. Kuna magonjwa mengine kama haya ya kisukari hatuna ma-*specialist*. Niombe sana Serikali mtusaidie hospitali hii tuweze kupata ma-*specialist* wa kutosha, mtakuwa mmetusaidia watu wa Kigoma na maeneo mengine Tanzania ambayo hakuna ma-*specialist* katika hospitali zao muweze kuwasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie tena suala la miundombinu hospitalini na kwenye shule zetu. Sote tunajua kwamba walimu, madaktari na wauguzi ni watu muhimu sana katika maisha yetu, lakini watu hawa wamekuwa wakiishi maisha magumu kwa maana ya kwamba hata nyumba bora za kukaa hawana. Niombe sana Wizara muweze kuangalia suala hilo, muwajengee nyumba wauguzi na walimu ili nao waweze kukaa katika mazingira bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la moboma, kuna majengo ambayo wananchi wamejitoa, niseme tu kwamba wananchi wanaunga mkono Serikali kwa kufanya vitu mbalimbali kama ujenzi wa zahanati, kujenga shule na *hostels* za wanafunzi lakini inafika muda na wao wanakwama. Niombe sana Serikali muwasaidie wananchi muweze kumaliza majengo haya ambayo yameishia kwenye lenta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano tu katika Mkoa wangu wa Kigoma, Awamu ya Nne Rais aliyepita aliahidi kujenga hospitali katika eneo la Nyarubanda na Mahembe na wananchi waliitikia wakaanza kujenga lakini sasa imesimama na hakuna mwendelezo wowote. Niombe sana Serikali muwasaidie watu hawa waweze kumaliza majengo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la vitambulisho. Niseme tu kwamba mimi ni mdau wa maendeleo na naunga mkono jitihada za Serikali katika ukusanyaji wa kodi lakini tuwe wakweli; pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais alisema hawa wajasiriamali wadogo wakate vitambulisho lakini tuwaangalie hawa wajasiriamali wadogo ni wa aina gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Mkoa wangu wa Kigoma, mimi natokea Kijiji cha Mwandiga, baada ya Bunge kuisha kuna akina mama nilikwenda kuwatembelea sokoni. Kuna mama ambaye anauza ndizi kwa sababu tu nyumbani kwake amepanda ndizi, anaona ndizi zimeiva anasema nipeleke sokoni nikapange chini ili wanangu waweze kupata daftari na kupata mafuta ya taa. Sasa hawa ambao wanakwenda kutoa vitambulisho hivi unakwenda kumtoa mama kama huyu Sh.20,000 anaitoa wapi wakati biashara anayofanya haikutani mzunguko wake kupata Sh.20,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kiukweli malalamiko ni mengi. Kama tunasema ni Serikali ya wanyonge, wanyonge ndiyo hawa akina mama na vijana...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Haule (Profesa Jay).

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nijielekeze kusoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13(1) inasema: “Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria”. Vilevile Ibara ya 14, inasema: “Kila mtu anayo Haki ya Kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye Wizara ya Utawala Bora. Wiki iliyopita nilisimama katika Bunge lako Tukufu nikizungumzia kwamba kuna upotevu wa watu kumi katika Jimbo la Mikumi maeneo ya Ruhembe, Kidodi pamoja na Ruaha na niliongea hapa kwenye Bunge nikiamini kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imo humu ndani. Pamoja na kuongea hapa Bungeni na kumfuata Waziri wa Maliasili na Utalii na kuwafuata wahusika wote mpaka leo watu wamenyamaza kimya kana kwamba hakuna kilichotokea katika Hifadhi za Mikumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimekuwa nikijjuliza, Serikali hii inajipambanua kwamba inajali utu, haki lakini pia utawala bora, pamoja na hayo kila siku tunaimba kwamba Tanzania ina amani lakini ni jambo la kushangaza sana unapooni kwamba kuna watu kumi na tunaripoti kwenye Serikali wamepotea katika mazingira ya kutatanisha tangu tarehe 2 Aprili, leo ni tarehe 12, siku kumi hakuna mtu yeyote

amezungumzia lolote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imetusikitisha sana na bado majonzi yamekuwa makubwa sana katika Jimbo la Mikumi maeneo Ruhembe na niseme kitu kimoja kwamba hali hii inaendelea kuleta taharuki na imani ya wananchi kwa Serikali imekuwa ndogo na inazidi kushuka kila siku. Kwa kuwa tunajua kwamba TANAPA na Polisi wana helikopta au helikopta hizo zinakuwa kwa ajili ya intelijensia kuwakamata wapinzani tu na kushindwa kuelewa Watanzania wengine wasiokuwa na hatia wanaopotea katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku kumi ni nyingi watu wanapokuwa hawaonekani. Tukasema labda tupeleke kwa Serikali itatafuta namna ya kutupa majibu ya jambo kama hilo, inasikitisha sana kuona mpaka leo siku ya kumi watu wamekuwa na majonzi. Basi hatuombe labda wamekufa tuseme lakini hatuombe hivyo, kama wamekufa basi mtupe hata nguo zao ili tukazizike au tukaendelee na misiba katika Jimbo la Mikumi, labda huo ndiyo utawala bora mnaoujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana imeundwa Kamati imekwenda kule, RCO pamoja na watu wa hifadhi, *you can't be a judge of your own case*, huwezi kuwapeleka watu ambao tunahisi na wananchi wanalia kwamba watu wamepotea katika hifadhi yao, halafu bado wao wao ndiyo wakaenda kuangalia na kufanya uchunguzi mpaka leo hakuna majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo tunaomba mliangalie kwa kina na tupate majibu ya Serikali hawa watu kama wamekufa tujue, kama wamepotea tujue, tunatakiwa tujue ripoti yao. Nina nia ya kuomba Bunge lako Tukufu liunde Tume ambayo itakwenda kufanya uchunguzi katika maeneo hayo ya Ruhembe ili tuweze kuwapa haki hawa wananchi ambao ndugu zao wamepotea katika hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu Tume ya Uchaguzi. Kila siku tumekuwa tukizungumza Tanzania ni kisiwa cha amani lakini naona watu wana nia ya kupoteza kisiwa cha amani cha Tanzania. Labda niwashauri tu Wabunge wa CCM ambao mnashabikia sana kuhusu hii Tume ya Uchaguzi, muangalie sasa hivi katika TV za kimataifa, CNN, Al-Jazeera na sehemu nyingine, jinsi ambavyo kumekuwa na *unrest* katika dunia kwa sababu ya mambo kama haya. Watu wamefungwa mikono, watu wanashindwa kusema lakini Tume imekuwa haitendi haki kwa wapinzani wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Sudan mmeona kimentokea nini Al-Bashir lakini ukiangalia Algeria na Venezuela kuna vitu kama hivyo na hapa Tanzania kama tutaendelea kucheka na hii Tume ya Uchaguzi ambayo sasa matokeo yamekuwa yakitangazwa *vice versa*, leo tu Mahakama ya Mbeya imetoa hukumu kwamba katika Kata ya Ndalambo ambapo alitangazwa mgombea wa CCM lakini wameona ni jinsi gani ambavyo Serikali ya CCM imekuwa ikiiba kura kila siku na sasa hivi wameonekana wameiba na mgombea wa CHADEMA ametangazwa kushinda pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wanasema Tume hii ni huru kwa sababu akina Profesa Jay walitangazwa; hamjui mbilinge tulizozifanya huko mpaka tukatangazwa. Tumefanya uchaguzi tarehe 25, tarehe 26 unaona magari yanakuja yanaondoka, tarehe 27 CCM wanabeba magari ya matangazo wanataka kujitangaza kwa nguvu, nyomi linaongezeka pale na pale kweli asingetoka mtu. Napenda kusema kwa Wanamikumi kwamba nitaendelea kusimama pamoja nanyi na niombe watu wote wapenda amani hapa Tanzania wasimame pamoja kuhakikisha kwamba Tume hii inabadilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwanamuziki wa *hip hop* lakini pia napiga ngumi mbili, tatu, napenda *boxing*; kama wewe ni *referee* kama Tume ya Uchaguzi, basi usinifunge mikono mimi halafu ukamuacha jamaa anipige

mangumi mengi mengi usoni, unanifunga kamba halafu unamwambia jamaa apige, haiwezekani. Ipo siku hizi kamba zitakatika na nitawapiga manondo ya kutosha ndugu zangu kwa sababu tunakwenda kushinda na tunaamini tutakwenda kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe tu watu wote ambao wamepitia katika nyanja na matatizo mbalimbali waamini kwamba haya mambo ni ya kupita tu. Watu wangu wa upinzani tulizeni *ball*, mwaka huu ni wa uchaguzi tunakwenda oya oya na mzuka kama kawaida maeneo ya katikati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niende kwenye Wizara ya TAMISEMI kwa Mheshimiwa Jafo. Nashukuru sana ulifanya ziara Jimboni Mikumi lakini kiukweli kabisa ni kwamba katika Kituo cha Afya cha Mikumi baada ya ziara yako ndiyo mambo kidogo yameanza kwenda vizuri na mimi kama Mbunge nimechangia mifuko 200 kuonesha kwamba nina-*support* kile kinachotokea kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mikumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya ni kwamba wale wafanyakazi waliopewa kazi za ziada bado hawajalipwa mpaka leo na wameniagiza nikwambie kwamba wameshaleta barua kwako wanasubiri uwasaidie. Wale ni walalahoi wa Mikumi wamefanya kazi pale wanataka uwasaidie wapate haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wananchi wa Malolo wanajenga Kituo cha Afya kwa nguvu zao wenyewe na mimi kama Mbunge nimepeleka tena mifuko 200 ku-*support* juhudi hizo. Tunaomba Serikai nayo ituongezee hela kidogo ili tuweze kukamilisha nia yao ya kuweza kuwa na kituo chao cha afya kama ambavyo sera inasema kila kata iwe na kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Ulaya, nilishaongea muda mrefu kimechakaa, tunaomba Serikali ipeleke pesa kule. Pia Waziri wa Nishati alishafanya ziara pale,

aliona kwamba hakuna umeme na alisema atatuletea umeme, watu wanasubiri maeneo ya Mikumi, Ulaya pale tuweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwamba tuliomba magari, kwa sababu Mikumi pale kuna ajali nyingi sana Mitaa ya Msimba, Ng'apa mpaka Ruaha Mbuyuni lakini sasa hivi kinajengwa pale kituo cha dharura kwa ajili ya ajali na kwamba tutaletewa magari mawili kama ambavyo Mbunge niliomba. Kwa sababu tumegundua kwamba pale Mikumi kuna matatizo mengi ya ajali mbugani na sehemu nyingine na tukasema kwamba tukipata magari ya wagonjwa yatasaidia kukimbiza wale watu wanaopewa rufaa. Maana kutoka Mikumi mpaka Kilosa ni kilometa 78; Mikumi mpaka Morogoro kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ni kilometa 120; Mikumi mpaka Iringa ni zaidi ya kilometa 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani kwamba tumeambiwa haya magari yapo, Wanamikumi wanayasubiri kwa nguvu na kwa hamu kubwa ili tuweze kuwasaidia Watanzania. Maana Mikumi pale inapita barabara kubwa inayotoka Tanzania kwenda Zambia mpaka South Africa, tunaamini hata watu wa Nyanda za Juu wanaopata ajali maeneo yale watapata nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *TARURA*. Kwa kweli *TARURA* bajeti yao ni ndogo na ndiyo maana mwaka jana nilipiga kelele hapa nikisema Wilaya ya Kilosa ni kubwa lakini imekuwa na bajeti ndogo sana, *TARURA* hawana hata gari. Nashukuru tumeletewa gari lakini bado *TARURA* uwezo wake ni mdogo. Kuna barabara kutoka Ruaha Mbuyuni - Malolo - Kibakwe; kuna barabara ya kutoka Dumila - Kilosa - Mikumi lakini pia kuna barabara nyingine ya kutoka Ulaya - Madizini - Malolo, hizo zote ziko chini ya *TARURA*, tunaamini inaweza kutusaidia. Hii barabara ya Dumila - Kilosa iko chini ya *TANROADS*, naamini nao watatusikia waweze kutusaidia kwa sababu ni barabara muhimu sana kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuongelea kuhusu upungufu wa watumishi na kwa Wizara ya Elimu katika Wilaya

yetu ya Kilosa tumekuwa na upungufu mkubwa sana wa walimu. Mfano shule ya msingi ina wanafunzi wa awali wa darasa la kwanza hadi la saba 107,000 lakini walimu wako 2,393 tu na tuna upungufu wa walimu 929. Pia tuna maboma 39 tunaomba Serikali itusaidie; sekondari tuna madarasa pungufu 129, majengo ya utawala 28, nyumba za walimu 689 lakini pia tuna upungufu wa *hostels* 27. Wananchi wamefanya juhudi kubwa sana ya kujenga maboma tunaamini Serikali itatusaidia ili tuweze kuboresha elimu katika Wilaya yetu ya Kilosa ambayo ni wilaya kongwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme kwamba tuko pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani na nimheshimu sana Mheshimiwa Japhary Michael ambaye amewasilisha hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Haule. Tunaendelea na Mheshimiwa Ngombale.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niseme machache katika Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na TAMISEMI na suala nzima la posho za Wenyeviti wa Vijiji na Vitongozi. Hawa ni viongozi ambao wanachaguliwa kama ambavyo Madiwani, Wabunge na Rais wanavyochaguliwa, lakini hatujaweka utaratibu wa kuangalia haki zao na hasa kuhakikisha kwamba wanapata posho. Napendekeza kwamba kama Serikali Kuu haina uwezo wa kuwawezesha viongozi hawa kupata posho, basi itoe maelekezo maalum katika makusanyo ya ndani ya vijiji husika, viongozi hawa walipwe kutokana makusanyo hayo. Hiyo itawasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la vitambulisho vya wajasiliamali, zoezi ili limeanza ghafla ghafla na limeleta taharuki kubwa huko kwa wananchi na hasa pale Serikali

inaposhindwa kubainisha ni yupi mjasiliamali ambaye anatakiwa apewe kitambulisho? Kumekuwa na sintofahamu, mama mwenye mafungu matatu ya mboga anatakiwa alipe shilingi 20,000/=, mama huyo huyo akiwa na mikungu mitano ya ndizi, anatakiwa alipe shilingi 20,000/= na sehemu nyingine kama kule kwangu mtu mmoja analazimishwa kulipia hata mara tatu kwa sababu ana biashara tatu tofauti. Hiyo ni sintofahamu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, vitambulisho hivi vinaenda kubana kabisa mapato ya vijiji na mapato ya Halmashauri. Halmashauri hizi zitastawi vipi kama mapato yake kwa namna tofauti tofauti yanaendelea kuchukuliwa na Serikali Kuu? Naiomba Serikali hilo waliangalie, kwa sababu wananchi sasa wananituma, Mheshimiwa Mbunge, hebu tuulizie, hivi ile kodi ya kichwa imerudi? Maanda sasa kila tukizunguka ni vitambulisho, vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipo familia ambayo hahijihusishi na ujasiliamali sasa. Kila familia lazima ifanye ujasiliamali, vinginevyo maisha ni magumu. Sasa kama unafanya ujasiliamali ni shilingi 20,000/=. Maisha kule ni magumu sana, naomba hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusiana na ujenzi wa zahanati kama sera inavyozungumza. Kwa bahati mbaya kabisa, mimi katika Jimbo langu kuna Kata moja aina zahanati hata moja za Serikali. Ile kata inaitwa Kata ya Namayuni. Ile kata ina vijiji sita, kuna kijiji kimoja kinaitwa Kijiji cha Naama, chenyewe wamejitahidi, wamejenga angalau kufikia boma. Naomba Wizara iwasaidie wale wananchi wapate ile zahanati iishe ili basi kata ile nzima iweze kupata huduma kwa sababu wananchi wanatembea kilometa zaidi ya 20 mpaka 50 kufuata huduma za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, bado kuna tatizo la miundombinu iliyokamilika kuendelea kutotumika. Katika Kata ya Mingumbi katika Kijiji cha Lyomanga, Mfuko wa TASAF ulitoa fedha na kujenga zahanati

toka mwaka 2009. Mpaka hivi tunavyozungumza, zahanati ile haijatumika na sasa inaelekea kubomoka. Naiomba Serikali ifuatilie hiyo zahanati na ione namna gani pesa za Serikali zinapotea bila kuwa na sababu ili basi ikiwezekana wafanye marekibisho na wananchi wapate huduma ya matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la korosho. Nachukuwa fursa hii kuipongeza Serikali na hasa ile kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Rais kuhusiana na kwamba itawalipa sasa wakulima wa korosho pamoja na wale kangomba. Nikiri kabisa, sasa angalau tunaishi kwa matumaini, kwa sababu hali mwanzoni ilikuwa ni ngumu sana. Ingawa malipo yenyewe bado hayajafanyika, lakini tunayo imani kwamba siku moja tutalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili niseme, Serikali iache tabia ya kuingilia michakato iliyopangwa kwa mujibu wa sheria. Suala la korosho na utata uliotokeza ni kwa sababu tu Bodi ya Mazao Mchanganyiko haina uzoefu wa kusimamia zao la korosho. Katika namna ambayo hatufahamu, ni kwa namna gani Bodi ya Korosho ambayo inatambulika kwa mujibu wa sheria ikawekwa pembeni na badala yake ikachukuliwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambapo mzigo umewalemea mpaka sasa wanashindwa kufanya malipo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajinasibu kwamba imetoa pesa, lakini bodi ile inashindwa kwa sababu haina uzoefu. Kwa hiyo, naomba hili liangaliwe sana. Kwa sababu maamuzi hayo yamepelekea hasara, athari za kisaikolojia, na kudumaza maendeleo, naitaka Serikali iwaombe radhi wakulima wa korosho kwa kitu kilichotokea. Kwa sababu kuna watu wamepoteza maisha, Serikali iwaombe radhi wakulima wa korosho kwa sababu lile lililofanyika, limefanywa kwa makusudi. Kwa hiyo, naomba hilo lifuatiliwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda niseme ni suala zima la *TARURA*. *TARURA* wanafanya kazi vizuri lakini bajeti yao haitoshi. Wanajitahidi, lakini bajeti yao

haitoshi. Naitaka Serikali iongeze bajeti *TARURA*. Nami katika Jimbo langu, naomba *TARURA* ishughilikie barabara ya kutoka Mbombwe – Anga - Nakindu mpaka Miangalaya; lakini pia ishunguilikie barabara ya kutoka Mkarango - Mitole na kutoka Chumo mpaka Mkoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nikumbushe ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne. Hii nalizungumza kwa mara ya tatu nikiwa humu Bungeni. Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Kikwete akiwa katika Sherehe za Kumbukumbu za Vita ya Maji Maji pale Nandete, aliahidi kwamba atajenga barabara kutoka Nandete mpaka Nyamwagi, ile ahadi mpaka sasa haijafanyiwa chochote. Naitaka Serikali ifuatilie utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ufuta. Jimbo la Kilwa Kaskazini na Kilwa ujumla, sisi ni wakulima wazuri wa ufuta. Mwaka 2018 kulitokea na tatizo kwamba ufuta ambao hauna bodi ulilazimika kusimamiwa na Ofisi ya Mkoa na siyo Halmashauri, matokeo yake yalipelekea mapato ya Halmashauri kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 tulikwenda TAMISEMI, tulifuatilia sana. Tunaomba zao la ufuta lisimamiwe na Halmashauri na siyo Mkoa kwa sababu zao hili halina bodi na Halmashauri ina uwezo wa kufanya hivyo. Kwa kufanya hivyo, kung'ang'ania kusimamiwa na mkoa, mapato ya Halmashauri yanapungua. Tunaomba sana zao hili lisimamiwe na Halmashauri na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie kuhusu upandishwaji wa madaraja. Tunaomba Serikali ijitahidi sasa kuona madaraja na mishahara ya watumishi inapandishwa. Watumishi hawa wanafanya kazi kwa kujitolea, wanafanya kazi kwa nguvu kubwa lakini wanakosa motisha kiasi kwamba ufanisi wa kazi unapungua. Kwa hiyo, Walimu, Watumishi wa Afya wote wale wapandishwe madaraja na mishahara iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie kuhusiana na fedha za Mfuko wa Wanawake Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Hili limezungumzwa sana na Wajumbe wa Kamati yangu, lakini pia nami niongezee. Tumefanya ziara sehemu mbalimbali, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama imefanya vizuri sana na imefanya vizuri katika eneo hilo kwa sababu imefanya maamuzi ya kuchukuwa hizi pesa badala ya kumpa mtu mmoja mmoja ikaandaa utaratibu ambao utaenda kuwasaidia kundi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie ile *model* ya Halmashauri ya Kahama, ikiwezekana ifanyike sehemu nyingine. Kwa sababu sasa mianya imefungwa. Mwanya peke yake ambao kama hatutakuwa makini, Watendaji wa Halmashauri wanaweza kutumia kupiga sana pesa, ni katika pesa hizi za asilimia kumi. Kwa hiyo, tuwe makini sana, hizi pesa ikiwezekana tuzielekeze katika namna ambayo tunaweza kufuatilia na walengwa wakapata mahitaji yao stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukukumbuke pia katika eneo la walemavu bado walemavu wanashindwa kupata yale mahitaji yao kulingana na aina ya ulemavu waliokuwano. Tuangalie uwezekano wa kuwasaidia walemavu wasioona wapate fimbo, walemavu viziwi wapate shimesikio, walemavu wa viongo wapate viungo bandia, wapate baiskeli na wale walemavu albino wapate mafuta kwa ajili ya kujinusuru na adhari za miale ya mwanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijielekeza huko tutakuwa tumewasaidia sana, vinginevyo hii mikopo tunaweza tukaipeleka na isiwe na marejesho. Ni heri tupeleke kwa kuwasaidia Walemavu kwa ulemavu walionao...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Vedasto.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Kiteto Koshuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau, Mheshimiwa Desderius Mipata na Dkt. Christine Ishengoma ajiandae. Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niendeleo kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu. Pia niendeleo kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendeleo kunijalia afya njema ili niweze kutoa michango yangu katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoanza kuchangia katika Wizara hii ya TAMISEMI na Utawala Bora, naomba kuanza kwa kusema kuwa mwanazuoni mmoja ametafsiri viongozi wa kisiasa kuwa ni muhimu sana katika mamlaka za Serikali na hufanya maamuzi sahihi yanayoweza kuleta manufaa zaidi katika ustawi wa Taifa na watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kuanza kwa kusema hivyo nikiamini kwamba sisi kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa kama viongozi wa kisiasa tunalo jukumu la kuhakikisha kuwa tunaishauri Serikali, tunaisimamia vyema ili kuhakikisha ustawi wa Taifa letu pamoja na wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa sababu yeye ameonyesha mfano wa yale ambayo nimeyatangulia kuongea, akiisimamia nchi yetu ya Tanzania kuhakikisha kwamba Watanzania wanaongozwa vizuri katika sehemu ya Utawala Bora lakini pia Watanzania wanaweza kupata ustawi na maendeleo katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI nikianza na suala la ujenzi wa vituo vya afya, pamoja na hospitali. Serikali imejitahidi sana kujenga na kukarabati vituo vya afya na hospitali, hiyo yote ni katika kuhakikisha inaboresha huduma za afya katika maeneo mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Mkoa wa Mwanza tumefaidika katika ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya kama ambavyo imekuwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini, Mkoa wa Mwanza tumepata takribani shilingi bilioni 10.3 ambayo imetusaidia kurekebisha vituo vya afya katika maeneo mbalimbali Mkoani Mwanza vikiwemo Wilaya ya Ukerewe, Wilaya ya Kwimba, Wilaya ya Magu, Wilaya ya Misungwi na Wilaya nyingine zote Mkoa wa Mwanza zimeweza kufaidika kwa kupata vituo vya afya na hospitali za wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizo za Serikali, zipo changamoto mbalimbali ambazo zinatokea katika jamii yetu. Maeneo kama ya visiwani, bado hawajaweza kupata huduma za afya kwa sababu wanatembea umbali mrefu na ukiangalia Mkoa wa Mwanza ni Mkoa umezungukwa na visiwa vingi. Kwa maana hiyo, wananchi wanapata changamoto ya usafiri kuweza kufikia huduma za afya kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ukiangalia Wilaya ya Ukerewe na Wilaya ya Ilemela, kuna Visiwa vya Irugwa Kisiwa cha Bezi. Wananchi ambao wanahishi katika visiwa hivyo ambavyo nimevitaja bado wanapata changamoto ya kufikia huduma huduma za afya. Ombi langu kwa Serikali, naiomba Serikali katika bajeti yake hii waweze kutenga fedha kwa ajili ya kutengeneza kujenga vituo vya afya katika maeneo hayo ya visiwani ili wananchi waweze kuzifikia huduma za afya kwa ukaribu na hatimaye kuweza kuokoa maisha ya wananchi, hususani tukiwalenga kundi maalum ambalo ni akina mama na watoto ili kuweza kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mwanza pia tunayo Hospitali ya Ukerewe ya Wilaya ambayo ipo pale Nansio. Hospitali hii ya Wilaya ya Ukerewe inawahudumia wananchi wengi sana kutoka maeneo ya visiwani kule Ukerewe. Sasa kuwapunguzia wananchi kutoka Ukerewe kwenda kupata tiba au kwenda kupata huduma za kiafya za kibigwa, ninaishauri Serikali kuweza kukarabati Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe ambayo ipo pale Nansio. Hii itawasaidia wananchi wanaotaka huduma maeneo yale kwani hawapati huduma za kibigwa za kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naiomba Serikali iweze kutenga fedha katika kipindi hiki cha bajeti ili kuhakikisha kwamba hospitali hii ya Wilaya ya Ukerewe ambayo inahudumia wananchi wengi iweze kutoa huduma za Kibigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuchangia katika suala la elimu. Pamoja na juhudi za Serikali kujenga madarasa na shule za mabweni katika maeneo mbalimbali, bado tunazo changamoto kwa watoto wetu wa kike ambao wanatembea mwendo mrefu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa kike anapotembea mwendo mrefu, njiani anakutana na vikwazo mbalimbali. Atakutana na madereva wa bodaboda watamshawishi kupanda usafiri ili aweze kufika haraka shuleni. Atakutana na watu tumezoea kuwaita mashunga dadys, wataweza kumrubuni mtoto wa kike na kukatisha masomo yake hatimaye aweze kupata ujauzito ama la aolewe akiwa bado ni mdogo na hatimaye kukatisha ndoto zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali kufanyika, lakini bado tunayo changamoto ambapo sehemu mbalimbali ambazo ziko mbali na maeneo ya shule za msingi, zinazo-*feed* shule zetu za Kata za Serikali kwa wanafunzi kutembea mwendo mrefu. Tunaishauri Serikali iweze kujenga shule za mabweni katika shule zetu za kata ili iweze

kuwasaidia watoto wa kike wasiweze kutembea mwendo mrefu kwenda kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mkoa wa Mwanza, sisi tunazo baadhi ya shule hapa ambazo nitazitaja ili Serikali iweze kuzisaidia. Kwa sababu nimeona katika ukurasa wa 124 katika kitabu hiki cha Wizara ya TAMISEMI wamesema kwamba watajenga shule za mabweni kwa kupitia *EP4R*. Kwa hiyo, naomba katika mpango huo shule hizi ikipendeza ziweze kuingia katika mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule ya Bwisia ambayo iko Wilayani Ukerewe, Shule ya Sekondari Bujiku Sakila ambayo ipo Kwimba, Shule ya Sekondari Kabila ambayo ipo Wilayani Magu na Shule ya Sekondari Nyamadoke ambayo ipo Buchosa. Sehemu hizi zote ambazo nimejaribu kuziainisha, wanafunzi wanatembea zaidi ya kilomita tano kwenda kutafuta elimu. Hivyo, naamini kabisa kwa kufanya hivyo, wanafunzi wa kike wataweza kufaidika na hatimaye kufikia ndoto zao kama sisi wengine tulivyoweza kuzifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kuongelea suala la asilimia kumi ambalo linatakiwa kutenga na Halmashauri zetu kwa mujibu wa sheria ambayo tulipitisha wenyewe hapa Bungeni kuhusiana na wanawake ambao wanapata asilimia nne, vijana ambao wanapata asilimia nne na asilimia mbili inatakiwa kutolewa kwa watu wenye ulemavu. Kwa bahati mbaya sana baadhi ya Halmashauri zetu hazitimizi sharti hili la kutenga hii asilimia kumi. Nafahamu kabisa kwamba Halmashauri mbalimbali zinapata changamoto ya mapato kuwa ni madogo lakini kwa sababu hiki kitu kimewekwa kisheria, ninaamini wanatakiwa kuzitenga fedha hizi. Kwa bahati mbaya fedha hizi hazitengwi, matokeo yake, hata viongozi wakubwa wanapokuja kutembelea katika Majimbo yetu, taarifa ambazo wanazopatiwa siyo za ukweli. Kwa mfano, wanaambiwa Halmashauri imetoa shilingi milioni 500, unajuliza swali, hivi katika Halmashauri kwa mfano ya Jiji, hiyo ndiyo fedha pekee iliyopatikana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kuhakikisha wanafuatilia Halmashauri ambazo hazitengi fedha hizo za asilimia kumi ili waweze kuzitenga na kuweza kuwasaidia wananchi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Mwantumu Dau na Mheshimiwa Mipata ajiandae.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa ruhusa yako nami napenda kuongelea katika taarifa hizi mbili za Wizara ya TAMISEMI na Serikali za Mitaa. Kwanza niweze kumpongeza Waziri wangu Mheshimiwa Jafo pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuchika.

Vilevile niwapongeze na Manaibu wake wote aliokuwa nao jinsi wanavyoweza kufanya kazi. Pia nampongeza mama yangu Mary Mwanjwela kwa kuteuliwa kuwa Naibu wangu wa TAMISEMI na Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Hebu jina likae, vizuri Mheshimiwa Mwantumu. Mheshimiwa Mwanjelwa.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Mwanjelwa nakupongeza sana, kuwa Naibu wangu wa Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja kwenye mchango wangu, kwanza nianze kuzungumzia suala la *TARURA*. *TARURA* ni chombo ambacho kinafanya kazi vizuri na wanafanya kazi kwa juhudi kubwa, lakini kila anayesimama hapa anaisifu *TARURA*. Katika kutembelea miradi yetu, nimeiona *TARURA* kama kweli inafanya kazi tulipokwenda Mtwara na nimeziona barabara zile za *TARURA* jinsi zinazofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokiona pale juu ya zile barabara, kuna barabara zimejengwa 2017 tu, lakini tayari zimeshaanza mashimo. Katika kuangalia barabara zile, mimi nahisi yale malori yetu ambayo yanasimama katika barabara, yanamwaga *oil*. Zikishamwaga *oil*, zile barabara zinavimba, zinafanya mashimo halafu utazona zipo kwenye uchakavu, kumbe zile barabara bado zingali mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuogelea katika suala hili napenda Serikali ifanye juu chini kutokana na zile barabara za *TARURA* na yale malori jinsi yanavyomwaga ile *oil* waweze kuzifuatilia na kuzifanyia utaratibu kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niogelea katika suala la mradi wa *TASAF*. Kila ninaposimama nazungumzia mradi wa *TASAF*, nawapongeza sana kwa sababu wanafanya kazi nzuri na kila siku nikisimama huwa nawaambia *big up*, maana wanafanya kazi kwa hali na mali, watu wetu ambao waliokuwa wanyonge hivi sasa hivi wana wanajisikia kutokana na *TASAF* inavyofanya kazi. Wale watu wanapata pesa za *TASAF*, kisha wanafanya miradi yao na ile miradi yao inaonekana; kuna wengine wana ufugaji wa mbuzi, kuna wengine wanajenga nyumba zao, wanapata kustirika na wengine wanapeleka watoto wao shuleni. Kwa hiyo, naomba sana, *TASAF* isije ikaondolewa maana tayari ni mkombozi wa wanyonge katika Tanzania yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niogelea pia kwenye suala la uzazi salama; hivi sasa hili neno lazima tuliweke mbele kutokana na watoto wetu. Uzazi salama, watoto wanapokuwa wamezaliwa na wazazi wao tayari wanakuwa wanashughulikiwa na watoto wale kila mmoja anapata haki yake kwa mama yake. Hata hivyo, kuna suala nimeliona kwa macho yangu Dar es Salaam, kuna watoto ambao wanapelekesha na wazazi wao, wanakaa pembeni ya barabara na wanatumwa watoto wa miaka minne waje pale kwenye barabara zile, gari zinapokuwa zimepaki, kuja kuomba pesa. Hapa tayari wale watoto wameshakuwa wanaanza kudhalilika, maana wazazi wamekaa pembeni watoto wao ndio wanaotumikishwa. Kwa hiyo, naiomba

Serikali ifanye juhudi juu chini, juu ya kazi zao wanazozifanya, maana inaonekana limepungua sana suala lile la ombaomba na kuwatumikisha watoto, lakini bado hili suala linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niogele katika suala la Bodi ya Mishahara ya Watumishi wa Umma. Bodi hii nimeangalia hapa vizuri tu katika taarifa ya Mheshimiwa Mkuchika kwamba kuna watumishi wa umma ambao wanafanyiwa utaratibu wa mishahara yao wapate kulipwa maslahi yao kihakika. Hata hivyo, bado watumishi wa umma wanasikitika hawapati mishahara yao kikamilifu na bado wanasikitika hawajaongezewa mishahara. Mishahara yao bado haijaongezwa na bado inakawia kuingizwa ili wajikwamue kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchango wangu kwa hii leo nilikuwa nataka nijikite katika masuala hayo. Pia nataka kumpongeza Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa jitihada zake anazozichukua hivi sasa kuzungukia mikoa yote na kesho tukijaaliwa tunaambiwa yuko hapa Dodoma. Kwa hiyo, nampongeza sana pamoja na Makamu wake, wanafanya kazi vizuri, waendele kufanya kazi ili wazidi kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa umeogelea vizuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Mipata, atafuata Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Bwanaussi ajiandae.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uzima. Vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya na kujitoa kwa moyo kutumikia Watanzania. Kazi anayoifanya tunaiona, tuko nyuma yake na kila mwenye

macho anaona. Kwa hiyo tunamuunga mkono, hayuko peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Mawaziri wote wawili mzee wangu Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Jafo, pamoja na Manaibu Waziri Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Mwanjelwa Machuche. Wamekuwa wakitusaidia sana na siku zote wanatusikiliza na mara tunapofikishia hoja zetu wanatusaidia vizuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na miradi ya afya. Kazi nzuri sana imefanywa na Wizara hii ya TAMISEMI hasa katika eneo hili la afya, sisi kwetu tumefanikiwa kupata vituo vya afya vitatu na sasa wanatuongezea kimoja lakini pia tumepata Hospitali ya Wilaya tumepata hela za kutosha bilioni moja na milioni mia tano mwaka jana na mwaka huu wametuongezea milioni mia tano, jambo hili ni zuri sana. Kwangu mimi nimeweza kupata pia kituo cha afya cha Wampembe ambacho Mheshimiwa Jafo aliweza kutembelea alipotushauri, tunamshukuru sana sana, kazi pale imefanyika vizuri na ushauri aliotupa tunaendelea nao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niseme changamoto moja, vituo hivi vinapokamilika kuna jambo bado linabaki kuwa ni tatizo kwa akinamama wetu hata wale wa vijiji vya jirani. Ningeshauri wazo hili liendelee kwenye vituo vyote vinavyokamilika, tuwe tunaweza kujenga jengo la kuwafanya akinamama wajisubirie pale, *maternity waiting home*, itatusaidia kufanya wale ambao wako mbali kidogo wasogee na waweze kujisaidia vizuri zaidi na kupata huduma inayotakiwa. Vinginevyo habari ya kujifungulia nyumbani itaendelea hata kama vituo vipo kwa sababu gharama zile wanashindwa kujimudu kwenda kukaa pale na kukaa kwa ndugu ni ngumu kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga vituo vya afya vingine Ninde, tunajenga kituo cha afya na wananchi wamejenga majengo mazuri, vyumba kumi wamekamilisha lakini King'ombe tunajenga kituo cha afya, Kate pia

wanajenga kituo cha afya, Kasu wanajenga kituo cha afya, tunaomba wanapopata nguvu tena waweze kutusaidia kwenye maeneo hayo. Hata hivyo, Kata ya Kala iko mbali sana na akipatikana mgonjwa kule anapata shida kufika kwenye kituo cha afya hasa akinamama na watoto, naomba tupate gari ya wagonjwa ili isaidie katika kuhudumia katika eneo hilo. Tumejenga zahanati nyingi zipatazo 10, zote zimefikia mtambaa panya, hatujapata uwezo wa kuweza kuezeka, lakini tunahamasisha wananchi ili tujenge. Naomba mtusaidie ziko zahanati ya Kisambala, Kantawa, Kipande, Kalundi, Nkomachindo, Ifundwa, Tundu, Kilambo, Ntuchi na Nchenje zimeezekwa, ni pesa kidogo tu zinatakiwa ili kuzikamilisha wananchi waanze kupata huduma. Naomba Serikali itusaidie na kama haiwezi kutusaidia itusaidie hata kuibana Halmashauri zaidi ili watusaidie katika zahanati hizi ambazo karibu zinakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nizungumzie kuhusu Bima ya Afya. Bima ya Afya nzuri na inasaidia sana wananchi na mara nyingi watumishi wa taasisi mbalimbali na wa Serikali ndio wanaosaidiwa zaidi. Mpango wa kuwezesha wananchi wote kwa ujumla Watanzania wapate huduma ya Bima ya Afya umefikia wapi? Naomba nihimise Serikali ione umuhimu wa kufanya hivyo. Sambamba na hilo niwaombe, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana watumishi wa Bima ya Afya hasa waliojipanga kuhudumia Wabunge yupo Flora Mtabwa na Felister Mabula, hawa watu wakipata dharura wanachukua kwa haraka sana na wanatusaidia na wanajipanga vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme kuhusu hospitali ya Muhimbili, Muhimbili sasa hivi huduma zimejipanga vizuri, watu wanafanya kazi kama mchwa, ukipata dharura ndio unaweza ukajua kumbe sasa tuna hospitali ya Taifa yenye kiwango na inahudumia vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waganga hatuna, tunaomba Wauguzi kwetu kule Nkasi hatuna hasa pembezoni. Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Jafo

watusikilize na Mheshimiwa Waziri anapajua, bahati nzuri umeshafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu *TARURA*. *TARURA* kama wenzangu wanavyosema naunga mkono tuwape asilimia 50 kwa 50, lakini sisi leo hii kutokana na *TARURA* hatuwezi kufikika kwenye vijiji kadhaa, Kijiji cha Kisula siweze kufika kwa sababu barabara imekatika na mvua na hakuna fedha za dharura. Kwa hiyo *TARURA* haina hata uwezo wa kukabili dharura yoyote inayotokea mpaka waombe. Sasa jambo hili sio zuri sana, kwa hiyo naomba sana Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba *TARURA* wanapata pesa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna daraja la Ninde, Kata nzima haiwezi kufikika kwa sababu ina barabara moja, daraja limevunjika hakuna pesa na tumeshatuma maombi, lakini bado hatujapata pesa, sababu hawana pesa, kwa hiyo tunaomba. *TARURA* pia hawana watumishi, watumishi wake wako kwa mkataba, naomba waajiriwe, kama ni kujaribiwa wamejaribiwa muda wa kutosha ili watu waweze kujiamini. Sasa hivi wanafanya kazi kwa mikataba ya miezi mitano mitano au sita sita haiwezekani! Wapeni uwezo *full mandate* waweze kufanya kazi vizuri itasaidia. Vilevile hawana magari ya *supervision* hasa kule wilayani, lakini vilevile hata huku hawana pesa za kutosha, naomba watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendee katika eneo la maji. Kuna miradi ya maji ambayo inatekelezwa ya vijiji kumi hivi vya Benki ya Dunia. Miradi mingi imefanya kazi bila utafiti wa kutosha, usanifu wake haukuwa mzuri, Kijiji cha Nkundi kina mradi umegharimu zaidi ya bilioni mbili, lakini maji hayatoki. Naomba Serikali ione utaratibu wa kuwezesha vijiji kama hivi viweze kupata wataalam wa kutosha au kuona vikwazo gani vinafanya maji yasitoke katika gharama yote hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kisula vilevile maji bado ingawaje wao wanaendelea na mradi. Miradi wa Mpasa, mradi wa Isale una zaidi ya bilioni tano katika Jimbo

langu, lakini unaendelea vizuri, tumeshafanya kazi za kutosha, mkandarasi anaendelea vizuri, ila *certificate* tuliyoomba bado haijarudi ili kazi iweze kuendelea vizuri zaidi. Kwa hiyo, naomba Serikali itupe hela ambayo tulishaomba ili Mkandarasi aendelee na kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme, kuna vijiji vilirukwa katika awamu ya kwanza na ya pili, nikienda kule naonekana kama kichekesho; Kijiji cha Katani, Kijiji cha Malongwe, Kijiji cha Nkana, Kijiji cha Sintali, Kijiji cha Nkomachindo, ni vijiji ambavyo vinanitesa, nashindwa hata namna gani niweze kwenda.

Naomba nitumie hadhara hii Mheshimiwa Waziri wa Nishati anisikie, vijiji hivi ni kero, nikienda jimboni, sina raha hasa kwa sababu wamezungukwa na vijiji vyote vyenye umeme. Ingawaje bado kuna vijiji vingi kabisa ambavyo havina umeme, lakini hivi ndio zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kama nitapata muda ni kilimo, kilimo kikiboresha ndio halmashauri zinaweza kupata mapato ya kutosha. Kwa sasa hivi natoa ushauri kwamba ruzuku iliyokuwa imewekwa kwenye kilimo, irudi kwa sababu ilikuwa inabeba watu wa chini zaidi. Ruzuku iliyoko sasa hivi inawabeba wakubwa wakubwa tu, wenye uwezo wa kwenda kununua pembejeo madukani, lakini wale wenzangu na mimi inakuwa ni ngumu sana kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia masoko ya mazao ya wakulima, Mkoa wa Rukwa bila kuwa na masoko ya kutosha, wataalam mko wapi? Tutafutieni masoko ya wakulima kwa sababu tunawahimiza wakulima walime, wanatupa sayansi za kuvuna vizuri zaid, sasa tukishavuna tunaweka vyakula vinaharibika na vinauzwa kwa bei ya chini, watu wanakufa moyo. Kwa hiyo naomba sana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Natambua sana kwamba Serikali ya Mitaa zinafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ili kumbukumbu zetu zikae vizuri jina la Mheshimiwa Naibu Waziri Mary Machuche Mwanjelwa, yeye yupo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na sio TAMISEMI.

Tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia machache kwenye Wizara hizi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri hasa wa Wizara hizi pamoja na Manaibu, nawapa hongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mambo ya afya; kwa Mkoa wetu wa Morogoro kwa kweli na Tanzania nzima afya imefanya vizuri sana, Nashukuru kuona kwenye bajeti hii ya mwaka 2019/2020 tumeweza kutengewa fedha kwenye vituo vya afya Mkoani Morogoro ikiwepo Mvumi, ambayo imetengewa milioni 200 ambayo na mimi nimeshaichangia matofali 2000. Pia napongeza kwa upande wa kituo cha afya cha Dumila ambao na wenyewe wametengewe milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwa vituo vya afya vingine ambavyo bado havijaweza kutengewa, kikiwepo kituo cha afya cha Mzinga, ambacho tayari wamejenga kwa nguvu za wananchi, lakini hakijakwisha, kikiwepo na Magadu pamoja na Mafisa na vituo vingine ambavyo sikuvitaja kwenye Mkoa wetu wa Morogoro kwenye Halmashauri zote za Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pongezi zangu kwa Serikali kwa upande wa kutenga fedha za hospitali za Halmashauri ya Wilaya. Tunashukuru sana kwa upande wa

Gairo, tumeweza kutengewa milioni 500, Kilombero milioni 500, Mvomero milioni 500, pamoja na Morogoro Wilaya milioni 500. Hii kwa kweli nashukuru kwa sababu Hospitali ya Mkoa ilikuwa inapata matatizo sana ya msongamano wa wagonjwa hasa kwa upande wa wazazi ilikuwa ni kazi kweli, kwa sasa hivi naona tatizo hili litakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona hela kwenye upande wa hospitali ya Wilaya ya Manispaa ya Morogoro ambayo inajengwa na inatumika, lakini haijatumika sawasawa kwa sababu bado haijakamilika. Kwa hiyo, naomba Serikali waweze kuangalia na waweze kunijibu kama kweli wamenitengea kwa sababu sijaona hela yoyote ya hospitali ya Manispaa pale mjini. Naomba hospitali hii iweze kuangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa watumishi hasa kada ya afya pamoja na elimu kwa Mkoa wa Morogoro bado tuna matatizo. Kwa upande wa wataalam wa afya na hasa ukikuta kwenye vituo vile ambavyo viko pembezoni kwenye Wilaya za pembezoni kama Malinyi, Ulanga unakuta kuwa kituo cha afya au zahanati inaweza ikawa na Mganga mmoja ambaye hawezi. Halafu mimi mwenyewe nimeshuhudia, unakuta hivi vituo vya afya vingine vinafungwa saa tisa. Jioni havifanyi kazi, usiku havifanyi kazi, hapo kwa kweli sielewi. Naomba Wizara waliangalie kwa sababu ugonjwa hauchagui ni saa ngapi unaumwa, saa yoyote unaumwa, kwa hiyo naomba waliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, Walimu ni pungufu na hasa kwa upande wa Walimu wa sayansi naomba watupatie hao Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha sana kuipongeza Serikali kwenye miradi ya kimkakati kwa kweli Manispaa ya Morogoro tunaringa na wananchi wanajivuna na Mkoa wa Morogoro wote kwa sababu Manispaa ni kioo. Mpaka sasa hivi tuna soko ambalo tunajenga, soko zuri sana ambalo tumetengewa shilingi bilioni tati na milioni mia tano kwa bajeti hii. Kwa hiyo tunashukuru, pia tuna wale

wanaopita pale Stendi, wote mnaiona kuwa Stendi ya Morogoro ni nzuri kwa hiyo tunaishukuru Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya msingi bila malipo, Mkoa wa Morogoro kwa kweli Serikali inafanya vizuri chini ya Mheshimiwa Rais, lazima niipongeze kwa sababu upande wa elimu bila malipo, kwa upande wa shule za msingi tumeweza kutengewa zaidi ya billioni sita na pia kwenye sekondari zaidi ya bilioni sita. Tunaishukuru sana Serikali iendelee kufanya vizuri kama inavyofanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ninaloomba ni kwa upande wa hosteli, hospitali ambazo zitajengwa naomba ziweze zijengwe kwenye shule za wasichana kwa sababu watoto wa kike wanapata matatizo sana na wao wanayajua kwa mimba za utotoni na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuwa kuna magari kama 40 ambayo yatanunuliwa na kutawanywa kwenye halmashauri ambazo zina mazingira magumu. Kwa kweli kwenye Halmashauri ambazo zina mazingira magumu naomba kuomba kupatiwa gari moja kwa Halmashauri ya Malinyi, ambayo iko mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wananchi kiuchumi, asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa walemavu ni jambo zuri sana ambalo limeweza kufanywa na Serikali, lakini kuna wale ambao hawatimizi masharti. Naomba hayo masharti yaangaliwe vizuri kusudi hao vijana waweze kurudisha kwa wakati na hizi hela ziweze kuwasaidia. Kwa upande wa wanawake wanarudisha vizuri, lakini vikundi viko vingi, kwa hiyo naomba Wizara wanisikilize, waweze kuangalia jinsi ya kuwasaidia hawa wanawake ili waweze kupata hela nyingi na za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TARURA*, ni kweli wanafanya vizuri lakini wanapata hela kidogo. Kwa upande wa Morogoro kwa barabara za vijijini naona hawajaweza kuendelea vizuri kwa sababu hela hazitoshi. Kwa

hiyo, naomba waongezewa hela ili kusudi waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Manispaa kuna barabara za pembezoni ambazo wanazisahau. Kwa mfano kama barabara za Magadu na SUA kwa wasomi. Naomba na zenyewe waweze kuzitengeneza vizuri kadiri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwa upande wa lische. Tanzania yetu ina udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ambapo 34% wamedumaa, kuna utapiamlo lakini Serikali imeweza kuona kuwa ni jambo...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Dkt.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja za Wizara zote mbili, ahsante sana na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ameen.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Bwanausi atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka na Mheshimiwa Zuberi Kabwe ajiandae.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kwenye hotuba ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Waziri wa Nchi anayeshughulikia mambo ya Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. Nimemshangaa sana ndugu ya Mheshimiwa Ngombale pale alipotamka kwamba anaitaka Serikali iwaombe radhi wakulima wa korosho.

Mimi nasema Serikali haiwezi kuomba radhi ila inapaswa kupongezwa kwa hatua iliyoichukua kwa kuwanusuru wakulima wa korosho. Mheshimiwa Ngombale yeye analima ufuta, nimeshangaa sana anaposema habari ya korosho na Wilaya Masasi ambayo natoka mimi ndiyo Wilaya ya pili kwa uzalishaji nchini baada ya Tandahimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa wa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi alivyolishughulikia suala la korosho na kuwasamehe wale ambao walinunua kinyume na utaratibu almaarufu kama 'kangomba'. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunashuhudia jinsi wananchi wanavyojitokeza kwa wingi, nimeona mkutano wa pale Mufindi, Iringa, Mtwara, Namtumbo, kwa kweli Watanzania wana imani kubwa na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. Nadhani vyama vya upinzani mwakani itabidi wajitafakari kuona kama kuna sababu ya kumweka mgombe Urais kwa sababu kwa hali ile navyoiona sidhani kama kutakuwa na mgombea yeyote atakayeweza kushindana na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

WABUNGE FULANI: Aaaaaa.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana jirani yangu Waziri Jafo na wasaidizi wake ndugu yangu Mheshimwa Kandege na Mheshimiwa Waitara kwa kazi kubwa mnayoifanya TAMISEMI, hongereni sana. Mheshimiwa Jafo namfahamu siku nyingi sana na wengi tunamfahamu pale alipokuwa *Plan International* aliwahi kuwa mfanyakazi bora lakini Bunge lililopita tulimchagua Mheshimiwa Jafo kutuwakilisha kwenye Bunge la *SADC*. Mheshimiwa Anne Makinda aliwahi kusimama hapa akasema anatuwakilisha vyema baada ya kupewa Kamati kule kwenye *SADC*, tunakupongeza sana. Kwa hiyo, haya unayofanya TAMISEMI ni mtiririko wa utendaji kazi wako uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri, Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika na Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, msaidizi wake katika Wizara hii. Tunapongeza tuna maana, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, yeye ni kati ya wachache ambao wapo madarakani waliowahi kuteuliwa kwa nafasi mbalimbali kuanzia DC, RC hadi Waziri katika vipindi vyote vya Marais watano walioongoza nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Baba wa Taifa alimteua kuwa DC na Mheshimiwa Rais Mwinyi akamteua kuwa DC baadaye Mzee Mkapa akamteua kuwa RC. Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete na Mheshimiwa Dkt. Magufuli wote wammeteua Mzee huu kuwa Waziri katika awamu zao. Kwa hiyo, kwa kweli tunampongeza kwa utendaji wake mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la TAMISEMI, hii ni Wizara ngumu sana. Bahati nzuri nimekulia TAMISEMI, nimekuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, Diwani kwa miaka 10, Meya na sasa Mbunge, naifahamu TAMISEMI ni ngumu sana. Kwa mfumo Mheshimiwa Jafo, Manaibu, Katibu Mkuu na watu wa TAMISEMI kwa ujumla sasa haitembezi bali inakimbia kwa utendaji wenu wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya elimu wengi wamezungumza sitaki kurudia sana lakini nikuombe Mheshimiwa Jafo pamoja na juhudi ambazo zimeendelea kufanywa hasa katika Jimbo la Lulindi kama nilivyokuwa nikieleza mara kwa mara kwamba sasa hivi kituo kinachofanya kazi ni kimoja tu cha Nagani. Namshukuru Mheshimiwa Rais nilipomuomba suala la gari amenikubalia na wananchi wa Lulindi wanashukuru sana kwa jinsi ambavyo amesikiliza kilio kile. Bado nikombe Mheshimiwa Jafo na Naibu Katibu Mkuu Afya na timu nzima ya Naibu Mawaziri, Mungu akiwajalia mkapata fedha za kuongeza vituo vya afya tunahitaji kituo muhimu sana cha afya cha Mnavila kilichopo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naomba kituo hiki kwa haraka sana? Tunalo tatizo kubwa sana la wananchi wetu kupoteza maisha na viungo kutokana na wimbi kubwa la kuzaana kwa mamba katika Mto huu wa Ruvuma. Tatizo lililopo ni kwamba hatuna kituo cha afya karibu, hivyo, kukitokea majanga ya namna hiyo wananchi wetu wanapata tatizo la kupoteza maisha ama kupata ulemavu kwa sababu hakuna huduma ya haraka katika eneo hilo. Kutoka pale Mnavila kwenda kwenye kituo cha afya ni zaidi ya kilomita 50. Kwa hiyo, nikuombe sana kwa huruma yako kwa kweli kituo hiki ni muhimu sana kipatikane ili tuweze kuwanusuru wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili hili la ujenzi wa hospitali, nishukuru kwa kunipatia Hospitali ya Wilaya ambayo inajengwa hivi sasa pamoja na kituo pale Chingutwa. Nashauri kitengo kile kinachohusika na gharama za majengo haya wawe waangalifu katika kutoa fedha aidha shilingi milioni 400 au 500 kwa sababu kuna baadhi ya maeneo ambapo upatikanaji wa vifaa ni mgumu inapelekwa shilingi milioni 400 lakini eneo ambalo halina tatizo inapelekwa shilingi milioni 500. Kwa hiyo, nadhani hili ni suala tu la marekebisho la kuangalia eneo ambalo lina changamoto nyingi basi ndiyo lipelekewe fedha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nishukuru kwa jinsi unavyoiongoza TARURA lakini bado Mheshimiwa Waziri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Naomba nianze kwa kuungana na walionitangulia kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa TAMISEMI na Utumishi na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazofanya chini ya Ofisi ya Rais. Suala la utawala bora ni mtambuka na nyeti na ndiyo maana labda Wizara hizi zipo chini ya Ofisi ya Rais, kwa hiyo, hapa tunazungumzia mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo basi, nianze tu kwa kueleza kwamba mapema mwaka huu nilikuwa na changamoto za kiafya nikaenda kutibiwa Marekani nikapata nafasi kukutana na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Katika maongozi yetu, alinipongeza sana na alisema maeneo yafuatavyo, namnukuu, alisema: "*You know Anna Tanzania is unique*". Ina maana kwamba Tanzania ni nchi ya pekee. Akasema kwa sababu katika katika nchi za Afrika ni nchi ambayo ina utamaduni na inaonyesha kwamba ina uwezo wa kuwa na changamoto zake na ikazitua yenyewe. Hayo ni maneno ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa Kiingereza anaitwa *Secretary General of the United Nations*, kuna wenzetu hapa walikuwa wanataka kukusikia Kiingereza chake. Tulipofika hapa katika dhana nzima ya utawala bora, sina budi kuwapongeza majemedari wetu Waheshimiwa Mawaziri ambao wana dhamana ya sekta hizi na Mheshimiwa Rais kwamba tulipofika si haba. Hii ndiyo salamu ambayo naileta kutoka kwa marafiki zangu na watu wengine ambao niko nao, juzi juzi nimetoka nchi za Nordic tulipofika si hapa. Ukiangalia Rais alipoanzia katika kuleta utawala bora tulianza na janga la madawa ya kulevya...

MBUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Kwa vyovyote mawazo yako juu ya mtu ni ya kwako lakini huwezi kusema mtu anayekuja kupambana na madawa ya kulevya atapata

marafiki, hilo ni la kwanza na dunia inalitambua. Tukaingia katika changamoto ya mikataba mibovu iliyokuwa inatumiza sana kwenye madini tukalikamilisha na mengine yanakuja. Kwa hiyo, katika dhana ya utawala bora, nafikiria Taifa zima bila kuangalia itikadi ya mtu tunatakiwa tuwe pamoja kuhakikisha kwamba tunaimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe kwa maumbile yangu (*by inclination*) ni mtu ambaye napenda sana hoja, ushindani na upinzani kama ikiwa lazima. Tunapozungumzia utawala bora lazima pia tuzungumzie upinzani bora maana hatuwezi kuwa na utawala bora kama hatuna upinzani bora, kwa sababu upinzani bora ndiyo utaleta utawala bora. Kwa hiyo, nataka kusema tunapokaa hapa wakati mwingine tunasahau *context* ya tunachotaka kufanya hapa.

TAARIFA

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa, kidogo tusikie taarifa, Mheshimiwa Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuumpa taarifa mzungumzaji anayeongea ambaye ni Profesa Mbobeve katika nchi hii. Nataka kumpa taarifa kwamba alipokuwa anaongea na huyo Kiongozi wa UN angemueleza kwamba upinzani bora unahitaji *fairness*. Kwa hiyo, nilifikiri kwamba angemsaidia na kumpa uwazi wa kinachofanyika katika Taifa letu. Mheshimiwa Profesa nataka nikukumbushe nawe ulikuwa Waziri wa awamu zilizopita na madawa hayo hayo yalikuwepo wakati wewe ukiwa Waziri. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa, taarifa hiyo.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mwakagenda kwa hiyo

perspective yake. Nimeshasema mimi ni mtu ambaye nakaribisha mawazo mbadala ila naweza kumhakikishia maongezi yangu na Katibu Mkuu yaligusa mambo yote hayo na zaidi. Cha msingi ni kwamba *Tanzania is unique*, tulipofika ni pazuri na tujipongeze na Rais wetu anakwenda vizuri Mheshimiwa Mwakagenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde dakika zangu alizozichukua Mheshimiwa Mwakagenda. Baba Mtakatifu Francis katika kazi yake ya kujaribu ku-*promote* utawala bora na uongozi wa kiroho alikuwa katika nchi za Uarabuni alifika Dubai, alitoa nasaha ambazo kwa ukosefu muda sitaweza kuzisoma hapa lakini naomba nikabidhi nyaraka hii kama sehemu ya *Hansard* ya hotoba yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba Mtakatifu anasema ni lazima tujue changamoto zipo, tatizo siyo changamoto, tatizo siyo watu wanakusema, tatizo siyo kwamba watu wanakuonea, tatizo ni wewe una-*respond* namna gani? Kwa hiyo, usikubali mtu yeyote aku-*pull down*, wewe weka hoja mezani, nyaraka hii naikabidhi ili isaidie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukiona kwenye mitandao Baba Mtakatifu anahakangaika na wenzetu wa South Sudan. South Sudan watu hawaelewani, sasa Baba Mtakatifu ameamua kuwapigia magoti, mtaona kwenye mitandao nadhani ina-*trend*, utawala bora pia unaamanisha dhamira zetu, kama unataka utawala bora lazima uangalie pia dhamira zetu. Kwa mantiki hiyo basi na kwa sifa tulizonazo tusizipoteze kwa kuokosa *nation dialog*. Ni kwa mantiki hiyo basi nataka kuchangia ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa utawala bora utataka utawala wa sheria na haki. Utawala bora lazima utokane na sheria na haki, sheria peke yake bila haki haiwezi kuleta utawala bora. Kwa mantiki hiyo, nataka kusema kwamba suala la haki Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, naomba liangaliwe kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (*DPP*) ni lazima ijiangalie pia kwa sababu huwezi kuwaweka watu gerezani bila kusikiliza kesi zao ukasema nina utawala bora. Hiyo naiweka kwa *perspective* niliyosema kwamba hapa tunachangia, hili ni Bunge la Jamhuri, tatizo letu hapa huwa ni *ideologies* zinatufanya tunashindwa kwenda *forward*. Kama mtu unatuhumiwa una makosa ni sawa lakini wachunguzi kama hawajawa na ushahidi, kusudi tukae vizuri mbele ya Mataifa na majirani wanaotuangalia na humu ndani, naomba suala hilo tuliangalie na nalisema hili bila kuwa na usabiki wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa, muda wako umeisha.

WABUNGE FULANI: Aaaaaa.

MBUNGE FULANI: Mwongezee.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Dakika tano, bado jamani, sijui kama nimeongea dakika tano. Kama nimemaliza dakika zangu nitaweka...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tibaijuka, kwa sababu Kanuni pia zinatambua watu fulani ambao wametoa mchango mkubwa kwa nchi hii na kwa Bunge hili, kwa hiyo, nakuongezea dakika tano. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa heshima hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo, naomba niende haraka na nitaweka hapa mchango wangu kama ulivyoandikwa, kwa sababu mimi ni Profesa nimeandika uingie wote kwenye *Hansard*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya muhimu ya kusema, niende kwenye suala la kuwezesha watu wetu katika utawala bora, kuna suala la kuwalipa wakandarasi wa ndani. Wakandarasi wa ndani sasa hivi Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa nalileta kwenu ni suala la utawala bora kwa sababu wasipolipwa fedha hawawezi kufanya kazi, hatuwezi kujijengea uwezo, tutabaki na Wachina peke yao. Kwa sababu ya muda umekuwa mfupi nimellafanua katika hotuba yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nikupe nyaraka nyingine ambapo kuna kitu kinaitwa Ilani ya Usafi. Utawala bora pia ni mkono wa Serikali wa kushoto kujua wa kulia unafanya nini. Sasa hivi kuna tabia mbaya, naomba niseme kwamba Maafisa Afya na Mazingira wanakwenda kwenye shule binafsi na hapa na-*declare interest* kwa sababu nina shule, wanategemea uwape bahasha kama bahasha haipo imekula kwako, unakuta unaandikiwa Ilani Chafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikukabidhi Ilani moja hapa ambayo imeandikwa kwenye Shule ya Wasichana ya Barbro ambayo huwa naisaidia, inasema tuong'oe vyoo (*WCs*) kama hivi hapa Bungeni tuweke vyoo vya kuchuchumaa. Hata hivyo, Bwana Afya hajui kwamba kwa wanawake kuchuchumaa inaweza pia ikaeneza UTI, hapa ndipo tulipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalileta jambo hili hapa mtu atashangaa kuwa ni la kisékta, siyo la kisékta ni la kiutawala bora. Sheria ya Elimu ndiyo inatawala shule, watu wa mazingira na watu wengine wale wakitaka kuingia kwenye shule lazima waende na Mkaguzi wa Shule, vitu kama hivi havifanyiki vinatuletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakaa hili lazima niliseme ni muhimu sana, naomba sana Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa na nadhani na Mheshimiwa Rais pia atatusikia ni kuhusu suala la watumishi walioachishwa kazi kwa sababu walidai kwamba wamemaliza *form four* wakati hawakumaliza, naomba tena

Mheshimiwa Rais atumie huruma na hekima yake kuliangalia upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa nafasi yangu ukiniuliza nasema kuna wengine walijaza *form* wakisema kwamba wana *form four* kwa sababu mabosi wao waliwaambia jaza *form four*. Tuje humu Bungeni, Mheshimiwa Lusinde leo sijui kama yupo au hayupo yeye huwa anapenda kujita darasa la saba lakini namjua ana-*masters* ni kwamba hana cheti tu. Unaona ni *persepective* tu huwezi kusema Mheshimiwa Lusinde ni darasa la saba siyo darasa la saba huyu, kwa elimu yake ana-*masters* na zaidi lakini kwa sababu ya *certification* ndiyo tusema darasa la saba, sisi tumekwama kwenye *certification* tunashindwa kwenda mbele. Kwa hiyo, naomba niseme jamani, jamani suala hili ni muhimu sana kuangaliwa upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kutunza vyeti, siyo kazi ya *individual*. Ni kazi ya *NACTE, BRELA*, Wizara ya Ardhi na wengine. Sisi raia hatuna *safe* ambayo ni *fireproof* kwa mfano. Kwa hiyo, cheti changu kikiungua nakwenda *NACTE* kuomba cheti changu. Sasa nina kesi za watu ambao ni Maprofesa, wamesimamishwa kazi katika Vyuuo Vikuu kwa sababu walipoteza vyeti vya *Form Four*. *This is not serious*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nitaleta kwa maandishi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zitto Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe.

MHE. KABWE Z. R. ZITO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Makadirio ya Bajeti ya Wizara hizi ambazo ziko chini ya Ofisi Rais, TAMISEMI na Utumishi na Utawala Bora. Nianze na jambo la

Utawala Bora ambalo Mheshimiwa Prof. Tibaijuka ameligusia kidogo. Naomba nilipanue zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utamaduni hivi sasa, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka kukamata watu. Hatujui kama kesi hizo wanabambikiwa au ni kesi halali, lakini baadaye tunaona kwamba watu wale wanakubaliana na Ofisi ya DPP, wanalipa fedha kesi zinakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nchi yetu ipate ufafanuzi, kwa sababu namna ambavyo jambo hili linafanywa, kwanza inawezekana kuna uonevu mkubwa sana kwamba kuna watu ambao wanabambikiwa kesi, wanapewa *money laundering offences*, wanawekwa ndani ili wakazungumze na DPP halafu waende Mahakamani wakiri walipe faini ya kile kiwango ambacho wameshtakiwa nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano dhahiri ni wa juji, ambapo taarifa ambayo VODACOM wameitoa, kwa sababu VODACOM ni *listed Company*; hawa watu wengine inawezekana *negotiations* zinafanyika na DPP zinaishia kimya kimya hatujui, lakini kwa VODACOM kwa sababu ni *listed Company* waliweka taarifa yao ile public kwa sababu wako *listed* kwenye Dar es Salaam Stock exchange na Johannesburg Stock exchange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, VODACOM wanasema, *VODACOM Tanzania has reached an agreement with Director of Public Prosecutions (DPP) for five detained employees to be released. The agreement include payment of five point two billion Tanzania Shillings by VODACOM to Tanzania in order to settle charges initiated by DPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nipate uelewa. Nchi yetu haina sheria wala kanuni zinazoweza pale ambapo mtu anakuwa ametuhumiwa kujadiliana na *prosecuter* ili ama kupunguza adhabu au kufuta adhabu au kulipa faini. Haya makubaliano ya DPP na watuhumiwa yanaendeshwa kwa sheria ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa *revenue book*, kila Mbunge amepewa. Ukitazama *revenue books* hizi, kuna kila senti ambapo kila Idara ya Serikali inaingiza. Nimeangalia *Vote 35 - The National Prosecutions Services*, kwa miaka mitatu yote ya nyuma na hata mwaka huu, wanatarajiwa kuingiza shilingi milioni 14 tu. Mwaka 2018 peke yake *DPP* wamefanya *transactions* za zaidi ya shilingi bilioni 23 kwa watu ambao wanakamatwa na ku-*settle* kesi kati yao na *DPP* wanaenda Mahakamani kesi zinafutwa. Naomba kufahamu, kwa sheria ipi? Fedha zinakwenda wapi? Nani anazikagua hizo fedha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni jambo ambalo tukilikalia kimya tunatengeneza *a gangstar republic*, kwamba dola inaweza ikaenda ikamkata mtu, ikamzushia, ikamwambia ukitaka utoke, toa hela; watu wanatoa hela, wanatoka. Hatuwezi kuendesha nchi kama *gangstars*. Naomba tupate maelezo ya jambo hili, ni namna gani ambavyo linakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili...

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MBUNGE FULANI: Tulia wewe...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stella Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kwa mujibu wa kauni ya 64 1(a) na kuendelea, naomba kufuatia maelezo ambayo Mheshimiwa Zitto anayazungumza, badala tu ya kuyaweka kwa ujumla jumla na kwa sababu vyombo anavyovizungumzia ni vizito na vinavyoheshimika katika nchi hii, ni vyema akatoa kwa vielelezo vikaja mbele ya kiti chako ili hata watakapokuja ku-*respond* wajue ni kitu gani anakizungumzia kwa uhakika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kulizungumzia ni TAKUKURU. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU ndiyo Taasisi ambayo tumeipa dhamana ya kupambana na Rushwa. Nimeona kwenye bajeti ya mwaka huu tunawaomba shilingi bilioni 75, lakini taarifa ambazo ninazo za uhakika ni kwamba kwa takribani miaka minane iliyopita TAKUKURU hesabu zake hazijawahi kukaguliwa na *auditor* yeyote yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu kutoka Ofisi ya Utawala Bora, ni kwa nini TAKUKURU, licha ya kwamba sheria tuliyoitunga mwaka 2007 inataka wafunge mahesabu na wakaguliwe, kwa nini TAKUKURU hawakaguliwi na kila mwaka tunawatengea mabilioni ya fedha, tunawaamini kwamba wanapambana na rushwa, lakini wao wenyewe fedha ambazo tunawapa hazikaguliwi na wala hili Bunge haliwezi kuziona? Ni kwa nini jambo hilo linaendelea kufanyika? Naomba Serikali iweze kutoa maelezo ya hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, utawala bora pia na hili jambo ni la muhimu sana; kuna watu kwenye nchi ambao ni lazima mhakikishe ya kwamba hawakugusiki na mambo machafu au hata hisia. Nimesoma hotuba ya Ofisi ya Rais hapa ukurasa wa 87 ambapo Bunge linajulishwa kuwa kwa mujibu wa *GN*Na. 252 ya mwaka 2018, sasa Wakala wa Ndege za Serikali umehamishiwa Ofisi ya Rais kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu kwamba mwaka 2017/2018 tulitenga fedha shilingi bilioni 509, mwaka uliofuata shilingi bilioni 497 na mwaka huu zinaombwa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa ndege za *ATCL*. Sisi wote tunajua *ATCL* hawamiliki ndege zile. Ndege zile zinamilikiwa na Wakala wa Ndege wa Serikali. *ATCL* inakodishiwa ndege zile. Halafu tumepitisha huko, tunategemea kwamba *CAG* atakwenda kukagua Wizara ya Ujenzi na kadhalika, ghafla tunaambiwa kwamba Wakala wa Ndege za Serikali hayuko

tena Ujenzi, iko Ofisi ya Rais. Serikali inaenda kuficha nini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mtu mwingine anafanya *procurement*, una mtu mwingine anamiliki ndege, una mtu mwingine anaziendesha zile ndege; Serikali inataka kuficha nini? Kwa nini mnafanya mambo bila kutumia maarifa mnajaza jambo kama hili lenye ma-*procurement* ya hela nyingi, chini ya Ofisi ya Rais? Likitokea doa hata kidogo, mnamgusa Rais moja kwa moja. Nasi hatulaza damu, tutasema moja kwa moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hivi vitu huwa vinatenganishwa ili angalau Mkuu wa Nchi anakuwa juu aweze ku-*deal* na hawa wa chini. Mnalundika *procurement* yote, zenye utata hatujui zilitangazwa lini, *negotiations* zilikuwaje, ndege zinadondoka kila siku. Juzi hapa *KQ Dreamliner* yao imekwama, imetua Dar es Salaam. Ikianguka yetu hapa, twende tukamlaumu Rais? Hivi si ni vitu vya kawaida tu ambavyo wataalam mnapaswa kukaa na muepushe! Hata mwenyewe akitaka, mnamwambia mzee hatuwezi kufanya, tukifanya tutakuletea shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya Serikali ni kwa nini maamuzi haya yamefanywa? Maamuzi haya mmefanya wakati Bunge linaendelea, maana yake ilikuwa Bunge linaendelea, ni Juni 2018, tayari tumeshapitisha Bajeti inayokwenda kununua hizo ndege kwa ajili ya kwenda Wizara ya Ujenzi, halafu pia mambo yote hayo yamepelekwa Ofisi ya Rais na tunajua hapa kuna *controversies* za *Vote 20* ambazo naomba nipate maelezo haya ya Serikali... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Freeman Mbowe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mlinga.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niungane na wenzangu kuchangia katika hoja hii ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanzia hapo ambapo amemaliza Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, kuzungumzia hoja ya utoaji haki katika Taifa na hilo suala amelizungumza vilevile Mheshimiwa Mama Tibajuka. Nalizungumza kama mhanga ambaye nimekaa Magereza kwa siku 104 na Mheshimiwa Matiko na fursa ile ya kuishi Magereza imetupa nafasi kubwa sana ya kujua hali halisi ya nchi yetu. Imetupa nafasi ya kujua hali halisi sisi Wabunge tunapotunga sheria tunafikiri sheria hizi hazituhusu, kwa hiyo, tunatunga sheria nyingine ambazo ni ngumu na mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umekuwa ni utamaduni wa Serikali kugeuza kesi za *money laundering* kama chanzo cha mapato ya Serikali, yaani inaonekana kama kesi za *money laundering* ni mkakati mpya wa kukuza mapato ya Serikali. Watu wanakamatwa, uchunguzi unaendelea miezi sita au mwaka mzima, Magereza za Dar es Salaam zimejaa mahabusu zaidi ya 5,000 ambao kesi zao zinaendelea hawapewi haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamekaa ndani miaka mitatu, wengine wamekaa miaka minne, kesi zao wengine hawazijui. Sasa tunalundika Magereza zetu kwa watu ambao kwa kweli walistahili kuwa nje kwa misingi ya dhamana. Utamaduni huu unaharibu *investment climate* ya nchi kwa sababu watu wanaokamatwa wanatoka kwenye Makampuni na Mashirika makubwa ambayo yanatoa mapato makubwa kwa Serikali yetu. Lazima Serikali iangalie namna ya ku-*leverage* haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kweli tukasimamia sheria na kukawa na haki katika Taifa, lakini upande wa pili tujue athari zake kwa uchumi wa nchi. Sasa tunakamata watu na watu wengine mnaowakamata, wanaoshtakiwa kwa makosa mbalimbali ya rushwa ni watu ambao wako katika

miradi ambayo iko chini ya PPP. Leo Mkurugenzi na mke wake na viongozi wengine wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam wako mahabusu kwa kesi za *money laundering* na huyu mtu ni mbia wenu, mngeweza mkakaa nao kwenye Vikao vya Bodi mkamaliza mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea na utamaduni huu, ni nani atakuwa na *confidence* ya kuwekeza na Serikali wakati Serikali yenyewe inawaweka ndani wabia wake? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nilizungumze hilo. Waheshimiwa Wabunge, tunatunga sheria nyingine ambazo zinawaumiza sana watu. Kuna watu kule wamekutwa na msokoto mmoja wa bangi, siungi mkono hoja ya bangi, lakini wanafungwa miaka 30. Kuna watu wamekutwa na mirungi kifurushi kimoja wanafungwa miaka 30. Ukienda Kenya, mirungi ni biashara halali. Hebu tujiangalie katika sehemu ya dunia, tuko wapi katika kusimamia mambo haya ili kuhakikisha kwamba tunapotunga sheria, tusitunge kwa ushabiki, tutambue kwamba zinawaumiza sana watu na Bunge linalaaniwa sana katika Magereza zetu zote kwa sababu halisimamii utoaji wa haki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, nizungumze suala la utawala la bora, yote haya nayazungumza katika mwamvuli wa utawala bora. Mheshimiwa Mkuchika wewe ni Waziri mzoefu sana, mnajua kwamba Vyama vya Siasa vimeruhusiwa kufanya kazi katika nchi hii katika misingi ambayo ni ya kweli kabisa. Jambo hili limezungumzwa na wengi, mimi kama Kiongozi wa Upinzani nilizungumze kulisisitiza. Ukiulizwa Serikalini, hivi mmezuia kazi za Vyama vya Siasa, kwa sheria gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mnaona sifa kutangaza kwamba tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwishoni mwa mwaka huu; mnaona sifa kusema tutashinda uchaguzi wa mwaka ujao, wakati mnazuia Vyama vya Siasa visifanye kazi zake za Kikatiba. Hivi vyama ambavyo havina Wabunge,

havina Madiwani, vitajitanua vipi? Vitaeleza vipi sera yake viweze kushiriki uchaguzi wa mwaka ujao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ya siasa ni maisha yetu ya kila siku. Mnazuia Mikutano halafu mnakuwa *proud* kwamba tunawashinda Wapinzani. Mnaogopa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hofu hii, unaiona hofu katika Taifa, watu wanaogopa. Leo nimekutana na msafara wa Mheshimiwa Rais, nimeogopa, nini kinaendelea nchi hii? Ni lazima Rais wetu alindwe, nakubali; na sipuuzi kabisa umuhimu wa ulinzi wa msafara wa Rais, lakini ukiangalia uzito wa ulinzi wa ule unaona kwamba hata hawa wanaomchungu Rais wanagundua kwamba kuna tatizo mahali. Kwa hiyo, ulinzi unawekwa wa ziada sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msururu wa magari karibu 80, helikopta ziko angani. Sasa unajiuliza, ile nchi yetu ya amani na utulivu tumegeuka tena! Kile kisiwa chetu cha amani na utulivu kinakuwaje sasa? Tulizoea kuona viongozi wetu wakiwa huru, wakiwa wana-*mix* na watu wetu bila hofu yoyote, lakini kwa namna mambo yanavyokwenda sasa, tunaona kuna tatizo kubwa la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali na Mheshimiwa Waziri atupe kauli, ruhusuni tukafanye kazi ya siasa. Msiwe marefarii na wakati huo huo mkawa wachezaji. Mnatufunga mikono halafu mnaringa hapa! Ruhusuni tufanye mikutano ya siasa, tukutane kwenye majukwaa ya wananchi tukaone haki iko wapi? Hilo ni jambo moja ambalo ningependa sana kulizungumza kwa sababu naona tuna-*restrict* sana *democracy*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo nizungumzie Tume Huru ya Uchaguzi. Hoja ya Tume Huru ya Uchaguzi imezungumzwa kwenye Bunge hili tangu mfumo wa Vyama Vingi umerudi kwa mara ya pili mwaka 1992, hakuna mwaka unapita Tume Huru haizungumzwi. Mnaogopa Tume Huru ya kazi gani? Tume Huru ndiyo inatupa misingi ya utawala bora, tunapata viongozi ambao wametokana na utashi wa

wananchi, kila kiongozi anayeingia ndani ya Bunge hili ajione yuko *proud*, akiwa wa CCM au wa Upinzani ajione yuko *proud* kwamba amechaguliwa katika uchaguzi ambao ulikuwa huru na haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mnakwenda kwenye uchaguzi na Tume yenu, Mheshimiwa Rais ambaye naye mdau; kuna *conflict of interest* hapa, anamchagua Mwenyekiti wa Tume, anachagua Makamishna, anawachagua Watendaji wake, anachagua Wakurugenzi ambao wanatokana na Chama cha Siasa, kitu ambacho Sheria ya Utumishi wa Umma inakataza. Hatuheshimu tena sheria wala katiba yetu, tunalipeleka Taifa hili wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunapendekeza *very strongly* kwamba ni wakati muafaka sasa, kama tunataka amani *sustainable* katika Taifa hili, tutafakari suala la kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi. Tusiubiri tuingie kwenye machafuko kama Mataifa mengine, halafu tukajiona kwamba tumeingia kwenye machafuko kwa sababu hatukujua tunafanya nini? Ningependa... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbowe. Mheshimiwa Mlinga atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Kingu ajiandae.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nianze nyuma niende mbele. Naomba nianze na hilo la Tume ya Uchaguzi kwa sababu limeongelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mwanasheria na Katiba ya mwaka 1977 na marekebisha yake yaliyofanywa mara kwa mara, wewe ulihusika. Tume ya Uchaguzi imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 74 1(a). Katiba imeelezea Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi anapatikanaje; japokuwa anachaguliwa na Rais, lakini (a) inasema,

“Mwenyekiti ambaye atakuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani, au mtu mwenye sifa ya kuwa Wakili na amekuwa na sifa na hizo kwa muda usiopungua miaka 15.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kipengele (b) kimetaja “Makamu Mwenyekiti,” naye, hivyo hivyo atakuwa Jaji wa Mahakama Kuu na sifa ambazo zinafanana. Wajumbe wengine watachaguliwa kwa mujibu wa sheria ambazo zimetungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 74(3) imetaja watu wafuatao ambao hawataweza kuwa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi; imetaja Waziri au Naibu Waziri, Mbunge, Diwani, kiongozi yeyote wa chama cha siasa. Sasa hawa wamewekwa kwa mujibu wa Katiba na wamewekwa na sifa. Hapa tumeona wapinzani wakiwasifia Majaji. Mfano, Jaji Rumanyika wamekuwa wakimsifia, sasa wangewekwa sifa sawa na walizochaguliwa Wakurugenzi hawa sio wangesema makada wa CCM au wanataka watumie mfumo gani kuwapata? Wangesema waje humu tuwapigie kura si bado tungewachagua hao hao wa CCM maana yake Wabunge wa CCM ni wengi.

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wanataka wajumbe wa namna gani wachaguliwe kuwa...

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuzungumza. Tunavyosema Tume Huru ya Uchaguzi, tuna maana tume ambayo baada ya kuchaguliwa hata angekuwa ni Mheshimiwa Mbowe na Mheshimiwa Zitto ndio Makamishna au ndio Mwenyekiti na sijui nani wa tume kwa muundo uliopo hiyo tume haiwezi kuwa huru kwa sababu

hiyo ina watumishi wengine wa kuazima kwenye TAMISEMI ambao msingi wao wa uteuzi ni makada na ushahidi upo na hawawajibiki kwa tume, wanawajibika kwa wale waliowaajiri ambao ni makada vilevile. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlinga unasemaje kuhusiana na taarifa hiyo?

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa kwa sababu namuheshimu nitaendelea. Tume hiyo hiyo ambayo wanailaumu wanasema si huru, katika majimbo 262, mwaka 2015 CCM imechukua majimbo 188, *CUF* wamechukua majimbo 35, CHADEMA wamechukua majimbo 34, *NCCCR* moja, *ACT* moja, Mheshimiwa Lowassa ambaye alikuwa mgombea wa UKAWA amepata kura milioni sita, Mheshimiwa Magufuli amepata kura milioni nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume hiyo ambayo siyo huru kuna Wabunge kama Mheshimiwa Halima Mdee ni mara ya pili anaingia Bungeni, Mheshimiwa John Mnyika anaingia mara ya pili, Mheshimiwa Sugu anaingia mara ya pili, Mheshimiwa Zitto mara ya tatu tena kabadilisha na majimbo bado kashinda, Mheshimiwa Mbowe mara ya pili, Mheshimiwa Selasini mara...

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo tume ya namna gani ambayo wao wanaitaka, hao watu wangeingiaje

MWENYEKITI: Taarifa

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa poyoyo kwamba mimi kuingia mara mbili mara ya kwanza walikufa watu wawili...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sugu, hebu futa hilo neno uliloanza kutumia

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuta poyoyo. Mimi kushinda mara ya pili, mara ya kwanza kuna watu walizikwa, vita *brother*, matairi yamechomwa, watu wamelazwa, watu wamepigwa risasi, watu wamekaa hospitali mwaka mzima, unaona wewe. Mara ya pili...

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Mlinga taarifa hiyo unasemaje?

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sishangai kuniita poyoyo kwa sababu umesikia mwenyekiti wake ametetea bangi kwa hiyo sio suala la kushangaa...

MHE. ALLY S. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwenye mada. Naomba nitoe pongezi sana kwa Mheshimiwa...

MHE. ALLY S. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilindie muda wangu.

MHE. ALLY S. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

WABUNGE FULANI: Kaa chini wewe, kaa chini wewe.

MWENYEKITI: Ukiona nimenyamaza nimeikataa, endelea Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimeitwa poyoyo japokuwa imefutwa, lakini sishangai kwa sababu umesikia Mwenyekiti wake ametetea bangi kwa hiyo sishangai wafuasi wake kutetea mambo ya kijinga.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlinga naomba ukae. Sasa naku-*address* wewe Mheshimiwa Mlinga. Nakuomba sana ile kauli ya kumuhusisha kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwamba ameruhusu bangi, naomba uifute tu hiyo, uendeleo kuchangia, futa kauli hiyo.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nafuta hiyo kauli na naendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa TAMISEMI...

MWENYEKITI: Nimekataa taarifa *please*.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Jafo ameitendea haki Wizara hii. Wizara hii ni kubwa sana na ina bajeti kubwa mno lakini ameitendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Ulanga naomba nitoe shukrani kwa mwaka wa fedha uliopita tumepata shilingi milioni 117 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya sekondari ya Celina Kombani tumepata

milioni 400 kwa ajili ya uboreshaji wa kituo cha afya cha Lupilo, tumepata milioni 214 kwa ajili ya umaliziaji wa maboma, tumepata ujenzi wa shule na madarasa zaidi ya milioni 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata pikipiki 19 na gari moja ya ukaguzi wa elimu, kwa kweli kazi inafanyika. Hata hivyo, nina jambo moja la uboreshaji wa kitengo cha ukaguzi. Wizara hii ni kubwa na bajeti yake ni kubwa ambayo inatolewa lakini bado kuna upungufu kwenye ufuatiliaji wa matumizi ya hizi pesa. Kuna kitengo cha *financial tracking* cha TAMISEMI, lakini hiko kitengo kinapata bajeti ndogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CAG anakagua kwa mfano Ulanga, tunakaguliwa kila mwaka lakini CAG wanavyokagua wanafanya *random sampling* yaani kama miradi 10 wanakagua miradi mitatu na wanatoa maksi kwa miradi yote kumi. Binafsi kitengo cha *financial tracking* kilivyokuja Ulanga kilikuta madudu sio ya kurudi nyuma. Kwa mfano tulipanga matumizi ya milioni 75 kwa ajili ya posho ya mkurugenzi ya safari lakini mkurugenzi alitumia posho shilingi milioni 192 lakini *financial tracking* ndio waliogundua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa Ulanga walichukua zaidi ya milioni 760 hawakuzipeleka benki na walizitumia binafsi. Ilifika kipindi watumishi wanaokusanya pesa wanaziweka kwenye akaunti zao binafsi, lakini Kitengo cha *Financial Tracking* ndio kilichogundua haya. Sasa mambo ambayo yalifanyika Ulanga yana-*reflect* halmashauri nyingine yanavyofanyika. Kwa hiyo nashauri Kitengo cha *Financial Tracking* cha TAMISEMI kiwezwe ili kiweze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwa Walimu. Nimekuwa msemaji sana wa Walimu. Walimu bado wananyanyaswa mno, upandishaji wa madaraja umekuwa wa shida, wanapata manyanyaso makubwa kutoka kwa Maafisa Utumishi kwani wamekuwa wazembe katika kufuatilia taarifa za Walimu kwa ajili ya kupandishwa madaraja. Matibabu yamekuwa shida, nilishuhudia kesi moja Mwalimu amesimamishwa kazi kwa kuambiwa mtoro kwa

sababu aliandikiwa *ED* na kituo cha afya cha *private*, lakini wanasema eti vituo vya afya vya *private* haviko kwenye *standing order* mbona sisi Wabunge tunatibiwa Apollo, Apollo iko kwenye *standing order*. Kwa mfano Dar es Salaam kuna Hospitali ya Hindu Mandal na Mwananyamala, sitojitendea haki kama nitaenda Mwananyamala nitaacha kwenda Hindu Mandal. Mbona *NHIF* wame-*credit* hivi vituo vya *private*, kwa hiyo Walimu wote hawa wananyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye posho za Madiwani. Ukimuuliza Waziri swali hapa Bungeni atakwambia Madiwani walipwe posho kulingana na uwezo wa halmashauri lakini kila kukicha TAMISEMI wanatoa waraka...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mlinga kwa mchango wako.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Hapana nimeshakataa hayo, tunaendelea.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo kuna jambo limetokea hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kabla sijaanza kuchangia kwanza niweke rekodi maana naona Wabunge wa CCM wakisimama wanaanza kufanya *reference* kwa chaguzi ambazo zilifanyika 2015

kurudi nyuma. Tuingize kwenye rekodi tu kwamba Marais waliotangulia hawakuwahi kutamka bayana kwamba Wakurugenzi Watendaji ambao wameteuliwa na yeye wasipomtangaza mtu wa CCM watakuwa hawana kazi, hawajawahi kutamka bayana, lakini Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli ametamka bayana na amenukuliwa na vyombo vyote. Kwa hiyo tukisimama hapa tukiongea inabidi wakae wakemee, vinginevyo wataingiza nchi kwenye machafuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niingize kwenye rekodi kwamba Makatibu Mezani mnapunja sana muda wa upinzani. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Kweli hiyoo, kweli hiyoo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama ameongea chini ya dakika saba na hajawa *interrupted*, sisi tulikuwa tunamrekodi hapa tunaomba muwe *fare* kabisa maana yake wote tuna-*deserve* muda wa kuongea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii ambayo ni muhimu sana kwenye mustakabali wa nchi yetu. Tumekuwa...

NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kwa mujibu wa...

MWENYEKITI: Ni kuhusu utaratibu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, umemkatalia *Chief Whip* hapa..

MWENYEKITI: Kwa mujibu wa kanuni gani Mheshimiwa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nirudie kwa mujibu wa kanuni ya 64 kwamba Mbunge hatatoa maneno ya

uwongo katika Bunge. Ninalotaka kusema ni kwamba namwomba mchangiaji aliyekuwa anakaa sasa hivi kwa sababu anamzungumzia Mheshimiwa Rais ambaye tunaamini kwamba anaamini katika uchaguzi na kwa maneno hayo aliyozungumza yaingie kwenye rekodi, ningeshauri yasiingie kwenye rekodi wakati yeye hajaleta uthibitisho wa hayo maneno aliyozungumza Mheshimiwa Rais.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko, endelea kuchangia. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tumekuwa tukishuhudia Mawaziri wanakuja wanaeleza wananchi kwamba uchumi wetu unakuwa kwa asilimia saba, yaani tumekuwa tukieleza uchumi wa nchi unakuwa kinadharia zaidi kuliko kiuhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kabisa taarifa ya Shirika la Fedha Duniani imesema bayana kwamba uchumi wetu unakuwa kwa asilimia nne. Uchumi kukua tunaupima vipi, moja ya kigezo ni kuangalia pia na kiwango cha umaskini cha watu wetu wananchi. Ukiangalia kiwango cha wananchi wa Tanzania awamu hii...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko, wewe ni Mbunge mzoefu sana ili ujenge hoja yako vizuri kuhusiana na ukuaji wa uchumi wa Tanzania kile kinachodaiwa na *IMF* ungelikuwa nacho hapa, unasema hiki hapa nakiweka hapa unaendelea kuchangia.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu ukitaka *document*...

MWENYEKITI: Narudia kama unayo *just lay on the table*, unaendelea kuchangia

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *I will lay it on the table right, I don't have it now, but I will do that.*

MWENYEKITI: *Very good, ahsante.*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi unapimwa pia kwa kuangalia umaskini wa wananchi wetu. Ukiangalia Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na kwamba sikatai lakini imejigemeza sana kwenye maendeleo ya vitu badala ya maendeleo ya watu. Ukiangalia hata kwenye mpango hapa wameainisha bayana kabisa kwamba ili kuweza kufikia uchumi wa kati kichwa chao mojawapo watawekezwa kwenye maendeleo ya watu. Maendeleo ya watu namaanisha elimu, afya, maji, kuhakikisha wanawawezesha wananchi wao kiuchumi kupitia uwekezaji na vitu vingine lakini ukiangalia kiuhalisia Serikali inafanya kwa kiwango kidogo sana katika kuhakikisha kwamba inaweka maendeleo kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye elimu, tumeshuhudia elimu yetu ambayo mmesema mnatoa elimu bure...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Nimeshakataa taarifa Waheshimiwa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia kwamba tumeendelea kuona watoto wetu wanasoma kwa kurundikana wanafunzi 200 wengine wanasoma kwenye miti. Tumeendelea kuona Walimu wakiwa wana-*work load* kubwa kinyume kabisa na uwiano wa mwanafunzi kwa Mwalimu. Tumeendelea kushuhudia ajira hazitolewi kwa Walimu. Tumeona juzi wametangaza ajira 4,000 tu lakini watanzia zaidi ya 91,300 wame-*apply* kwa ajira 4,000 tu ambazo zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, ningepomba kuweka kwenye kumbukumbu, Mheshimiwa Waziri alivyoleta taarifa hapa angetuambia upungufu wa Walimu ni kiasi gani,

lakini ameonyesha tu kwamba Walimu waliopo mwaka jana tumeajiri kiasi fulani, sasa hivi tunategemea kuajiri kiasi fulani. Tusipowekeza kwenye elimu, Taifa ambalo haliwekezi kwenye elimu kamwe halitakaa liendeleo. Haya mambo tunayoyajenga sijui *Stieglers Gorge, SGR*, nimeenda juzi pale Kinyerezi naambiwa hata wale wanaokuja kufanya *maintenance* pale inabidi watoke nje kuja kufanya *maintenance* ya vifaa vile vya Kinyerezi, ina maana vikiharibika mitambo mingine lbebe ipeleke nje hii yote ni kazi, inabidi tuwekeze kwa watu wetu ili waweze kuja kuwa wanahudumia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *statistically* kwa Tarime tu mwaka jana nikiwa gerezani niliona watoto waliofaulu kwenda *form one* wengi wameachwa. Nilitarajia kuona Serikali ingewekeza kuhakikisha kwamba inamalizia maboma yote ambayo yamejengwa na wananchi. Kwa mfano Tarime wananchi walijitolea wakajenga maboma 40 kwa shule za sekondari na tukaandika kuja wizarani ili tuweze kupata fedha, hatukuweza kupata fedha za kumalizia maboma 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika halmashauri za Mkoa wa Mara Tarime Mji na Bunda Mji ambapo mapato yetu ni madogo sana hatukuweza kupata hata senti tano ya kumalizia maboma ili watoto wetu waweze kwenda sekondari na waweze kusoma. Kwa hiyo utanona kwamba kipaumbele cha Serikali ni kuwekeza kwenye vitu badala ya kwenye maendeleo ya watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia kwenye afya ni *the same* hata kama tumejenga vituo mia tatu na kitu. Nashukuru Nkende nimepata kituo kimoja, lakini bado tatizo halimaliziki, tunahitaji kuenga vituo vya afya, tunahitaji mahospitali yawe na dawa, vitendanishi na wataalam, waajiri Madaktari wa kutosha, tunahitaji kuona kwamba Mtanzania mfanyabiashara, mkulima wanakuwa na afya bora kuweza kufanya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema tu kwamba kwa Tarime Mji ile hospitali tunahudumia Rorya, Serengeti na wengine, lakini mnatupa fedha za *basket fund* kama vile ni watu wa Tarime Mji, watu 78,000. Tunaomba mkiwa mnatoa fedha muweze ku-*consider* kwamba tuna *work load* kubwa. Vilevile Daktari wa Kinywa na Meno wa Tarime alifariki lakini mpaka sasa hivi hatujapata *replacement*, wananchi wetu wanahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vitambulisho vya wajasiriamali, wamevizungumzia pamoja na kwamba vimeathiri ushuru kwa maana ya kwa halmashauri zetu mapato yanapungua, lakini nataka nijue zaidi. Hivi vitambulisho tunaambiwa kwamba vimetengenezwa Ikulu, vimetengenezwa na Rais, nataka nijue vitambulisho hivi vimetengenezwa kutoka fungu gani, maana yake sina kumbukumbu kama tulishawahi kupitisha fungu hapa kwa ajili ya kwenda kutengeneza hivyo vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia je, hivi vitambulisho vimefuata Sheria ya Manunuzi ya Umma, Na.7 ya mwaka 2011 na 2016? Je, walishindanisha tenda? Mzabuni ni nani aliyeshinda kutengeneza hivi maana yake mwisho wa siku atakuja atapita *CAG*, halafu itakuja *Audit quarries* tujue. Mbaya zaidi hivi vitambulisho ambavyo wanasema laki sita wanaovitoa ni Ma-DC ambao sio Maafisa Masuuli. Kwa hiyo, hii inaacha maswali mengi sana na wananchi wanasema badala ya Chama cha Mapinduzi kupeleka zile milioni 50 kama walivyoahidi kwa kila kijiji, ila sasa wameenda tena kuwakata wale maskini elfu 20 kujaza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua, je, hivi vitambulisho ni chaka ambalo linakusanya fedha kwa ajili ya uchaguzi mkuu ujao au ni nini? Tunaomba watuondoe huo wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Tarime ni Mji ambao unakua, tunahitaji taa za barabarani, hata Mheshimiwa Rais alivyopita alisema mji ule unakua. Kama ambavyo wameweka Lamadi, tunaomba na Tarime nako waweze

kutuwekea taa za barabarani. Uteuzi wa Wakurugenzi tumeukemea hapa na tutaendelea kuukemea kwa mujibu wa sheria inatakiwa angalau Mkurugenzi anayeteuliwa awe ametumikia kwenye utumishi wa umma angalau miaka mitano, lakini tumeshuhudia wakurugenzi wanaoteuliwa ni makada. Mfano wa juzi tu wa *somebody* Mhagama, alikuwa ni Katibu wa CCM kateuliwa kuwa Mkurugenzi, wanaziua halmashauri zetu kuleta watu ambao hawana, lazima tufanye *succession plan* kwenye halmashauri zetu. Wateue ma-DC ambao ni makada wao lakini kwenye kada ya Ukurugenzi, wazingatie sheria. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Matiko, muda wetu ndio huo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kingu.

MHE. ELIBARIKI E. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako tukufu kwa kunipa nafasi ya mimi kutoa mchango katika ofisi ya Rais TAMISEMI na Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi binafsi naomba ku-*declare* kwamba Mheshimiwa Freeman Mbowe namuheshimu sana kama kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa sababu ni mtu makini nina imani. Hata hivyo, kuna vitu ambavyo kaka yangu Mheshimiwa Mbowe amevizungumza naomba nivitolee ufafanuzi kidogo sana hasa katika suala zima la ulinzi wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ulinzi wa Rais, naomba nieleweke, kwa namna ambavyo Rais wetu amechukua maamuzi katika masuala mazima ya uchumi wa nchi, usalama wa Rais wetu lazima utakuwa kwenye mashaka makubwa kwa sababu ya maamuzi Rais wetu aliyoyachukua. Wewe ni shahidi, Bunge lililopita Mheshimiwa Zitto Kabwe na

timu yake walileta hoja hapa kuna watu walipiga fedha katika masuala ya *ESCROW*, Mheshimiwa Rais Magufuli ameingia madarakani, watuhumiwa wote waliokuwa wamefanya ubadhirifu kwenye mambo ya *ESCROW*, amewakamata, sasa wako magerezani. Kwa kiwango cha fedha zilizokuwa zimeliwa, Rais amekamata watu hawa mnataka kuniambia hawa ma-*Taikun* hawana watu wanaoweza wakaleta *insecurity* kwa usalama wa Rais? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema Serikali inatekeleza miradi ambayo Wazungu wanaipiga vita, *Stiegler's George*, tunakwenda kuzalisha MW2400 za umeme, Wazungu wanapiga vita, Rais kwa ujasiri anatekeleza hilo. Hizi ni ahadi zilifanywa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, jasiri na jemedari Rais wa Awamu ya Tano anayetokana na Chama cha Mapinduzi ameingia madarakani, hajaangalia Wazungu ameangalia maslahi ya nchi, *Stiegler's George* inajengwa, mnafikiri Wazungu wanafurahi? Mnafikiri usalama wa Rais utakuwa sawasawa? Leo tunavyozungumza Rais anajenga *Standard Gauge*, mnafikiri mataifa ya Ulaya wanapenda? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe taarifa, ulinzi wa Rais tena uongezwe mara dufu kwa sababu usalama wa Rais wetu kwa mambo anayoyafanya kwa maslahi ya Taifa hili hatuwezi kuacha usalama wa Rais ukawa katika *stake* kwa sababu tunaogopa kupiga makofi, Wazungu walikuwa wanataka wavae vichupi wakapige picha kwenye *Stiegler's George* kule Ruvu, haiwezekani. Tunaomba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na sisi ndiyo *majority*, ndiyo sauti ya nchi humu Bungeni, ulinzi wa Rais wetu ikiwezekana uongezwe hata mara kumi zaidi kwa sababu usalama wake hauko sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nalotaka kulizungumza ni suala la utawala bora. Mwaka mmoja baada ya kuingia hapa Bungeni tuliona Taifa letu lilivyojaribiwa na hapa mimi nazungumza kwa sababu toka nimemaliza kusoma chuo kikuu sijawahi kufanya kazi mahali popote zaidi

ya kuitumikia Serikali hii. Tumeingia Bungeni hapa kuna mambo mengine Serikali haiwezi kuya-*disclose* kwa sababu ya siri za nchi, Mataifa ya Ulaya kwa kushirikiana na watu ndani ya nchi mmeona kilichokuwa kinatokea kule Rufiji, watu wameuawa Kibiti, ili Taifa kudhihirisha kwamba lina utawala bora, dola ya Tanzania imekwenda kudhibiti upumbavu uliokuwa unafanyika pale Kibiti na nchi imetulia. Nataka niseme katika suala la utawala bora hakuna mahali ambapo tunaweza tukapigia kelele utawala bora, tunafanya vurugu, tuache Taifa letu liwe *torn apart, never shall we allow this.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye michango, moja ya vitu pia ambavyo tunaweza tukavizungumza katika utawala bora ni *equal distribution of national cake*. Nampongeza sana Mkurugenzi wa *TARURA* na timu yake na Mheshimiwa Jafo na timu yake na Mzee wetu Mheshimiwa Mkuchika, toka nimeingia madarakani fedha zilizoletwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwasaidia wapigakura wanyonge, walipa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeletewa fedha shilingi bilioni 1.3 na tumejenga madaraja; tumeletewa fedha za vituo vya afya Sepuka, Ihanja na sasa hivi tuna kituo cha afya kule Iyumbu, yote haya ni mambo ya utawala bora. Zaidi ya hapo, hata kwa Jimbo jirani la kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye amepata matatizo, hapa napozungumza Serikali ya CCM bila kujali hayupo na anaumwa, zimepelekwa fedha vijiji 19 watu wake wanachimbiwa maji. Leo mnataka kusema nini hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Mheshimiwa Esther Matiko anazungumza hapa, Serikali ya CCM hapa napozungumza imemjengea Kituo cha Afya cha Mkende kwa shilingi milioni 400. Hapa tunapozungumza Serikali imemtengoa shilingi bilioni 8 kumjengea soko la kisasa pale kwake Tarime. Hapa tunapozungumza boma lake la Halmashauri amepelekewa shilingi bilioni 2 na shilingi milioni 500 zimeshakwenda. Msije hapa kuwadanganya Watanzania, msije hapa kuudanganya umma, sisi tunachokisema Serikali ya Chama cha Mapinduzi, chini ya Dkt. John Joseph Magufuli inafanya kazi. Nataka niwaambie,

mimi kwenye Jimbo langu Rais alipata asilimia 73 ya kura ya uchaguzi uliopita lakini kwa kazi hizi 2020, Rais anakwenda kuchukua zaidi ya asilimia 95 ya kura. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nitoe rai kwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kingu subiri kidogo, Kanuni gani?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a). Sisi Wabunge ni *taxpayer representatives*, tuko hapa kuidhibiti Serikali namna ya kutumia fedha lakini Mbunge anayechangia sasa hivi anaharibu kwa kuonyesha kana kwamba Serikali inapoleta fedha ni fadhila kwa wananchi. Kwa kusema hivyo tunali-*lower*Bunge, inaonekana kama Bunge tunapewa fadhila na Serikali. Hii ni kupotosha umma na kuharibu utaratibu wa utendaji kazi wa Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umwelekeze ajue kazi ya Bunge ni nini maana kuletewa fedha na Serikali ni kama vile Serikali inatusaidia. Sisi Wabunge tumekuja hapa kusimamia kodi ya wananchi na kodi hiyo ndiyo inaleta maendeleo. Sasa anaposifu tumeletewa, tumeletewa na Wabunge wote hata nakotoka mimi kuna watu wanalipa kodi, mimi fedha hizi sipewi bure. Sasa hebu tukuze kiwango cha Bunge, tunali-*lower* Bunge, tunatia aibu kwa watu, hatuonyeshi kama tumekuja kufanya kazi ya Bunge hapa. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, nadhani ulitaka kuchangia tu lakini Mheshimiwa Kingu anatumkumbusha sisi kama Wabunge yale ambayo yanafanywa na Serikali kupitia bajeti hii bila kujali kama wewe unatoka upinzani au hautoki

upinzani. Serikali inatenda haki kusukuma maendeleo kwa wananchi wake wote na ndiyo hoja yake hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaona, nakataa sana taarifa hizi kwa sababu itapendeza zaidi kama tutatumia vizuri muda wetu kwa kujenga hoja kama anavyofanya Mheshimiwa sasa na kama alivyofanya Mheshimiwa Mbowe. Huko ndiyo kujenga hoja. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Sisi mnatubana muda.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wote hapa tumeangalia muda.

MBUNGE FULANI: Na sisi tunarekodi hii hapa.

MWENYEKITI: *That's not official. (Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, *please*, hawa ni makini sana, nimeona hata mimi hapa.

WABUNGE FULANI: Hakuna, siyo kweli.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakajoka liache hilo lakini nawaomba sana sisi Wabunge tufahamu kwamba tunajenga nyumba moja. Mheshimiwa Kingu endelea.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema sina maana kazi yangu hapa ni kuja kusifu tu lakini upotoshwaji unaofanywa juu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, nikiwa kama Mbunge nayetokana na chama hiki lazima tuje hapa Bungeni tuweze kufafanua ili dunia na Watanzania waweze kujua ni kweli chama chetu na Serikali yetu inatekeleza au haitekelezi. Ndiyo maana nimetoa mfano, Jimboni kwa kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu aliyepata matatizo, hayupo hapa Bungeni lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi imepeleka miradi ya maji katika vijiji

21 na hapa tunapozungumza miradi ya maji inaendelea kutekelezwa. Nimesema miongoni mwa mambo ambayo yanaweza yakaingia katika *components* za *good governance* ni pamoja *equal distribution of resources* na *national cake* na ndivyo Serikali ya Chama cha Mapindizi inavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimalize kwa kusema...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, muda wako umekwisha.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, kidumu Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Tunaendelea.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, Kanuni ya 68(1), tafadhali.

MWENYEKITI: Kanuni ya 28?

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(1) na Kanuni iliyovunjwa ni ya 62(1)(a). Kanuni inasema: "Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo kwenye Kanuni hizi, kila Mbunge anayejadili hoja, ataruhusiwa kusema hivyo kwa muda usiozidi dakika 15".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ilitolewa hoja wakati tunaanza Bunge kwamba dakika zile 15 tuchangie kwa dakika 10. Sasa imekuwa *trend* ya watu wanaokaa hapo

kupunja muda wa Wabunge wa Upinzani wanapochangia.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kinaleta ubaguzi wa hali ya juu na kutufanya sisi tu-*feel* kama *second class*. Kwa sababu hapa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbowe wakati anazungumza ametumia dakika 6.47, *this is very unfair*. Hata kama wakitaka kuthibitisha wenyewe na mimi nimerekodi hapa, *unless* mseme muda wetu ni tofauti na wa watu wengine wanaozungumza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutendeane haki kama Wabunge tulioletwa na wananchi. Tunajisikia vibaya sana mnavyotufanyia hapo, tafadhali sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Tutafika vizuri tu, nikuongoze tu kwenye Kanuni husika. Tuko kwenye Bunge la Bajeti, hoja yako tunahitimisha kama navyotaka kusema mimi sasa hivi lakini mlango wa kuingilia siyo ule uliotumia wewe. Mlango uliopaswa kutumia kufikia hapo hapo ni Kanuni ya 99(12), ili wote tufahamu namna ya kutumia kanuni hizi.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu suala la kuminya muda, mimi nasema hivi, Makatibu hawa ni watumishi wa Bunge na hawategemewi kwamba watakuwa wanaminya muda kwa sababu huyu ni Mbunge wa CCM, CHADEMA au CUF, hapana. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge, hiyo ni kauli nzito sana ya kubagua Wabunge, hakuna *second class* Mbunge humu, twende vizuri tu. Hapa tunalinda muda wenu na ndiyo maana mimi huwa nasema nakulindia muda wako kama nimeku-*interrupt*.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Aron Njeza ajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya uhai na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu lakini nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa sababu ni bajeti yangu ya kwanza nikiwa upande huu lakini hasa kwa sababu ni bajeti ya kwanza tokea limetokea tukio baya sana la kuzama kwa kivuko cha MV Nyerere, nitumie nafasi hii kumwomba Mwenyezi Mungu ampumzishe roho za marehemu wote 228 waliopoteza maisha kwenye ajali ile. Tatu, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa sana anayoifanya kuliongoza Taifa hili na kuwaletoa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Jafo na wasaidizi wake na Mheshimiwa Mkuchika na wasaidizi wake wote. Hakika wanafanya kazi kubwa sana, wanatendea haki Wizara zao na wanawatendea haki wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa kwenye maeneo mawili. La kwanza niombe tutambue kwamba tunaweza kwenda kasi sana kwa maendeleo katika nchi hii kama tutakuwa na Serikali za Mitaa zilizo imara. Kimsingi tunaposema uimara wa Serikali za Mitaa ni kwa sababu huduma zote za kijamii ziko chini ya Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, kama tutaimarisha Serikali za Mitaa, kasi ya maendeleo kama inavyokwenda sasa itakuwa nzuri na itawagusa zaidi wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa mpaka sasa mambo yanaenda vizuri, naipongeze Serikali kwa kazi kubwa sana wanayoifanya kwa mfano Ukerewe kwenye eneo la afya kazi kubwa sana imefanyika, vituo viwili vimepata pesa, vinakamilika. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI lakini nimpongeze zaidi Mheshimiwa Rais kwa sababu baada ya matatizo yale alielekeza pesa zijenge Kituo cha Afya cha Bwisya, kituo kinaelekea kukamilika na

naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu. Tatizo kubwa ambalo napenda Serikali itambue, ujenzi wa vituo hivi vya afya iende sambamba na upatikanaji wa watumishi ili viwe na tija, visikamilike halafu vikashindwa kutoa huduma ile iliyokuwa inatarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la elimu kazi kubwa sana imefanyika kupitia elimu bila malipo, watoto wengi sana wameweza kusajiliwa kwenye shule zetu za msingi. Kusajiliwa kwa watoto wengi kumeenda sambamba na upungufu wa miundombinu kama madarasa. Niipongeze sana Serikali hivi karibuni imejitahidi kuleta pesa kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kwenye eneo letu la Ukerewe kupitia Mfuko wa Jimbo lakini pamoja na wananchi, niwapongeze sana wananchi wa Visiwa vya Ukerewe, tumehamasishana tumejenga maboma zaidi ya 300 kwa ajili ya madarasa, niombe Serikali sasa itusaidie kuezeka madarasa haya. Kwa sababu wananchi wamejitoa sana na Mbunge wao nimejitoa, nimepeleka mifuko zaidi ya 3,000 kwenye shule zetu mbalimbali, basi Serikali itusaidie tuweze kuezeka maboma haya ili angalau watoto wetu wapate madarasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye utekelezaji nimeona kuna wazee zaidi ya 700,000 wametambuliwa lakini katika wazee hao ni asilimia 33 tu ya wazee hawa ndiyo waliopata vitambulisho ili waweze kupata huduma ya afya. Kuna tatizo kubwa sana huko chini, wazee wetu wananyanyasika sana wanapokwenda kupata huduma za afya. Niombe Wizara ya TAMISEMI iweke ukomo wa muda ili Halmashauri zetu ziweze kuwatambua wazee hawa na kupata vitambulisho ili wapate huduma za afya kuliko kuendelea kunyanyasika kama ambavyo imekuwa inatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende eneo la *TARURA*, wamesema Wabunge wengi sana, niwapongeze *TARURA* lakini nampongeza sana Mtendaji Mkuu wa *TARURA* amekuwa msikivu pamoja na changamoto mbalimbali anazokabiliana nazo. Kwa kazi kubwa wanazozifanya *TARURA*

tukizingatia kwamba wana mtandao mkubwa sana wa barabara kilomita zaidi ya 100,000 ni nyingi sana lakini kwa fedha wanazozipata tutaendelea kulalamika. Kwa hiyo, niombe katika bajeti tunayoendelea nayo Serikali ilete pendekezo tuweze kubadili fomula ya ugawaji wa pesa hizi ili *TARURA* angalau waweze kupata asilima 40 au asilimia 50 tuweze kuwapa uwezo washughulikie barabara zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipoanza kuzungumza nilisema juu ya umuhimu wa kuimarisha Serikali za Mitaa na hasa Halmashauri zetu kwa sababu ndipo sehemu ambapo miradi mingi inayowagusa wananchi inasimamiwa. Tunapoongelea Serikali za Mitaa hasa Halmashauri tunaongelea Madiwani na watumishi. Kuna changamoto kubwa katika suala zima la posho kwa ajili ya Madiwani wetu. Hili ni tatizo kubwa sana ambalo linaathiri utendaji wa Madiwani wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni umetolewa mwongozo juu ya posho za Madiwani katika vikao vyetu vya Halmashauri. Madiwani hawa wanafanya kazi kubwa sana lakini wanapokwenda kuhudhuria vikao wanalipwa Sh.40,000 ni fedha ndogo sana. Kwa hiyo, niombe TAMISEMI muangalie upya suala hili ili angalau kuweza kuwajengea kujiamini Madiwani hawa ambao wanafanya kazi kubwa sana ya kusimamia miradi yetu kule chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji, hawa ni watu muhimu sana lakini malipo wanayopata; posho zao za kila mwezi lakini hata baada ya kutoka kwenye nafasi zao wanazotumikia ni kitu gani wanakipata? Nashauri TAMISEMI aingalie eneo hili pamoja na kwamba inawezekana wakawa wengi sana Serikali isiweze kuwalipa wote lakini tuangalie kama inawezekana baada ya kipindi chao cha utumishi kuwe na *package* fulani ambayo wanaweza kuipata ili wawe na moyo wa kuendelea kufanya kazi na kusimamia maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Ukerewe, Mwenyekiti wa Kitongoji analipwa Sh.3,000 kwa mwezi. Tafsiri yake ni nini?

Tafsiri yake ni kwamba kwa siku analipwa Sh.100 kwa ajili ya kusimamia shughuli za maendeleo, inawavunja moyo. Kwa hiyo, niombe Serikali ilianganalie sana suala hili.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mpakate, muda wetu si rafiki.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nitaenda moja kwa moja kwenye hoja ya msingi. Kwanza napenda kuunga mkono kwa asilimia mia moja hoja zote mbili na nitaanzia kwenye TAMISEMI kwa upande wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali yetu kwa kutupatia Jimbo letu la Tunduru Kusini vituo viwili vya afya ambavyo vimejengwa pale Mchoteka na kingine kimejengwa Rukasale. Nasikitika kwa kile kituo cha kwanza cha Rukasale kama Mheshimiwa Waziri alikuwa hana taarifa, bado hakijakamilika mpaka leo kutokana na matumizi mabaya ya fedha yaliyotokana na usimamizi mbovu wa Watendaji wetu. Hii imetokana na kwamba Halmashauri ya Tunduru haina mhandisi ambaye angeweza kusimamia vizuri katika ujenzi wa zile zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukurani hizo, Jimbo la Tunduru Kusini lina Kata 15 na katika Kata 15 tuna vituo vya afya vitatu tu na tuna ahadi ya muda mrefu ya Kituo cha Afya Narasi iliyotokana na Rais wa Awamu ya Nne ambaye aliahidi kujenga kituo cha afya katika eneo lile. Nimeleta swali hili mara tatu katika Bunge lako Tukufu,

nimeahidiwa kupewa pesa lakini hadi leo kile kituo bado hakijajengwa na watu zaidi ya 30,000 wako katika Kata zile mbili ambazo zinakitegemea sana na wapo mbali zaidi ya kilometa 70 kutoka Mjini Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia katika hilo hilo, kulikuwa na ahadi vile vile ya Rais wa Awamu ya Nne ya kutoa gari kwa ajili ya Kituo cha Afya Mchoteka. Jambo hili bado nalo ni tatizo na Halmashauri yetu ina gari chakavu, ukizingatia kwamba Hamashauri ya Wilaya ya Tunduru ina eneo kubwa sana kuliko hata Mkoa wa Mtwara kwa ujumla wake. Kwa hiyo, tuna gari bovu la miaka ya 1980 mpaka leo hii, hatuna gari yoyote ambayo inaweza kusaidia wagonjwa wetu kutoka katika sehemu moja kwenda sehemu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kuzungumzia ni suala la elimu. Katika suala la elimu tuishukuru Serikali kwa kutoa elimu ya msingi bila malipo, lakini kuna changamoto kubwa ambayo imejitokeza katika maeneo yetu hasa katika Jimbo la Tunduru Kusini kwamba watoto wamekuwa wengi, madarasa yamekuwa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababisha watoto wengi kusoma katika darasa moja zaidi ya 100 mpaka 200. Nikichukua mfano katika Shule ya Msingi Tuwe Macho ina zaidi ya watoto 800; Shule ya Msingi Semeni ina zaidi ya watoto 900; Shule ya Msingi Mtina ina watoto zaidi ya 1,000, lakini madarasa yaliyokuwepo hayazidi saba au matano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba katika miundombinu ya shule za msingi iongezwe bajeti ili kuhakikisha kwamba majengo yanajengwa ili watoto wale waweze kusoma katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la watumishi. Kwa kweli tatizo la watumishi limekuwa ni kubwa sana katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru. Tuna upungufu wa wafanyakazi katika

Sekta ya Afya zaidi ya asilimia 65. Katika Sekta ya Elimu zaidi ya asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi za msingi katika jimbo langu zina walimu ambao hawazidi watano na *minimum* ni watatu; na shule hizo ziko kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba. Kwa kweli kwa walimu wale imekuwa ni mzigo mkubwa sana kufundisha madarasa saba wakiwa walimu watatu, wanne au watano. Naomba sana kwa kuwa tuko ndani ya bajeti tunaomba sana watumishi wa Sekta ya Elimu waongezwe ili kuhakikisha kwamba wanaweza kufanya kazi vizuri kwa ajili ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna tatizo la walimu waliostaafu katika kipindi hiki ambacho kikokotoo kipyua kimetengenezwa. Walilipwa kwa hesabu ile ya kikokotoo cha zamani. Wamekuja ofisini kwangu mara mbili mpaka mara tatu, wanasema itakuwaje? Tumelipwa kwa kupunjwa na Rais amesema kikokotoo kitumike kile cha zamani. Walimu hawa wanaulizia watapewa lini mapunjo yao ili waweze kujikimu katika maisha yao ya kustaafu kama ilivyo sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni suala la Makatibu Tarafa. Naishukuru Serikali katika Jimbo kangu la Tunduru Kusini kuna Tarafa tatu, mwaka 2018 tumepata watumishi wote, Maafisa Tarafa watatu. Changamoto waliyokuwanayo, hawana ofisi kabisa. Ofisi za Maafisa Tarafa hakuna kwenye Tarafa zetu. Halmashauri yote ina ofisi moja tu katika Tarafa saba. Kwa hiyo, hawana ofisi, hawana nyumba za kuishi, tunabanana nao humo humo kwenye maeneo yetu ambayo tunaishi. Tunaomba sana, mtengeneze angalau bajeti kwa kuwajali hao Maafisa Tarafa ili waweze kupata Ofisi na nyumba za kuishi waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ambalo napenda nizungumzie ni suala la *TARURA*. Kwa kweli *TARURA* pamoja na kazi nzuri wanayoifanya, tatizo fedha inakuwa ni

kidogo. Kwenye upande wa Jimbo langu la Tunduru Kusini, kuna barabara zina zaidi ya miaka 10 hazijawahi kutengenezwa. Tulitegemea *TARURA* atakuwa ni mkombozi katika kutengeneza barabara zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Lukumbule – Imani – Kazamoyo, kuna barabara ya Mlingoti – Tuwemacho – Ligoma, kuna barabara ya Chemchemi – Namasakata – Liwanga mpaka Msechela, kuna barabara ya Namasakata – Amani – Msechela, kuna barabara ya Nandembo – Mpanji mpaka Njenga, kuna barabara ya Mchoteka – Masuguru – Malumba. Barabara hizi zina zaidi ya miaka saba hazijafanyiwa kazi yoyote. *TARURA* kwa kweli kila unapoonna hesabu yao, ukiangalia kwa sasa wamepewa *1.3 billion* na hizi barabara zina zaidi ya kilometa 455. Kwa hela ile waliyopewa kwa matengenezo ya kawaida tu kwa kweli haitaweza kukidhi haja ya kutengeneza barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana *TARURA* waongezewe pesa ili waweze kufanyia matengenezo barabara zetu ambazo zinatumiwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kulizungumza ni suala la mapato ya Halmashauri zetu. Hapa kuna shida, hasa kwenye mikoa ya kusini; mwaka jana na mwaka juzi tulikuwa tunaenda vizuri, mapato yetu mengi tunapata kutokana na ushuru wa korosho. Bahati mbaya mwaka huu biashara ilivyokwenda, hatukuweza kupata ushuru wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, kwa kutambua kwamba walikuwa na mipango na bajeti zao kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ambayo ilikuwepo kwenye mahesabu, basi Serikali ifanye huruma kuwasaidia angalau ruzuku Halmashauri zile ziweze kukidhi haja ya kuweza kutekeleza ile miradi ambayo ilikuwa imepangwa mwaka 2018/2019. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Oran Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara hizi muhimu, bajeti ya TAMISEMI na bajeti ya Utumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili pamoja na *team* zote mbili, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Wanafanya kazi nzuri na kwa ushahidi kabisa, kwenye Jimbo langu TAMISEMI wamefanya kazi nzuri sana katika eneo la *TARURA*, eneo la Afya na eneo la Elimu. Kwa kweli nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kumpongeza Mheshimiwa Rais naye kwa kazi nzuri iliyotukuka. Amefanya mageuzi makubwa ya nchi hii, amefanya makubwa mno. Ushahidi ni mkubwa pamoja na miradi ya kimkakati kwenye Jimbo langu, ni mambo mengi ambayo ameyafanya na haijawahi kutokea toka enzi za ukoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa suala la *TARURA*. *TARURA* chombo chenyewe ni kizuri sana, lakini kuna tatizo kubwa kwamba *TARURA* haina pesa kabisa. Kwenye Jimbo langu nina mtandao wa barabara usiopungua 1,000. Bajeti tumepewa shilingi bilioni 1.5 ambazo ni kilometa 35 kama sikosei. Kuna madaraja chungu nzima, hayapungui 200. Utamaliza miaka mingapi kukamilisha hiyo kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tungeenda kiuchumi zaidi, tuangalie ni namna gani haya maeneo ambayo ni muhimu yapewe kipaumbele. Unapozungumzia Mbeya Vijijini, unazungumzia kilimo cha nchi hii. Mazao yanatoka kwenye mashamba, lakini hatuna barabara kabisa. Mazao hayawezi kutoka shambani kuja sokoni na vile vile hatuwezi kupeleka pembejeo kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hivi leo, barabara ya kuanzia Songwe Viwandani kwenda Jojo haipitiki kwa vile daraja lilikuwa limeshabomoka. Daraja hilo moja linahitaji zaidi ya shilingi milioni 250. Leo ni mwaka wa tatu wananchi wanasumbuka daraja halijajengwa. Pamoja na maombi maalum, inavyoelekea, tatizo katika bajeti, tuangalie ni namna gani *TARURA* waongezewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine ya kuanzia Kawetere kwenda Ikuwa, barabara ya Irambo kuja lhango mpaka Nsonyanga, barabara za Mbonile mpaka Nyarwerwa. Tuna barabara nyingi mno ambazo ni muhimu na za kiuchumi lakini hazimo kabisa hata kwenye mpango wa bajeti. Kama nilivyosema, kwa bajeti ya shilingi bilioni 1.5 utafanya nini kwenye mtandao kilometa 1,000?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani itatunusuru kwenye barabara? Bila barabara hakuna kilimo, bila barabara hakuna elimu, bila barabara hakuna hata shughuli za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuchangia kidogo katika Wizara hizi mbili ni suala la afya. Napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais na Waziri Mheshimiwa Jafo, wamefanya kazi kubwa mno. Halmashauri ya Mbeya tulikuwa hatuna Hospitali ya Wilaya, tulikuwa hatuna vituo vya afya vya kutosha, lakini wametupatia vituo vya afya vitatu; Kituo cha Afya cha Ikuwa, Kituo cha Afya cha Ilembo na Kituo cha Afya cha Santiria. Vituo hivi vimebadilisha kabisa muundo na huduma za afya katika Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji mahitaji makubwa zaidi. Wananchi wamejenga zahanati, maboma hayapungui 70 ambayo yanahitaji msukumo na bajeti ya Serikali. Pia kuna vituo vya afya vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi; kuna Kituo cha Afya cha Ifupa, wananchi wameshajenga, wametumia karibu shilingi milioni 200. Kwa hiyo, tunaomba tu kama shilingi milioni 200 tuweze kumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kituo cha Afya cha Isuto, nacho kimefikia hatua nzuri, tuna Kituo cha Afya cha Ihoho, Kituo cha Afya cha Maendeleo na Kata ya Tembela. Hivi viko katika hatua nzuri. Kama ikiwezekana, tunaiomba tena TAMISEMI waangalie ni namna gani kwa upendeleo kabisa hivi vituo vipate bajeti ya ku tosha ili tuweze kuvikamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la elimu, napo napenda kupongeza tu kwa vile tumefanya vizuri, Serikali kwa kweli imefanya jitihada na wananchi wenyewe nao wamefanya jitihada kiasi cha Halmashauri yangu ya Mbeya kiufaulu tumefanya vizuri sana. Shule zimefanya vizuri na wananchi wameweza kufungua shule tatu ikiwemo moja ya *high school* na shule moja ya wasichana ambayo ni ya bwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ni mengi. Sasa ukiangalia tuna wanafunzi karibu 70,000, walimu tulionao ni 1,035, angalia *gap* hiyo. Pamoja na jitihada za wazazi, bado tunahitaji walimu ili waweze kuinua uchumi wa vijana wetu. Kuna shule ambayo ina mwalimu mmoja, inaitwa Ilindi. Hii shule ina wanafunzi karibu 300, mwalimu mmoja. Kimaajabu ile shule imefaulisha watoto na ikapata nafasi nzuri. Kwa mshangao wa kila mtu akauliza, itakuwaje shule ya mwalimu mmoja, madarasa saba ikafausha kuliko shule zenye walimu wengi? Tukagundua kumbe hata wazazi nao wanashiriki kwenda darasani kufundisha watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hali kama hii nafikiri siyo nzuri sana. Ili tuweze kushindana na wenzetu, inabidi elimu yetu nayo iwe nzuri, tufanye vizuri katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda nichangie kidogo, ni suala la uendelezaji wa miji na mipango miji. Kwa sisi ambao tunazunguka majiji, majiji sasa hivi yamejaa na watu wengi ujenzi unakuja kwenye vijiji vyetu ambavyo havijapimwa. Kwa hiyo, tunaongeza *squatters* zile ambazo tulizikuta. Sasa hivi *squatters* zinahamia kwenye Halmashauri ambazo zinaizunguka Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ijaribu kuangalia iwe na mkakati wa kuhakikisha kuwa vijiji vyote ambavyo vinazunguka majiji, vipimwe, viwe katika mpangilio mzuri na yale maeneo ambayo yapo mijini kama maeneo ya *Tanganyika Parkers*, haya yagawiwe kwa wananchi. *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Wageni.

Kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga ambao ni Madaktari na Wauguzi wa Hospitali ya Bwagala iliyopo Mvomero Mkoani Morogoro ambao ni Ndugu Eva Kisimbo, Ndugu Irene Kuhanga, Ndugu Mathias Suhi na Ndugu Slam Mganga.

Katibu wa Bunge anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho tarehe 13 Aprili, 2019 kutakuwa na usafiri wa mabasi hapa Bungeni kwa ajili ya kuwapeleka Waheshimiwa Wabunge kwenye sherehe za uzinduzi wa Mji wa Serikali huko Mtumba. Mabasi yatakuwa

katika maeneo ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote wanaotaka kwenda; na tunaombwa wote twende, muwe mmefika hapa Bungeni saa 12.00 asubuhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii fupi niweze kuwataarifu rasmi Waheshimiwa Wabunge kwamba Jumapili, tarehe 14 mwezi wa Nne mwaka huu, vijana wetu wa *Serengeti Boys*, Timu ya Taifa chini ya umri wa miaka 17 wanaingia Uwanja wa Taifa kupambana na wenzao kutoka Taifa la Nigeria. Ni mchezo mkubwa katika historia ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni siku ya *weekend*, ingekuwa ni siku ya kazi ningeomba pengine Kamati yangu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pengine niombee kwa Spika, lakini kwa kweli kwa siku ya *weekend* naomba tu Waheshimiwa Wabunge wote tuweze kufika uwanjani kuona kiwango cha soka ambacho Tanzania tumefikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kama nitaweza pengine kupitia kwa Mheshimiwa Ngeleja, *star* wetu hapa wa michezo Bungeni, kupata majina ya Waheshimiwa Wabunge wote ili niweze kuweka utaratibu mzuri wa Waheshimiwa Wabunge kuacha magari mjini, nikawatafutia gari au basi la kuwapeleka uwanjani na vile vile kuwarudisha ili kuepuka fujo ambazo zinaweza kuwapata maana msongamano ni mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba niwatangazie kwamba viingilio ni rafiki sana, ni shilingi 2,000 kwa viti vya kawaida na shilingi 5,000/= viti vya *VIP* ili Watanzania wengi waweze kuingia na vile vile watoto wote wa shule ni bure. Watoto wa Shule za Msingi mradi wameongozwa na mwalimu wao, wataingia bure. Watoto

wa Shule za Sekondari lazima waje na vitambulisho vyao vya shule ili waweze kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kwamba Waheshimiwa Wabunge tuweze kufika kuwasindikiza watoto wetu kwa kuwashangalia. Mgeni rasmi atakuwa ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mwongozo wa Spika kuhusu hoja ya tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya mapato ya Serikali na makusanyo na *re-allocation* ya shilingi bilioni 976.96 iliyoibuliwa na Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi katika majadiliano yetu ya Mkutano huu wa 15 unaoendelea wa bajeti wakati wa kujadili hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora). Mheshimiwa Mnyika, Mbunge, alipata nafasi ya kuchangia, katika mchango wake, pamoja na mambo mengine, alizungumzia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG, ya mwaka 2016/2017, kuhusu hoja ya tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya mapato ya Serikali na makusanyo yake.

Katika mchango wake, alieleza ifuatavyo, nanukuu; *“Ripoti ya mwaka uliopita iliibua suala la 1.5 trillion ambayo baadaye ilipanda mpaka kuwa 2.5 trillion. Katika ufafanuzi wa Serikali juu ya triloni 1.5, kuna taarifa zilitolewa toka triloni 1.5 mpaka triloni 2.4, kwamba shilingi bilioni 976.96 zilihamishwa kwenye mafungu mbalimbali zikapelekwa ku... kwa maana ya bajeti reallocation.”* Mwisho wa kunukuu.

Aliendelea kueleza kuwa, yeye kama Mbunge anaamini kuwa, Bunge halikuridhia *reallocation* ya shilingi bilioni 976.96 kupelekwa Fungu namba 20. Nilitoa ufafanuzi wa hoja hiyo kwamba suala la *reallocation* huzingatia utaratibu uliowekwa na Sheria ya Bajeti, Mbunge anaweza

kuhoji pale ambapo kiwango cha *reallocation* kimezidi kiwango kilichowekwa kwa mujibu wa sheria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo, Mheshimiwa Mnyika aliibua hoja nyingine kutaka Serikali kutoa mchanganuo wa namna shilingi bilioni 976.96 zilivyotumika. Alieleza, nanukuu; *"Ili tuondoe utata kuhusu jambo hili la shilingi bilioni 976.96, Ofisi ya Rais ikija kwenye majumuisho hapa itueleze hizi shilingi bilioni 976.96, Ikulu zilitumika kwa matumizi yapi, tupewe mchanganuo wa kina."*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo ya Mheshimiwa *Good luck* Mlinga, Mbunge, alihoji uhalali wa Mheshimiwa Mbunge kuhoji suala la *1.5 trillion*, wakati Kamati ya PAC ilikwishatoa taarifa na kueleza kwamba tofauti hiyo ya *1.5 trillion*, haikuwepo baada ya marekebisho ya maheshabu kufanyika. Aliendelea kueleza kwamba suala hilo linaendelea kuzungumzwa ili kuichafua Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, niliahidi kupitia Taarifa Rasmi ya Bunge (*Hansard*) ya Kikao cha leo, nilifanya hivyo na nimejiridhisha kuwa Mheshimiwa Mnyika, Mbunge alikuwa anajadili suala ambalo Kamati ya PAC ilikwishalitolea ufafanuzi, ambapo katika Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2018, katika ukurasa wa 35 ambapo ilibaini na kueleza kuwa hapakuwepo na tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya mapato ya Serikali na makusanyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, baada ya marekebisho ya hesabu kufanyika na nanukuu; *"Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha suala la tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya mapato ya Serikali na makusanyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naomba kuweka kumbukumbu sahihi katika Bunge lako tukufu kuwa tofauti hiyo haikuwepo baada ya marekebisho ya hesabu kufanyika."* Mwisho wa kunukuu.

Baada ya hapo Bunge liliazimia na kuthibitisha kwamba hakuna tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya makusanyo na mapato ya Serikali katika Mfuko Mkuu kwa

mwaka wa fedha 2016/2017, angalia ukurasa wa 73 wa taarifa ya PAC.

Waheshimiwa Wabunge, wakati akianza kuchangia tena Mheshimiwa Mbunge Mnyika, aliongelea suala la *1.5 trillion*, ambazo zilipanda mpaka *2.4 trillion* na kusema kuwa bilioni 976.96 zililhamishwa kwa njia ya *reallocation* kwenda Fungu namba 20.

Waheshimiwa Wabunge, unapoongelea suala la tofauti ya shilingi trilioni 1.5 na trilioni 2.4 pamoja na *reallocation* ya shilingi bilioni 976.96, unakuwa unaongelea kitu kimoja. Jambo hili tayari Bunge lilikwishalitolea uamuzi tarehe Mosi Februari, mwaka huu, wakati kiti kilipojibu Mwongozo wa Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), aliyehoji kuhusu uhalali wa mchango wa Mheshimiwa Catherine Ruge, aliyedai kuwa kwenye Taarifa ya CAG kuna *reallocation* ya shilingi bilioni 997 na mchango wa Mheshimiwa Anatropia Theonest, aliyedai kwamba kiwango kilichopotea ni zaidi ya triloni mbili.

Uamuzi uliotolewa na kiti ni kwamba, suala hilo haliruhusiwi, kwa kuwa, ufafanuzi ulishatolewa na CAG na Kamati ya CAG kuhusu kutokuwepo tofauti hiyo ya shilingi trioni 1.5 kati ya mapato na makusanyo ya Serikali. Kiti kiliamua kuwa, mchango wa Mheshimiwa Ruge na Mheshimiwa Anatropia Theonest, uondolewe kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge (*Hansard*).

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 53(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, inakataza kujadili jambo ambalo lilikwishaamuriwa na Bunge katika mkutano uliopo au uliotangulia, nanukuu; *“Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo ambalo Bunge lilikwisha kuliama ama katika mkutano huo uliopo au ule uliotangulia,isipokuwa kwa kufuata masharti ya Kanuni hizi...”*

Vilevile Kanuni ya 64(1)(c), inazuia kujadili jambo lililokwishaamuriwa na Bunge iwapo hakuna hoja mahususi

iliyotolewa na kanuni hiyo inasema; *“Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye mkutano uliopo au uliotangulia na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahususi na vilevile hatapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge, isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahususi inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya;”*

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na uamuzi huo na masharti ya Kanuni hizo mbili nilizozitaja, naelekeza kwamba suala hilo lisiendeleo kujadiliwa Bungeni na naelekeza kwamba mchango wa Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge kuhusu hoja ya shilingi trilioni 1.5 na *reallocation* kuhusu suala hilo ifutwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Huo ndiyo mwongozo wangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuruni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa siku ya leo, kwa michango yenu na nimeshatoa matangazo. Tujitahidi kesho mapema saa kumi na mbili, wale ambao, itapendeza kama tutachukua usafiri ambao Bunge limetoa kwa sababu ya nafasi kule tunakokwenda itakuwa finyu kwa magari binafsi. Kwa hiyo, sina la ziada, kwa maana hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, wiki ijayo saa tatu asubuhi.

(Saa 1.50 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 15 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)